MTUME WA REHMA MUHAMMAD ﷺ

Matukio yenye kusisimua katika maisha yake

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Istanbul - 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

MTUME WA REHMA
MUHAMMAD ﷺ

Othman Nuri Topbash

Jina la Asili : Rahmet Peygamberi'nden Rahmet Esintileri

Mwandishi : Othman Nuri Topbash

Msimamizi Mkuu : Abdi Mohamed Adam

Mfasiri : Ibrahimu H. Kabuga

Mhariri : Aziza A. Ngume

Msanifu jalada : Sarkhan Isgandarov

Kupangiliwa vizuri na Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov

ISBN: 978-9944-83-685-2

Mchapaji: Erkam Printhouse

Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi Mah.
Atatürk Bulvarı, Haseyad 1. Kısım No: 60/3-
C Başakşehir, Istanbul, Turkey

Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748

Barua pepe: info@islamicpublishing.org

Tovuti: www.islamicpublishing.org

Language : Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

MTUME WA REHMA

MUHAMMAD ﷺ

Matukio yenye yenye kusisimua katika maisha yake

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

YALIYOMO

NENO LA MFASIRI 7

FAHARI YA ULIMWENGU 11

Ujio Wake ni Heshima kubwa kwa Ulimwengu..... 14

MAISHA YA MFANO NA NAFASI YAKE KATIKA MITUME 45

Mtume (s.a.w) kama alivyotazamwa na makafiri 63

SIFA NA TABIA ADHIMU ZA MTUME WA REHMA (S.A.W)..... 75

Usafi wa Moyo wa Mtume wa Rehma (s.a.w) 78

Unyenyekevu wa Mtume wa Rehma..... 97

Staha, Huruma na Uungwana katika Maisha ya Mtume wa Rehma 104

Mwenendo wa Mfano kwa Watu 109

Staha na Adabu za Mtume wa Rehma (s.a.w) kwa Masikini 114

Jinsi Mtume wa Rehma alivyoilea jamii
Hatua kwa Hatua 126

Muamala wa Mtume wa Rehma (s.a.w)
kwa Wanawake 129

Muamala wa Mtume wa Rehma Kwa Wanyama 132

Muamala wa Mtume wa Rehma kwa Yatima 136

Wosia wa Mtume kuhusu Haki za Majirani 138

Muamala wa Mtume kwa Wahalifu
na Mateka wa Vita 139

Muamala wa Mtume kwa Maadui na
Wasiokuwa Waislamu. 140

Msamaha wa Mtume (s.a.w) 141

Ukarimu wa Mtume (s.a.w) 146

Ukarimu wa Maswahaba 147

Ikhlasi, Uaminifu na Uadilifu wa Mtume (s.a.w) 151

Hayaa za Mtume (s.a.w) 152

Uungwana wa Mtume (s.a.w) 154

Uwajibikaji Wake 157

HITIMISHO 165

BIBLIOGRAFIA 181

NENO LA MFASIRI

Nilipoambiwa nitafsiri kitabu hiki kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili, nilisita. Lakini, baada ya kukisoma kwa umakini, nilihamasika na kushawishika kuwa Waislamu na Wasiokuwa Waislamu wanaozungumza Kiswahili watafurahia na watanufaika kwa kujifunza kipengele muhimu cha maisha ya Mtume (s.a.w) ambacho kwa kawaida kimekuwa kikipuuzwa - kwa kukusudia au kwa kutokusudia. Kipengele kinachoelezwa na kukusudiwa katika kitabu hiki ni huruma ya Mtume (s.a.w), ambayo bila shaka, ndiyo nara (kauli mbiu) mashuhuri na maarufu ya maisha yake yote. Leo hii, Waislamu na wasiokuwa Waislamu wanahitaji kujua kuwa katika historia yote hakuna mtu yeyote anayeweza kuwa na huruma iliyojidhihirisha katika maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w). Wanatakiwa wajue kuwa mfano wake ni muhimu sana, hasa katika ulimwengu uliotawaliwa zaidi na choyo, ubinafsi na mitindo ya maisha ya kimaada. Kitabu hiki ni wito wa kuielekea Rehma katika uhusiano wetu wa kijamii na pia maingiliano yetu na mazingira kwa kuyatathmini upya maisha ya mfano ya rehma hii iliyoletwa kwa wanadamu wote, Mtume Muhammad (s.a.w) .

Kitabu hiki ni utangulizi mzuri juu ya maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w), kilichoandikwa na Mwandishi maarufu wa Kituruki ambaye amejitolea maisha yake kwa kujifunza,

kufanyia kazi, kuyaeneza na kuyasambaza mafundisho ya Mtume (s.a.w). Mwandishi amewafungulia dirisha la staha wale wote wanaotamani kuyatazama maisha ya mtu ambaye, leo hii, kiigizo na mfano wake unafuatwa na moja ya tano ya wakazi wote ulimwenguni. Hakuna mtu yeyote katika historia ya mwanadamu ambaye amekuwa na athari na kuacha taathira kwa wanadamu na historia ya binaadamu kama Mtume Muhammad (s.a.w). Aliwaongoza watu katika moja ya dini kubwa kabisa ulimwenguni, akaweka msingi wa moja ya staarabu za hali ya juu kabisa kuwahi kushuhudiwa na ulimwengu katika zama za uhai wake. Lakini, kwa mujibu wa mwandishi, haya sio sifa kuu zaidi za maisha ya Mtume (s.a.w). Bali, kitabu hiki kinaeleza kuwa ukuu na Utukufu wa Mtume (s.a.w) umetokana na ukweli kuwa alileta kanuni za kimaadili za hali ya juu kabisa katika kila kipengele cha maisha yake na mahusiano ya kijamii. Aligusa mioyo ya mafukara, masikini na wanyonge; alifanikiwa kuwanyanyua watu hawa hadi kuwa walimu kwa wanadamu wote, katika kipindi kile na kipindi chote kijacho. Upendo wake, huruma yake, na Rehma zake si tu ziliwajumuisha wanadamu, bali pia kwa wanyama na hata sayari. Ni Mtume anayekumbukwa kwa maadili yake ya kiutu na upendo wake kwa viumbe vyote.

Cheo ambacho Mwenyezi Mungu alimpa Mtume Muhammad (s.a.w) katika Qur'an Tukufu ni "Rehma kwa Walimwengu". Ulimwengu wa mwanadamu ni moja kati ya ulimwengu ulioumbwa na Mwenyezi Mungu "Mola wa Walimwengu". Huruma ya Mwenyezi Mungu isiyokuwa na kikomo na ya milele, inayotangazwa na majina ya 'Mwingi wa Rehma' na 'Mwenye Kurehemu', pamoja na majina mengineyo, inajidhihirisha kwa wanadamu kupitia maisha ya Mtume Wake (s.a.w). Huruma hii haikupata kupungua

wakati wa kuifungua Arabia na wakati wa kuwashinda maadui. Kinyume chake, maadui zake walifaidika na Rehma zake katika matukio mbalimbali, kama historia inavyosema. Hakumpiga mtoto, mtumwa, mwanamke, na alipinga vikali na kukataza sana tabia hiyo; pia hakusita kuwapa msaada wale wote waliohitaji msaada wake.

Kumpenda Mtume Muhammad (s.a.w) ni sehemu ya imani katika Uislam. Kama Waislamu wanavyotakiwa kumpenda Mwenyezi Mungu, ndivyo hivyo hivyo wanatakiwa kumpenda Mtume Wake (s.a.w). Bila upendo huu, imani haitakubalika. Na upendo wao kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake unatakiwa uzidi mapenzi yao na kitu kingine chochote. Waislamu wanaonesha upendo na heshima zao kwa Mtume Muhammad (s.a.w) kwa kumtukuza pale ambapo jina lake linatajwa kwa kusema : *S. a. w,* au kwa kiarabu *sallallahu 'alayhi wa sallam*. Hii ni sehemu ya adabu katika uhusiano wao na Mtume (s.a.w). Muumini anapojifunza juu ya maisha yake, moja kwa moja upendo huu hustawi ndani ya moyo wake, na kuusikia kikamilifu. Mwandishi, Othman Nuri Topbash, kwa sasa anaishi Istanbul. Amepata elimu ya kisasa na ya kimapokeo. Ameandika vitabu vingi tofauti vinavyohusu vipengele vya Uislamu kama dini na ustaarabu. Mada ambayo imekuwa ikijirudia sana katika vitabu na maandiko yake ni kuhusu umuhimu wa huruma, upendo na ukarimu katika uhusiano wetu wa kijamii kama msingi wa njia sahihi ya maisha ya Kiislamu. Kitabu hiki, ambacho kimeandikwa katika mazingira ya upendo kwa Mtume Muhammad (s.a.w), kinaakisi Rehma hii, huku kikijadili tabia adhimu kabisa za mfumo wa maisha ya Mtume (s.a.w) na maadili yake. Kinakusudia kuwaongoza watu katika ukarimu na kuutakasa moyo, hivyo kinalenga kuwasaidia

kupata furaha duniani na akhera. Habari zilizoandikwa katika kitabu hiki zimekusanywa kutoka katika vyanzo vyenye kutegemewa sana na vya wasomi wa zamani, ambavyo vimewekwa katika eneo la tanbihi. Kauli za Mtume Muhammad (s.a.w) zimetolewa katika vitabu sahihi na vitabu vya hadith. Kwa wale wanaotaka maelezo zaidi, yanapatikana pia katika vitabu vya kiarabu ambavyo vimetajwa.

Nina hamasa kubwa, kuwa kitabu hiki kitaziba pengo lavitabu kuhusu Mtume Muhammad (s.a.w) kwa kuelezea upande wa maisha yake ambao umesahauliwa. Katika ulimwengu ambao umetawaliwa na hitajio la mazungumzo baina ya staarabu na dini mbalimbali, rehma ndicho kitu tunachokihitaji zaidi. Wito wa Mwenyezi Mungu unaotutaka tuielekee rehma kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w) unatakiwa kutoa mwangwi ndani ya mioyo ya wenye kufuata nyayo zake. Hamna njia nzuri ya kupata Rehma zaidi ya kufuata yale yote yaliyofanywa na watu waliochaguliwa na Mwenyezi Mungu kutuongoza sisi wanadamu.

Ibrahimu H. Kabuga



Fahari Ya Ulimwengu

REHMA NA AMANI ZIWE JUU YAKE

“Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa.”

Salamu kwa Muhammad Mustafa, Rehma ya ulimwengu wa binadamu na majini!

Salamu kwa Muhammad Mustafa, mjumbe aliyetumwa kwa ulimwengu wa binadamu na majini!

Salamu kwa Muhammad Mustafa, Imamu wa misikiti miwili MiTukufu ya Makkah na Madina!

Salamu kwa Muhammad Mustafa, babu wa Hasan na Husayn!

Mwenyezi Mungu Mtukufu, ameufunika ulimwengu kwa Rehma zake zisizo na kikomo. Amewapa wanadamu, ambao ni tunda kamili la rehma na huruma yake, daraja ya juu kabisa katika ulimwengu.

Pia nafasi hii ya adhimu haitoshi kwa mwanadamu kuufikia ukweli kwa kiwango anachokitaka Mwenyezi Mungu. Hivyo wakapewa Baraka mbalimbali kutoka kwa Mwenyezi Mungu kama vile akili na muoo. Mbali na Baraka hizo, wakaongezewa zawadi nyingine, katika mfumo wa muongozo uliotolewa na wajumbe wa Mwenyezi Mungu. Hivyo, nguvu hii ambayo wanadamu walipewa na Mwenyezi Mungu, iliandaa njia ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu kwa namna iliyo bora. Kilele halisi cha msaada huu kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni nuru ya Muhammad (s.a.w), ambaye alikuwa

Mtume wa mwisho kutekeleza kazi hii ulimwenguni, na ambaye ujio wake wa kimwili katika ulimwengu wetu kama Mtume ni zawadi kwa wanadamu wote.

Ujio Wake ni Heshima kubwa kwa Ulimwengu

Mtume (s.a.w), ambaye ni kilele cha nyororo ya viumbe, alikuja ulimwenguni siku ya Jumatatu, tarehe 12 ya mwezi wa Rabi al-Awwal, ambayo ni sawa na tarehe 20 ya mwezi Aprili, mwaka 571. Alizaliwa kabla ya jua kuchomoza.

Kwa kuzaliwa kwake, rehma za Mwenyezi Mungu ziliingia kama mafuriko ndani ya ulimwengu. Rangi za asubuhi na usiku zilibadilika. Hisia kuu zikaongezeka. Maneno, urafiki na faraja vilifunguliwa bila kikomo. Kila kitu kilipata maana mpya na kupata furaha mpya. Masanamu yalitikisika na kuvunjika. Huko Madayin, katika ardhi ya wafalme wa Iran, makasri na minara ilivunjika. Maji ya Ziwa Sawa yalitoweka, ziwa lote kukauka, kwa maana maji yenye tope la dhulma na ukandamizaji yalianza kutokomea.

Mioyo ilifurika maji ya Baraka na rehma hii kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Baba yake Mtume alikuwa katika mji wa Damascus kwa sababu za kibiashara na alipokuwa akirejea nyumbani alipita Madina, miezi miwili kabla ya kuzaliwa kwa mwanae.

Kama ilivyo katika desturi za kiarabu, mtoto huyo aliyebarikiwa, aliendelea kubaki chini ya mama wa kufikia, Halima, kwa muda wa miaka minne.

Akiwa na umri wa miaka sita, ili kulitembelea kaburi la mumewe, mama yake Mtume Bibi Aminah alisuhubiana

na Muhammad (s.a.w) na Umm Ayman, kijakazi wa familia hiyo, kwenda Madina. Maradhi yalimkumba Bibi Aminah wakiwa safarini. Alifariki katika eneo lililoitwa Abwa. Malenga mmoja alilielezea tukio hilo kama ifuatavyo:

Ewe Marehemu, uliyelala katika mji wa Abwa!
Lilichanua katika bustani lako
Uaridi zuri zaidi ulimwenguni.. .

Hivyo Muhammad (s.a.w) akawa yatima na kurudi Makkah pamoja na Umm Ayman.

Akiwa na umri wa miaka nane, alimpoteza babu yake, Abdul-Muttalib. Haukupita muda mrefu akampoteza pia ami yake, Abu Talib, aliyekuwa akimlinda kwa moyo wote. Hivyo, wasaidizi wake wa kimaada walikuwa wameondoka duniani. Sasa, Mola wake ndiye pekee aliyekuwa wamebaki kama mlinzi na mwalimu wake. Kwa hakika, alipewa walezi wake hawa wa kibinadamu wake wa kipindi dhaifu kabisa cha maisha yake, kwa hekma maalumu ili awe mfano bora na kamili wa kufuatwa na wanadamu wote.

Maisha yake ya utoto wake na ujana wake kama yatima yalikuwa yamejaa staha, usafi na maadili ya hali ya juu, yaliyoashiria nuru katika maisha yake ya baadaye.

❀

Alipofika umri wa miaka 25, Muhammad (s.a.w) alimuoa Bi Khadijah (r.a) Alikuwa mwanamke Mtukufu na mwenye kuheshimika kutoka katika kabila la Kiquraysh, kabila kubwa katika Arabia.

Bibi Khadijah (r.a) akawa msaidizi mkubwa wa Mtume kwa kujitolea maisha yake na mali zake kwa ajili ya Mtume. Bibi Khadijah (r.a), alimzidi Mtume Muhammad (s.a.w) kwa

miaka kumi na tano, alikuwa ni mjane mwenye watoto. Mtume (s.a.w) alikuwa na uhusiano naye mzuri sana, ambao ni mfano bora kwa ulimwengu wote.

Mtume akipambana peke yake, Bibi Khadijah alikuwa wa kwanza kumsaidia na kumuunga mkono. Kwa mfano Mtume Muhammad (s.a.w) aliposhushiwa wahai kwa mara ya kwanza katika pango la mlima Hira, alishtushwa sana kwa majukumu mazito aliyopewa na Mwenyezi Mungu. Muda huohuo, Mtume alirudi nyumbani akiwa na hofu kubwa.

"Ewe Khadijah!Nani atakaeniamini?"

Mke huyu aliyebarikiwa akamjibu Mtume Muhammad (s.a.w) kwa kusema:

"Naapa kwa Mwenyezi Mungu! Kamwe Mwenyezi Mungu hatakutupa mkono; unawajali ndugu zako, unabeba mizigo ya wale wasioweza kuibeba wao wenyewe, una upendo kwa masikini na unawasaidia watu kupata vile ambavyo hawawezi kupata. Wewe ni mkarimu kwa wageni. Unawasaidia watu katika matatizo yanayowakabili.. . Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nitakukubali na kukuamini. Nilinganie mimi kwanza katika njia ya Mwenyezi Mungu!"[1]

Kwa hiyo Bibi Khadija akawa muumini na mfuasi wa kwanza.

Kamwe Mtume (s.a.w) hakusahau upendo, tabia njema na ukarimu wa Bibi Khadijah (s.a.w). Hata baada ya Bibi Khadijah kufariki, kila alipochinja nyama, alikuwa akiwatumia nyama ndugu wa Khadija (r.a). [2] Mtume alihifadhi kumbukumbu za mambo yote mazuri ya Bi Khadija.

---

1. Bukhârî, *Zakât* 1; Muslim, Îmân 12; Nasâî, *Salât* 10; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad,V, 417, 418.
2. Muslim, *Fadhaâil al-Sahâbah* 75; Ibn Hibbân, *al-Sahîh*, XV, 467.

Miaka 24 ya mwanzo katika ndoa yake, ambacho kipindi cha ujana wake na kipindi cha nguvu nyingi, alikitumia akiwa na Bibi Khadija (r.a). Wakeze wengi aliowaoa baadaye walikuwa wakubwa kuliko yeye na walikuwa wajane. Aliyekuwa bikira na mwanamke mdogo kuliko wakeze wote alikuwa Aishah (r.a). Aishah aliyakamata vyema mambo ya kidini yahusuyo wanawake kwa uelewa na maarifa ya hali ya juu. Baada ya kifo cha Mtume (s.a.w), Aishah aliendelea kuishi kwa kipindi kirefu, a mbapo aliwaelimisha watu, wake kwa waume kuhusu Uislamu. Maarifa hayo baadaye yalikuwa miongoni mwa msingi imara ya fikara za Kiislamu.

Maelezo yafuatayo yanathibitisha jinsi lengo hili lililofikiwa: Abu Musa al-Ashari, moja kati ya maswahaba wakubwa wa Mtume Muhammad (s.a.w) anasema: "Sisi, maswahaba wa Mtume , kila tulipokabiliana na swali kuhusu hadith yoyote ya Mtume tulikuwa tukimuuliza Aishah na kuridhika na majibu anayotupatia."[3]

Sababu nyingine ni kuimarisha urafiki na ukaribu uliokuwepo kati ya Mtume (r.a) na Abu Bakr (r.a), ambaye alikuwa "wa pili kati ya wawili" waliokuwa katika pango la Thawr, kama ilivyonukuliwa ndani ya Qur'an. [4]

Mtume Muhammad (s.a.w) alipandishwa daraja ya utume akiwa na umri wa miaka arobaini baada ya kuishi maisha ya utakatifu na katika familia Tukufu wakati wa ujana wake. Miezi sita kabla ya kutimiza umri wa miaka arobaini, Mwenyezi Mungu Mtukufu alimfungulia pango la Hira, karibu na mji wa Makkah, kama shule ya kiroho.

3. Tirmidhî, *Manâqib* 62.
4. Rejea Qur'an Tukufu, Surah Tawba, 9: 40.

Katika darasa hili la kiroho, ambapo mafunzo na malezi matukufu yaliendelea kwa siri, alifundishwa kuhusu kile kisichodumu na kile kinachodumu. Hatimaye, alipotimiza umri wa miaka arobaini, alipewa nguvu na mamlaka ya kuwaongoza watu na kupewa kibali cha utume kwa amri ya: *"Soma: Kwa jina la Mola wako mlezi aliyeuumba!"* (Qur'an, Alaq, 96: 1-2)

Miezi sita baada ya baraka hii, baraka ambayo inaweza kutambuliwa wale tu wenye akili zenye utambuzi, iliambatana na "ndoto za kweli." Kiuhalisia, pango la Hira ni mfano wa safari ya mbegu iliyo ardhini, mahali pa malezi ya kiroho yatakayoendelea kuwa siri kwa watu daima. Sababu za Mtume Muhammad (s.a.w) kuelekea kwenye pango hilo ni huruma na huzuni kubwa aliyokuwa nayo kwa watu wa zama zake kutokana na mateso na uasi wao. Kwa kweli, hiki kilikuwa ni kipindi cha maandalizi ya kushuka kwa Qur'an Tukufu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kuja kwenye uelewa wa mwanadamu kupitia moyo safi wa Muhammad (s.a.w). Ilikuwa ni kipindi cha kuziandaa nguvu zake dhaifu kubeba mzigo mzito wa wahyi, mzigo ambao mtu wa kawaida hawezi kuubeba. Hatua hii ni mfano wa hatua ya kubadili chuma ghafi kuwa chuma pua; uwezo wa ndani ya chuma hicho huibuliwa kupitia mchakato maalumu. Haiwezekani kuifikiria akili inayoweza kulikaribia shina la siri hii au moyo unaoweza kuipenya na kisha ukawa haujasambaratika na kuwa vipande vipande pindi unapoigusa siri hii.

Wale walioshindwa kuutazama ulimwengu huu kupitia dirisha la moyo ni wale waliokuwa katika kundi lililathirika lililokuwa chini ya bendera nyeusi ya Abu Jahl na Abu Lahab, maadui wakubwa wa Uislamu mjini Makka.

Maisha ya Mtume (s.a.w) yamejaa ishara za kimungu za

heshima, heshima ambayo hawakuipata Mitume wengine waliopita. Yeye pekee ndiye aliyeitwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa cheo cha "kipenzi changu" *(Habibi).* Vivyo hivyo alikuwa ni mtu pekee aliyepata Baraka ya *Miraj* (yaani safari ya kupaa kuelekea mbinguni kwenye arshi ya Mwenyezi Mungu). [5]

Ubora wake ulidhihiri pale alipowaswalisha Mitume wote waliomtanguliza katika ibada kule Yerusalemu kabla ya kwenda *Miraj*. Siri ya *"lan tarani"*[6] katika kipindi cha Nabii Musa (a.s) ilijidhihirisha kama *"qaba qawsayni aw adna"*[7]

---

5. Bukhârî, Salât I; Muslim, Îmân 259; Abû Dâwûd, Sunnah 23; Tirmidhî, Tıb 12; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 224.
6. 6 siri ya *"lan tarani"* (Kamwe hutaniona!) ilikuwa kama ifuatavyo; Nabii Mussa (a.s) aliwekwa katika hatua ya maandalizi ili aweze kuongea na Mwenyezi Mungu. Aliambiwa afunge siku thelathini, kisha akaongezewa hadi ziku arobaini. Kilikuwa ni kipindi cha maandalizi ya kuongea na Mwenyezi Mungu, kipindi cha kumtakasa na kumsafisha Nabii Musa (a.s) dhidi ya matamanio ya kihayawani. Nabii Musa (a.s) hakuongea na Mwenyezi Mungu katika njia ya kijawhari (kimaada), au ya kawaida, bali ilikuwa kupitia sifa thabiti ya kimungu ya *Kalaam*. Hamna yeyote aliyesikia maongezi hayo, hata malaika Jibril hakusikia hata mashuhuda sabini walioandamana na Nabii Musa (a.s) hawakusikia. Hata hivyo, Nabii Musa (a.s) alizimia kutokana na ishara hii ya kimungu. Alishindwa kuelewa kama alikuwa katika ulimwengu huu au Mbinguni, akahisi kubanwa na sehemu na wakati. Kutoka na kuzama katika upendo na uchaji, alipata shauku kubwa ya kumuona Mungu. Ndipo Mwenyezi Mungu akamjibu: "lan tarani" (kamwe hutaniona!). Lakini Nabii Musa (a.s) akiwa katika hali hii ya nusu-ufahamu, aliendelea kusisitiza kuwa anataka kumuona Mungu, Mwenyezi Mungu akamwambia aangalie mlimani. Alimwambia Musa kuwa kamamlima ule utaweza kuhimili ishara ya Mungu, basi Musa naye ataweza. Riwaya inaeleza kuwa, Nuru ndogo ya Kimungu kutoka katika pazia zisizokuwa na kikomo iliangaza kwenye mlima ule. Mlima ukatawanyika vipande vipande. Nabii Musa (a.s) akazimia kutokana na tukio hilo lenye kuogofya. Alipozinduka, alimhimidi Mwenyezi Mungu na kutubu kwa kujaribu kuvuka mipaka.
7. "Qaba qawsayni aw adna" [Kisha akakaribia na akateremka.

wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w). Katika dini yake, Uislamu, *salat* (sala), ilitolewa zawadi kwa ummah wake kama baraka itokayo kwa Mwenyezi Mungu.

❀

Baada ya miaka kumi na tatu ya jitihada za kuwaongoza watu, Mtume Muhammad (s.a.w) alipelekwa katika pango jingine. Pango la Thawr wakati wa Hijrah. Hakupelekwa katika pango hili kwa ajili ya kupewa mafunzo, bali apate kuzama ndani ya za Mwenyezi Mungu na kuukamilisha moyo wake. Alikaa pangoni siku tatu mchana na usiku. Kipindi hiki hakuwa peke yake. Alikuwa na swahaba wake Abu Bakr, ambaye alikuwa tajiri mkubwa sana kiimani, kiroho na kimaanawi baada ya Mtume (s.a.w). Abu Bakr alipata heshima kubwa kuwa pamoja na Mtume (s.a.w) kule pangoni. Hivyo akawa "wa pili kati ya wawili." Mtume Muhammad (s.a.w) akamwambia rafiki yake mpendwa:*"Usihuzunike hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi."* (Qur'an, Tawba, 9:40)

Kwa njia hii, alimfundisha jinsi ya kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu (*mai'yyah*). Hili ni funzo la kwanza katika siri ya *dhikr* na kuzifurahisha nyoyo kwa kuzifungulia milango ielekeayo kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa maneno mengine, pango la *Thawr* ndiyo sehemu ya kwanza katika mafundisho ya awali na ya msingi ya

---

Akawa ni kama baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi. Najm 8-9]: Mtume (s.a.w) alipelekwa mpaka nyumba ya *Sidra al-Muntaha*. Hata malaika Jibril haruhusiwi kukaribia eneo hili. Aya inauelezea ukaribu huu kama "mipinde miwili au karibu zaidi." Makutano ya siri kati ya Mtume na Mwenyezi Mungu yalifanyika katika umbali huu, umbali ambao ni vigumu kwa akili ya mwanadamu kuuelewa. Akili zetu zenye ukomo na udhaifu zinaletewa mfano huu kuonesha ulinganisho baina ya Nabii Musa (a.s) na Mtume Muhammad (S.a.w).

moyo; moyo ndio humbeba mja kumpeleka kwa Mwenyezi Mungu ndani ya anga lisilokuwa na kikomo la siri mbalimbali. Vilevile, kukaa kwa muda pangoni ilikuwa kituo chake cha kwanza cha safari hii takatifu. Katika kipindi hiki ndipo Mtume Muhammad (s.a.w) alipoanza kumfunulia Abu Bakr (r.a) siri zilizokuwa moyoni mwake, moyo ambao ulikuwa chemchem ya nuru. Hii ilitengeneza kiunganishi cha kwanza kabisa katika Nyororo ya Dhahabu, itakayoendelea kuwepo milele na milele. Imani hupata nguvu kutoka kwenye upendo. Madhumuni na lengo la msingi la safari zote Tukufu ni upendo kwa ajili ya Mtume (s.a.w). Njia ya pekee ambayo mtu anaweza kuifuata na akaipata Baraka ya Mwenyezi Mungu ni kufuata mfano wa Mtume (s.a.w). Kwa sababu kanuni ya upendo hailazimishi kumpenda mtu tu bali pia kukipenda kile kinachopendwa na mpendwa wake huyo. Ni vigumu kuelewa upendo huo wa kimungu kwa uelewa wetu mdogo wenye upungufu na udhaifu.

Tunaamini kuwa kisa kifuatacho kitakuwa na athari kubwa kwenye nyoyo zozote; athari ambayo itahama kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, kutegemeana na upeo vipawa vya moyo wake. Abu Bakr Siddiq (mtiifu) katika maisha yake yote alipata furaha mpya na ya kipekee kwenye kila mazungumzo na usuhuba wake na Mtume (s.a.w). Kutokana na kuzizoea na kuzielewa siri za ndani kabisa za utume na kupata Baraka ya ishara zake nyingi, muda wote alikuwa na shauku na Mtume (s.a.w) hata kama wangekuwa pamoja.

Alipomsikia Mtume Muhammad (s.a.w) akisema: “Sijanufaika sana na mali ya mtu yeyote zaidi ya nilivyonufaika na mali ya Abu Bakr,”, Abu Bakr (r.a) alijibu huku akilia: “Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hakika mimi mwenyewe

na mali zangu vyote ni mali yako!"[8] Kwa njia hii alionesha kuwa amejisalimisha yeye pamoja na mali zake zote kwa Mtume (s.a.w) na kuwa mwenye "kuyeyuka" (*fani*) ndani yake. (Katika Tasawwuf, hali hii hujulikana kama *fana fi al-Rasul* [kuyeyuka ndani ya Mtume]). Abu Bakr alitumia mali zake zote kwa ajili ya Mtume (s.a.w). Kwa mfano, siku moja Mtume Muhammad (s.a.w) alipomwambia:

"Wasaidie askari!"

Abu Bakr alileta kila kilichokuwa na thamani kwa Mtume . Mtume Muhammad (s.a.w) alipomuuliza:

"Umewaachia nini familia na watoto wako?" alijibu kwa imani ya hali ya juu kabisa:

"Mwenyezi Mungu na Mtume wake.. . !"[9] Muawiyah ibn Abi Sufyan alimzungumzia Abu Bakr akisema: "Dunia hai-kumtaka Abu Bakr; naye pia hakuitaka dunia.. ."[10]

Inatakiwa ifahamike kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) aliijali familia ya Abu Bakr na hakutaka watekeseke. Tukio la Abu Bakr (r. a) kujitolea mali zake zote lilikuwa tukio maalumu miongoni mwa Maswahaba. Hii ni kutokana na ukweli kuwa Abu Bakr na familia yake walikuwa na subira na *tawakkul* ya hali ya juu sana kwa Mwenyezi Mungu.

Mwenyezi Mungu ndiye aliyekuwa msaidizi, mlinzi na mwenyeji wa wasafiri hawa wawili. Makafiri walipokuwa

8. Ibn Mâjah, Fadâil Ashâb al-Nabî 11; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 253; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XV, 273; Ibn Abî 'Âsim, al-Sunnah, II, 577.
9. Tirmidhî, Manâqib 16; Abû Dâwûd, Zakat 40; Dârimî, Zakât 26; al-Hâkim, al-Mustadrak, I, 574; al-Bayhaqî, al- Sunan, TV, 180; al-Bazzâr, al-Musnad, I, 263, 394.
10. Ahmad ibn Hanbal, Kitâb al-Zuhd, uk. 18.

wanawatafuta, hawakuwaona badala yake waliona utando wa buibui katika mlango wa pango, walipokuwa wamejificha katika mlima wa Thawr. Baada ya Mtume na Abu Bakr kuingia mle pangoni, buibui alitandaza utando kwenye mlango wa pango; hii iliwachanganya makafiri wakadhani kuwa mle pangoni hakukuwa na mtu. Mshairi Arif Nihat Asya analielezea tukio hilo utenzi wake akisema:

Utando wa buibui haukuwa hewani,
Haukuwa ndani ya maji, wala haukuwa ardhini;
Bali ulikuwa mbele ya macho
Ya wale waliokuwa vipofu dhidi ya haki. [11]

Wasafiri hao adhimu, wakiwa chini ya ulinzi wa Mwenyezi Mungu, waliwasili Quba jirani na mji wa Madina. Walikuwa wakisubiriwa kwa hamu na shauku kubwa; hatimaye sasa walikuwa wamewasili, na hivyo, hali ya furaha na shangwe ilitanda juu ya mji wote.

Mwangwi wa sauti za *"Tala'al-badru 'alayna"* (mwezi umechomoza juu yetu) kutoka kwenye vilima, ulisikika na kutanda katika anga, na kuzipa raha nyoyo za watu. Ilikuwa tarehe 12 ya mwezi Rabi al-Awwal, na kalenda mpya iliasisiwa kwa ajili ya ustawi na mafanikio yote. Kuanzia siku hiyo, matukio yote yangeanza kurikodiwa.

Tokea siku hiyo, Madina ikawa kitovu na kioo cha maendeleo ya kuenea kwa Uislamu. Kutokana na *Hijrah*, wajihi mweusi na wenye giza wa ukafiri ukasawijika. Msikiti wa Mtume Madina na ule wa Quba ukapata daraja adhimu na kubaki kuwa mahali patakatifu na penye kuwakumbusha watu juu ya Hijra Tukufu.

11. Asya, Arif Nihat, Dualar ve Aminler, (Istanbul, 1973), uk.122.

Ansar (wenyeji wa mji wa Madina) waliwaonesha *Muhajirun* (wahamiaji kutoka Makka) mali zao, wakawaambia: "Hii ni mali yangu; nusu itakuwa yangu na nusu itakuwa yako…" Hivyo, msingi wa undugu wa Kiislamu, ambao tumekuwa tukijitahidi kuuendeleza kupitia juhudi zetu za hisani na misaada mbalimbali, ukaasisiwa. Kwa njia hii, Madina ikawa mahali pasiposahauliwa katika historia ya Uislamu. Adhana, mfungo wa mwezi wa Ramadhan, Eid, na Zakat zikawa sehemu ya maisha ya jamii ya Kiislamu na pia mapambano na vita kubwa za kihistoria zilitokea Madina. Amali na matukio haya yote yalitengeneza mifano adhimu ya mustakbali wa *Ummah* mzima.

Vita ya Badr ilikuwa mtihani wa makabiliano ya imani ya kweli dhidi ya ukafiri, matokeo yake imani iliushinda ukafiri. Mshikamano wa kidini ulichukua nafasi ya mshikamano wa kikabila. Kwa mfano, Abu Bakr (r.a) alipambana na mwanae vitani, ambaye alikuwa kafiri. Abu Ubayda ibn Jarrah (r.a) pia alipambana na baba yake, ambaye alikuwa kafiri. Mwisho, Hamzah (r.a) alikabiliana uso kwa uso vitani na kaka yake alikuwa kafiri. Walikutana wote wakiwa wameshika upanga tayari kwa kupambana. Makabiliano hayo ya kupigania imani baina ya watu wanaounganishwa na muungano wa damu hayakuwahi kufikiriwa kabisa kabla ya Uislamu; vita zilizokuwa zikipiganwa hapo kabla zilikuwa zikisababishwa na mizozo ya kikabila. Aidha, Mwenyezi Mungu Mtukufu alituma jeshi la Malaika. Malaika hawa, walishiriki kikamilifu katika mapambano haya adhimu, walipata heshima kuliko malaika wengine. Baada ya tukio hili kubwa, Mwenyezi Mungu Mtukufu akashusha aya ifuatayo ili kuwalinda Waislamu dhidi ya majigambo na takabari yoyote: *"Hamkuwaua nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewauwa. Na wewe*

hukutupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye tupa, ili awajaribu waumini majaribio mema yatokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Msikizi na Mjuzi." (Qur'an, Anfal, 8:17)

Katika Vita ya Uhud, iliyotokea baada ya vita ya Badr, damu ya Hamzah ilishuhudiwa ikimwagika. Idadi ya waliouawa kishahidi, akiwemo Hamzah, ilifikia watu sabini. Swala ya maiti (*salat al-janazah*) ilifanyika kwa mashahidi kumi kwa pamoja. Mashahidi nane walikuwa wakizikwa kwa wakati mmoja, Hamza akazikwa kwa wakati wake; hivyo alijumuishwa katika kila swala ya maiti. Hamzah aliswaliwa mara nyingi. Tusisahau kuwa Mtume (s.a.w) alimpenda mno ami yake huyo kiasi kwamba alimuelezea Hamza kuwa ni sehemu ya moyo wake.

Vita ya Uhud ilijaa matukio yenye kuogofya na majozi makubwa kama hayo yaliyoelezwa. Kupitia mitihani hii, umma ulipata ukomavu kwa namna ya kumtumikia Mwenyezi Mungu na kujisalimisha Kwake. Matokeo ya ukomavu huo ni kuridhika na kadari ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambayo ni daraja ya juu kabisa ya imani ya Kiislamu.

Wakati wa vita hii, tukio lililotetemesha ardhi na mbingu lilitokea; vizingo viwili katika ngao ya Mtume (s.a.w) vilimgonga shavuni na kuvunja jino lake moja. Tukio hilo liliwazamisha Maswahaba wote katika huzuni kubwa.

Mtukufu Mtume (s.a.w) alifuta damu usoni mwake kwa mikono yake na hakuiacha idondoke chini, akiogopa kuwa inaweza kusababisha kushuka kwa ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Pia ni kutokana na sababu hii iliyomfanya kujilinda kwa Mwenyezi Mungu na kuomba : "Ewe Mwenyezi Mungu! Umma wangu haujakutambua! Ninakuomba uwape uongofu!"[12]

12. Bukhârî, Anbiyâ 54; Muslim, Jihâd 104; Ibn Mâjah, Fitan 23; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 380.

Kuna hadith moja inatuambia kuwa:

"Ghadhabu ya Mwenyezi Mungu iliongezeka dhidi ya wale wote walioufanya uso wa Mtume ukavuja damu."[13]

Vita ya Uhud ndiyo iliyokuwa imejaa matukio hayo mazito na ya kuhuzunisha.

Maswahaba wa Mtume (s.a.w) walimfuata bila kusukumwa wala bila masharti. Wakamwambia: "Ewe, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tunakuamini. Tumeikubali kwa moyo wote Qu'ran uliyotuletea kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Na tuliwekeana agano kwamba tutakutii na kukufuata. Fanya utakavyo, tupe maagizo! Daima tutakuwa pamoja nawe! Tunaapa kwa Mwenyezi Mungu alyekuleta kwetu, ukiingia baharini nasi tutaingia nawe. Hakuna kati yetu atakae kataa kufanya hivyo…"[14] Maswahaba waliyatamka maneno haya wakiwa katika kilele cha furaha na raha ya imani.

Lakini, katika mapigano ya Uhud, walipoacha kufuata agizo lililotolewa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na walipoelekea kidogo tu kwenye manufaa ya kidunia, kulibadilisha matokeo ya vita. Onyo kutoka kwa Mwenyezi Mungu lilidhihirika na hatimaye wakachelewa kupata ushindi.

Mlima Uhud ni eneo lenye kuheshimika katika moyo wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Katika maisha yake yote aliendelea kuutembelea mlima Uhud na kuwatembelea mashahidi wote wa vita ya Uhud. Mara kwa mara alikuwa

13. Ibn Ishâq, Sîrah, p. 311; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 317; Ibn Abî Shaybah, al-Musasnnaf, VII, 373.
14. Bukhârî, Magâzi, 4; Muslim, Jihâd 83; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 389, 428, 457; Ibn Abî Shaybah, al-Musasnnaf, VII, 6

akisema: "Tunaipenda Uhud, nayo inatupenda!"[15] Maneno haya yameipa heshima sehemu hii, ambayo inajulikana kwa kuwa na makaburi ya mashahid wa mapigano hayo, na ni sehemu maalumu iliyokuwa moyoni mwa Mtume (s.a.w), daraja ambayo inaonekana kwa ziara zake za mara kwa mara katika eneo hilo. Eneo hili litaendelea kuwa maalumu kwa Waislamu wote.

❀

Katika vita vya Khandaq (handaki) Mtukufu Mtume (s.a.w) aliweza kuvunja mwamba mgumu ambao maswahaba zake walishindwa kuuondosha. Alipopiga mara ya kwanza, alisema kuwa aliliona kasri la Kaisari. Katika pigo la pili, akasema kuwa aliona kasri ya Kisra, mfalme wa Uajemi. Katika pigo la tatu, alisema kuwa aliona makasri yaliyo ya mji wa San'ah, Yemen, yakianguka. Hapa alikuwa akitoa bishara ya kuenea kwa Uislamu katika ardhi hizi, na hivyo kuingiza matarajio ya ushindi mkubwa ndani ya nyoyo za Waislamu. Alikuwa akitoa bishara njema kwamba haki itaishinda batili na alikuwa akichora ramani ya ulimwengu ambamo yale yaliyokuwa yameshindikana sasa yatawezekana, yatatokea moja baada ya jingine.

Vita ya Khandaq ilikuwa ni moja kati ya maumivu makubwa, uchovu, njaa, baridi, na kiza. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliomba akisema:

"Mola wangu! Maisha ya kweli ni maisha akhera, wanusuru *Ansar na Muhajirun*."[16]

---

15. Bukhârî, I'tisâm 16; Muslim Fadâil 10; Ibn Mâjah, Manâsik 104; Muwatta, Madînah 10; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 140.
16. Bukhârî, Jihâd 34; Abû Dâwûd, Salât 12; Nasâî, Masâjid 12; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 289.

Katika dua hizi alikuwa akieleza kuwa mateso, maumivu na tabu zote za hapa ulimwenguni si chochote ukilinganisha na maisha ya akhera, na hili ndilo lililowafanya maswahaba zake kuhangaikia akhera na kuifanya kuwa ndio lengo lao.

❀

Kama ilivyobashiriwa na Mtukufu Mtume (s.a.w) wakati wa Mkataba wa amani wa Hudaybiya, Waislamu watashinda katika mapambano na vita vilivyokuwa mbele yao na watu wa Makkah watazisalimisha silaha zao kwa wamiliki wake wa kweli. Makkah ilitekwa kiroho na wale wote walioipenda kwa msamaha, amani, usalama na uongofu. Matamanio ya Makkah, yaliyojaa mateso, uonevu na tabu, yalifikia kikomo. Miaka mingi ya huzuni ikabadilika na kuwa ya furaha. Kisha, ikiwa kama shukrani kwa Mwenyezi Mungu, tukio kubwa kabisa la msamaha katika historia lilitokea. Kupitia msamaha huu, watu wengi waliowaua Waislamu hapo mwanzo na wale wote waliofanya uahalifu walipata Utukufu , heshima na hadhi ya Uislamu.

Hatimaye, Aya ya mwisho ilishuka katika kipindi cha Hijjah ya Kuaga (*Hajjat'ul-Wada'*). Ilitangazwa kuwa dini ilikuwa imekabilishwa. Wakati huo huo, aya hii ilikuwa kama kiashirio kuwa Mtume Muhammad (s.a.w), ambaye aliletwa kama Rehma kwa ulimwengu, alikuwa amekamilisha jukumu lake na sasa muda wa yeye kurejea kwa Mola wake ulikuwa umewadia. Katika kupata ushuhuda wa yeye kufundisha dini, aliwauliza mara tatu maswahaba zake:

" Je nimewasilisha dini kwenu? Je nimewasilisha dini kwenu?Je nimewasilisha dini kwenu?"

Baada ya kupata jibu kutoka kwa maswahaba kukubali

kuwa alikuwa amefikisha alichotumwa na Mola wake, aliinua mikono na kumuomba Mwenyezi Mungu ashuhudie tukio hilo. Alisema:

"Ewe Mwenyezi Mungu, shuhudia! Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia! Ewe Mwenyezi Mungu shuhudia!"[17]

Katika tukio hili, amana Tukufu , ambayo Mtume (s.a.w) alikuwa amepewa na Mwenyezi Mungu kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu ya Utume katika miji ya Makka na Madina, sasa amana hiyo ilihamishwa na kupewa Ummah wake waitunze na kuilinda mpaka Siku ya mwisho.

Baadhi ya Ansari walikuwa na wasiwasi kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa ameifungua ardhi aliyozaliwa; wakaanza kupaza sauti za wasiwasi wao:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu amemfungulia Mtume wake Makkah, kuanzia leo, ataishi Makkah na hatarudi tena Madina."

Japokuwa haya yalikuwa ni mazungumzo baina yao wenyewe, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) baadaye alijadiliana nao kuhusu wasiwasi waliokuwa nao. Walitahayari na kukiri kuwa walikuwa wameyasemaa. *Rasulullah* (s.a.w) aliwaambia *Ansar*:

"Ninaomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu kwa kufanya hivyo!Maisha yangu na kifo changu kitakuwa nanyi.. ."[18]

17. Bukhârî, Fitan 8; Muslim, Îmân 378; Abû Dâwûd, Manâsık 56 Nasâî, Ihdâs 4; Ibn Mâjah, Fitan 2; Dârimî, Manâsik 34; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 447.
18. Muslim, Jihâd 86; Ahmad ibn Habal,, al-Musnad, II,538; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XI, 75; Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, VI, 382,al-Bayhaqi, al-Sunan al Kubrâ, IX, 117.

Alionesha mfano wa uaminifu usio kifani na kurejea Madina.

❀

Muhammad alikuwa Mtume wa mwisho, lakini kulikuwa na mitume wengi waliomtangulia. Ifuatayo ni orodha baadhi ya mitume walioletwa na Mwenyezi Mungu ili kuwaongoza na kuwashauri wanadamu.

Adam (a.s), ambaye malaika waliamrishwa kumsujudia;

Eliya (a.s), aliyeona siri za Mbinguni;

Nuhu (a.s), aliyeitakasa Ardhi kwa mafuriko;

Hud (a.s), aliyezigeuza ardhi za makafir juu chini kwa dhoruba;

Saleh (a.s), aliyetikisa misingi ya nyumba za wakaidi na waasi;

Ibrahim (a.s), aliyeugeuza moto wa Nimrod kuwa bustani la mawaridi kutokana na kujisalimisha kwake na kumtegemea Mwenyezi Mungu;

Ismail (a.s), ambaye ni alama ya usafi wa moyo, aminifu, utiifu, kumtegemea Allah; simulizi kuhusu Ismail zitaendelea kukumbukwa na waumini wakati wa Hijjah hadi siku ya mwisho;

Is-haq (a.s), ambaye mitume wa Israel wanatokana na uzao wake;

Lut (a.s), nabii aliyekandamizwa na watu Sodoma na Gomorra, watu walioishi katika nyika ya historia kwa kufutwa katika uso wa dunia kutokana na maovu na maasi yao yaliyopindukia.

Zulqarnayn (a.s), aliyebeba nuru ya Tawhid kutoka Mashariki kwenda Magharibi;

Yakubu (a.s), aliyekuwa alama ya uvumilivu, upendo, na shauku;

Yusufu (a.s), ambaye uzuri wake uliufanya uzuri wa mwezi ufifie na aliye kuwa sultani wa Misri baada ya kuishi kama mtumwa na mpweke gerezani, aliyeishi kama mgeni katika ardhi hii, akapata mateso, maumivu, na kupambana na matamanio;

Shuayb (a.s), alijulikana kama khatibu wa Mtume na aliyezijaza nyoyo furaha kutokana na mahubiri yake;

Khidhr (a.s), aliyemfundisha Musa siri za kutoka kwa Mwenyezi Mungu;

Musa (a.s), aliyevunja mamlaka ya Farao na kufungua njia katika bahari ya Sham kwa fimbo yake;

Haruon (a.s), aliyemsaidia kaka yake Musa (a.s) muda wote na mahali kote;

Daudi (a.s), ambaye kwa dua zake (*dhikr*), aliifanya milima, mawe na wanyama kuingia katika unyenyekevu;

Sulayman (a.s), ambaye moyo wake adhimu ulikataa kukipigia magoti chochote katika ufalme wake;

Uzayr (a.s), alama ya ufufuko wa siku ya mwisho, aliyefufuliwa baada ya kufa kwa miaka mia moja;

Ayubu (a.s), aliyekuwa msingi wa ustahimilivu;

Yunusu (a.s), aliyelishinda giza kwa kuzama ndani ya *dhikr*, maombi na toba akiwa katika hali ya unyenyekevu wa hali ya juu;

Ilyas (a.s), aliyepata Baraka kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu alipopokea salamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu: "Iwe salama kwa Ilyas." (Qur'an, Saffat, 37: 130);

Iliya (a.s), aliyepaishwa juu ya walimwengu;

Nabii mwenye moyo safi (Zulkifl) (a.s), aliyepewa Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu;

Luqman (a.s), mkuu wa matabibu, wa kiroho na kimwili, anayekumbukwa kwa hekma zake yakinifu;

Nabii Zakaria aliyeonewa (a.s), aliyendelea kujisalimsha na kumtegemea Mwenyezi Mungu, hata mwili wake ulipogawanywa katika vipande viwili hakulalamika;

Yahyaa (a.s), ambaye, kama ilivyokuwa kwa baba yake, alikufa kama shahidi;

Na Issa (a.s), ambaye sifa zake adhimu zilijumuisha usafi wa moyo, uponyaji wa wagonjwa na kufufua wafu kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kupitia maombi yake ya dhati. Hii ni mifano ya mitume wapatao laki moja na ishirini walioletwa ulimwenguni ili kuwaongoza wanadamu kwa ishara na matukio yaliyoteremka kama mvua juu ya ardhi ya kimaanawi ya mwanadamu. Mitume hao waliokuwa kama cheche Tukufu za Muongozo wa Mwenyezi Mungu, ambao kwa mifano na ujumbe walikuwa kama nyororo ya unabii, walikuwa kama bishara njema iliyobashiri ujio wa Muhammad (s.a.w) aliyeletwa kama Rehma ya ulimwengu.

❀

Vyanzo vyetu vinatuambia kuwa mwanamke mwenye bahati Suwayba alikuwa ni mmoja kati ya walezi wa mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Alikuwa kijakazi wa Abu Lahab.

Alikuwa ni mwanamke wa kwanza kumpa Abu Lahab habari za kuzaliwa mpwa wake. Baada ya kuleta habari hizo nzuri, akamwachia huru kutokana na msukumo na furaha ya kikabila. Tukio hili lilitokea siku ya Jumatatu. Furaha hiyo ya Abu Lahab kwa kuzaliwa kwa Muhammad (s.a.w), japokuwa ilikuwa imechanganyika na hisia za undugu wa kikabila, husababisha adhabu ya moto kwa kafiri huyo kupungua kila siku ya Jumatatu.

Baada ya kifo chake, baadhi walimuona Abu Lahab ndotoni ambapo waliweza kumuuliza kuhusu maisha yake ya akhera:

"Abu Lahab! Una hali gani?"

"Huwa ninaadhibiwa motoni! Lakini adhabu yangu inapungua mkesha wa siku ya Jumatatu. Usiku huo huwa ninanyonya maji yatokayo katikati ya vidole vyangu. Nasikia baridi kwa kuyanywa. Hii ni kwa sababu siku kama hii nilimwachia huru Suwayba baada ya kuja kwangu na kunipa habari njema za kuzaliwa kwa mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Mwenyezi Mungu amenilipa kwa kunipunguzia adhabu yangu siku ya Jumatatu usiku."

Ibn al-Jazari anasema:

"Kafiri kama Abu Lahab alinufaika kwa kuonesha furaha siku aliyozaliwa Mtume (s.a.w) ijapokuwa furaha hiyo ilikuwa imechanganyika na hisia za ukabila. Kama kafiri anapata faida kama hiyo, vuta picha ya tunu na Baraka za Mwenyezi Mungu wanazozipata waumini kwa kumfungulia Mtume (s.a.w) nyoyo zao na kuwakaribisha wageni kwa ajili ya kuadhimisha usiku huo…"

Njia muafaka ya kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume

(s.a.w) ni kuandaa mikutano na vikao kwa ajili ya kuiwasha upya nuru ya moyo wake katika mwezi huu aliozaliwa. Lengo la shughuli hizi ni ili tunufaike na hali ya kiroho ya mwezi huu uliobarikiwa wakati wa karamu kwa *Ummah*, ili kuzifariji nyoyo zilizokata tamaa za masikini, wageni, yatima, na wasiojiweza, kwa kuwasaidia kwa njia mbalimbali na kuwapa sadaka, na kuandaa visomo vya wazi vya Qur'an. [19]

Yatima huyu hakuwahi kusoma wala kuandika kwa sababu hakusoma kwa mwalimu wa kibinadamu, lakini alikuja kama mwokozi wa wanadamu wote, mkalimani wa ulimwengu wa ghayb (usioonekana) na mwalimu wa shule ya ukweli.

Nabii Mussa (a.s) alileta sheria na kanuni mbalimbali. Nabii Daudi (a.s) alitofautishwa kwa uwezo wake wa dua na kunong'ona na Mwenyezi Mungu Mtukufu . Nabii Issa (a.s) aliletwa kumfundisha mwanadamu tabia njema, na kuwa mfano na kielelezo cha zuhdi na kuipa nyongo dunia katika ulimwengu wa jauhari. Lakini, Mtume wa Uislamu, Muhammad, (s.a.w), alikuja na yote hayo: aliweka seheria na kufundisha jinsi ya kuitakasa nafsi na kumuabudu Mwenyezi Mungu kwa moyo msafi. Alimlea mwanadamu katika maadili bora na kuyaonesha maadili hayo katika kila kipengele cha maisha yake. Aliainisha njia ambazo mwanadamu hapaswi kupotoshwa na mvuto bandia wa dunia hii. Kwa kifupi, shakhsia na juhudi zake zilikusanya uwezo na wajibu

19. Yusuf ibn Ismâil al-Nabhânî, al-Anwâr al-Muhammadiyyah min almawâhib al-ladunniyah, uk. 28-29. (Sehemu ya riwayah ilisimuliwa na al-San'ân, al-Mosesnnaf, VII, 478; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, I, 261; al-Marwazî, al-Sunnah, I, 82; İbn Hagar al-'Asqalânî, Fath al-Bârî,IX, 145).

wa mitume wote. Katika shakhsia yake kuna utu uliodhihiri kutokana na nasaba na maadili yake, neema ilioonekana katika uzuri wa maadili na mwili wake.

Alipofikisha umri wa miaka arobaini, bila shaka hiki kilikuwa ni kipindi muhimu sana kwa mwanadamu.

Alikuwa ameishi miaka arobaini akiwa pamoja na watu wake. Vitu vingi vizuri ambavyo angekuja navyo bado walikuwa hawavijui. Hakuwa akijulikana kama mkuu wa dola, au kama mhubiri, wala hata kuwa mhadhiri. Sio tu katika kipindi hiki kwamba watu hawakujua kama ni kamanda mahiri, bali pia hakujua kuwa ni askari wa kawaida.

Hakuwa amewahi kutoa hotuba kuhusu historia ya umma zilizopita, mitume, Siku ya Hukumu, au pepo au Jahannam. Alikuwa mtu wa kipekee, akiishi maisha adhimu ya aina yake katika hali ya maadili ya hali ya juu. Lakini baada ya kutoka katika pango la Mlima Hira, alikuwa amebadilika kabisa. Alikuwa amekabidhiwa maamrisho ya Mwenyezi Mungu.

Watu wote wa Arabia walishtuka na kujawa na hofu alipoanza kazi yake. Hotuba na ufasaha wake usiokuwa wa kawaida viliwavuta watu wote. Ghafla mashindano ya ushairi, fasihi, arudhi na hotuba vikafikia kikomo. Washairi hawakuthubutu tena kubandika mashairi yao kwenye kuta za Kaabah Tukufu. Hivyo, desturi hiyo iliyokuwa imedumu kwa karne nyingi, ikafikia kikomo, kiasi kwamba hata binti wa mshairi maarufu wa Kiarabu, Imru'ul-Qays, alivutiwa mno baada ya kuzisikia aya za Qur'an, na kumfanya aseme kwa mshangao:

"Haya hayawezi kuwa maneno ya mwanadamu! Kama kuna maneno kama hayo katika dunia hii, mashairi ya baba yangu yanapaswa kuondolewa kabisa kwenye kuta za kaabah. Nendeni myaondoshe; na mahali pake wekeni hizi aya…!"

❀

Mtume, na Qur'an yenyewe, viliupa changamoto ulimwengu wote kuleta sura mfano wa sura za Qur'an. Lakini, mpaka leo changamoto hii ya kuwataka watu walete sura inayofanana na sura za Qur'an haijajibiwa wala kuitikiwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

"Na ikiwa mna shaka kwa hayo tuliyo mteremshia mja wetu basi leteni sura moja ya mfano wake, na muwaite mashaidi wenu badala ya Mwenyezi Mungu, ikiwa mnasema kweli." (Qur'an, Baqara, 2:23)

❀

Mtu huyu, ambaye hakuwa akijua kusoma wala kuandika, aliyetokea katika jamii isiyostaarabika, aliwashangaza watu wa zama zake kutokana na maarifa, elimu na hekma kubwa iliyoteremshwa kwake, ambayo imekuwa kama bahari ya miujiza itakayoendelea kuwashangaza mpaka Siku ya Mwisho. Qur'an Tukufu imezungumzia mambo kadhaa ya kielimu na kisayansi, pamoja na tabiri mbalimbali kuhusu mambo yatakayotokea baadaye; maelezo yote hayo hayajawahi kupingana na ugunduzi wowote mpya wa kisayansi. Kinyume na Qur'an Tukufu , insaiklopidia zinazoheshimika hulazimika kuchapisha juzuu mpya kila mwaka ili kusahihisha makosa, kuongezea taarifa za machapisho yake ya zamani, kitu ambacho Qur'an Tukufu imeepukana nacho kabisa.

Mtume Muhammad (s.a.w) aliwaambia watu wote kuwa alikuwa mwakilishi (Khalifah) wa Mwenyezi Mungu Ardhini.

Aliweka sheria za msingi za mfumo wa kijamii, kiutamaduni na kiuchumi, kanuni za msingi za utawala na uhusiano wa kimataifa, na aliyafanyahayo katika namna ambayo inaweza kueleweka tu kupitia utafiti wa muda mrefu uliofanywa na wasomi wakubwa wanaoheshimika wa zama zetu juu ya ulimwengu wa kimaada na kimaanawi. Kwa hakika, mwanadamu atauelewa uhalisia wa Muhammad (s.a.w) kwa kuingia katika maeneo ya elimu ya nadharia na uzoefu wa kivitendo.

Mtume Muhammad (s.a.w) – japokuwa hakuwa amewahi kushika upanga, kupitia mafunzo ya kijeshi, na hakuwa amewahi kushiriki katika kampeni ya kivita, isipokuwa mara moja kama mtazamaji tu – alikuja kuibuka kuwa askari mahiri, asiyekata tamaa, hata katika vita ngumu pindi alipokuwa akipambana kueneza imani ya umoja wa Mwenyezi Mungu. Mtume (s.a.w) alilazimika kupambana katika vita hivi, licha ya kutopenda vurugu, ili kuhakikisha amani katika jamii; hii ilikuwa sehemu ya huruma yake isiyokuwa na kikomo iliyowazunguka wanadamu wote. Katika miaka tisa aliweza kuifungua Arabia yote kwa kutumia kikosi kidogo cha jeshi ukilinganisha na vikosi vya maadui. Alipata mafanikio ya ajabu katika kuwapa uwezo wa kiroho na mafunzo ya kijeshi watu wa zama zake ambao hawakuwa katika nidhamu na mpangilio maalumu. Mafanikio yake yalikuwa makubwa sana kiasi kwamba wafuasi wake waliweza kuzishinda himaya mbili kubwa na zenye nguvu sana wakati huo, yaani Warumi na Waajemi. Hivyo habari njema alizokuwa amezitoa miaka iliyopita katika mji wa Makka zikatimia. Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa amewaambia watu wa Makka:

"Ikubalini dini yangu na mnifuate!" Abu Jahl akapinga na kusema:

"Hata kama tutakufuata, makabila ya Mudar na Rabi'a hayatakutii!"

Mtukufu Mtume (s.a.w) akamjibu: "Watanifuata kwa hiari au bila hiari, sio wao tu, bali pia Waajemi na Warumi watanifuata!" [20] Haukupita muda mrefu ahadi hii ikatimia.

Licha ya mazingira yote hasi, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alileta mapinduzi makubwa kabisa katika historia ya mwanadamu, akawanyamazisha madhalimu, na kuyakomesha machozi ya wanyonge. Alikuwa akizichana nywele za yatima kwa vidole vyake. Kwa faraja aliyoitoa, nyoyo ziliondoshwa katika wasiwasi.

Mshairi maarufu wa Kituruki, Mehmet Akif, anaielezea hali hii katika namna nzuri kabisa:

Ghafla yatima alikuwa na kufikia umri wa miaka arobaini.
Miguu yenye damu inayopita juu ya vichwa iliyafikia maji!
Kwa pumzi moja, maasumu huyu aliukomboa ubinadamu,
Kwa taharuki moja, aliwashinda Kaizari na Kisra,
Wanyonge, waliokuwa wakikandamizwa, waliamka,
Waakandamizaji, ambao hawakutegemea kushindwa, walitoweka,
Rehma kwa ulimwengu ndiyo iliyokuwa dini yake yenye kung'ara,
Kwa mbawa zake, aliifunika nchi ya wale waliotaka uadilifu,
Vyote vilivyo ulimwenguni ni zawadi kutoka kwake,
Jamii ni mdeni kwake; watu ni wadeni kwake,
Wanadamu wote ni wadeni wa maasumu huyu,
Ewe Mwenyezi Mungu! Tufufue siku ya mwisho tukiwa na imani hii,

20. Ibn Ishâq, Sirah, p.190 (riwaya kama hiyo pia inapatikana katika, Ahmad b.Hanbal, al-Musnad, IV, 128; al-Hâkim, al-Mustadrak, III, 728; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, IX, 31; Ibn Abi Shaybah, al-Musannaf, VI, 311; Ma'mar ibn Rashid, al-Jâmi', XI, 48).

Kama Mtume Muhammad (s.a.w), aliyekusanya usta-arabu wote ndani ya shakhsia yake, asingekuja ulimwenguni, wanadamu wangendelea kuwa chini ya ukandamizaji na ukatili, na mnyonge angendelea kufanywa mtumwa mpaka saa ya mwisho. Uzuri na uwiano wa ulimwengu ungebadilika kwa sababu ya uovu. Katika mazingira hayo, ulimwengu ungetawaliwa na madhalimu, na ungemilikiwa na wachache wenye nguvu. Mshairi mmoja anaielezea kwa uzuri hali hii:

Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!
Kama usingekuja ulimwenguni,
Mawaridi yasingechanua, kurumbizi wasingeimba,
Majina ya Mwenyezi Mungu yasingefahamika kwa watu,
Maisha yangepoteza maana na yangetamalikiwa na huzuni!

❀

Mtume Muhammad (s.a.w) alishiriki mapambano ishirini na saba na alituma vikosi vijulikanavyo kama *sariyya* mara hamisini. Uislamu ulipata nguvu kabisa baada ya kukombolewa kwa Makkah. Allah anasema katika aya ifuatayo katika Qur'an kwamba Uislamu ni daraja ya juu kabisa ya ukamilifu wa mwanadamu:

"Leo nimekukamilishieni dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu na nimekupendeleni Uislamu uwe ndiyo dini." (Qur'an, Maida, 5:3)

Kipindi cha utengano na muungano mkubwa kilikuwa kimewadia. Siku chache kabla ya kuanza kuumwa, Mtume alienda kwenye uwanja wa makaburi huko Madina, uitwao *Jannat'ul-Baqi'*, ambapo aliwaombea dua wafu kama ifuatavyo:

"Ewe Mwenyezi Mungu, Mtukufu ! Usiache kusamehe watu wote waliolala hapa."[21] Hii ilikuwa kama ishara ya kuwaaga.

Baada ya kurudi toka makaburini, ilikuwa ni muda wa kuwaaga maswahaba zake. Aliwapa wosia ufuatao:

"Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa hiari mmoja wa waja wake ya kuchagua baina ya ulimwengu huu na vivutio vyake au baraka na neema za Peponi. Mja huyo akachagua neema za Peponi…"

Baada ya kusikia maneno haya, Abu Bakr (r.a), ambaye alikuwa na moyo wenye hisia kali, alitambua kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akiwaaga. Huzuni kubwa ilimvama, moyo wake ukajawa na majonzi, machozi yakabubujika moyoni na machoni. Akasema kwa kugugumia:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, wazazi wangu wawe fidia kwa ajili yako! Tuko tayari kuzitoa fidia roho zetu, roho za wazazi wetu, roho za watoto wetu na mali zote kwa ajili yako…"

Hakuna mwingine yeyote katika mkusanyiko ule aliyeweza kuelewa ujumbe wa Mtume au kuelewea hisia za Mtume Muhammad (s.a.w). Abu Bakr alikuwa "wa pili kati ya wawili" kwenye pango la Thawr, daraja iliyomfanya awe makini kuliko wengine. [22]

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimzungumzia na kusema:

"Nimeweka katika moyo wa Abu Bakr vyote nilivyonavyo moyoni mwangu…"

---

21. Muslim, Janâiz 102; Nasâî, Janâiz 103; Ibn Hibbân, al-Sahîh, VII, 444.
22. Bukhârî, Salât 80; Muslim, Fadâil al-Sahâbah 2; Tirmidhî, Manâqıb 15; Dârimâ, Muqaddimah 14; Nasâî, Janâiz 69; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 18.

Maswahaba, walipoona rafiki mkubwa wa Rasulullah (s.a.w) akilia, wakaulizana:

"Je, hamshangazwi kumuona bwana huyu akilia baada ya kusikia Mtume (s.a.w) akielezea kuhusu mtu fulani aliyechagua kukutana na mola wake?!…"

Moyo safi wa Abu Bakr, ulitambua maagano yale ndio maana alianza kulia kama filimbi ya mwanzi inayolalamika kwa kutengena na shina lake.

Binti yake Mtume, mama yetu Mtukufu Fatimah, kiongozi wa wanawake wa peponi, alihuzunika kwa kuachana kwa muda na baba yake, Mtume wa Rehma kwa ulimwengu (s.a.w), alisema:

"Mtume Muhammad (s.a.w) alipokwenda Akhera, huzuni kubwa iliniangukia. Ilikuwa huzuni nzito ambayo ingeuangukia mchana basi ungegeuka kuwa usiku."[23]

Alituachia miongozo mikubwa miwili, Qur'an Tukufu na Sunnah. Qur'an Tukufu na Sunnah ni ukumbusho wa milele wa Mtume Muhammad (s.a.w) ; ni misingi ya furaha ulimwenguni na Akhera.

Mtume alirudi Madina na hapo alishikwa na mardhi yaliyodumu kwa siku kumi na tatu; kisha anga za uzuri zilifunguliwa kwa ajili ya roho yake. Ilikuwa tarehe 8 ya mwezi wa sita, 632, au12 ya Rabi'ul-awwal katika mwaka wa ll wa kalenda ya Hijiria.

Katikati ya bapa mbili za mabega ya Mtume kulikuwa na alama tukufu inayoonesha kuwa yeye alikuwa Mtume

23. al-Nabhânî, al-Anwâr al-Muhammadiyyah min al-mawâhib alladunniyah, uk. 593.

wa mwisho. Maswahaba wengi walitamani kuibusu. Imamu Bayhaqi anasema:

"Maswahaba hawakuwa na uhakika kama kweli Mtume (s.a.w) alikuwa amesafiri kwenda akhera baada ya kutoona mabadiliko yoyote usoni mwake baada ya kuhamia katika Ulimwengu wa milele. Asma (r.a) aliitafuta alama hiyo ya utume katika mwili wa Mtume. Baada ya kuona alama hiyo imepotea, wakapata uhakika kuwa amekwenda katika ulimwengu wa Akhera."[24]

Dini ilikuwa imekamilika; uthibitisho wa maswahaba kuhusu kufikishwa ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wanadamu ulitolewa hao na kutolewa kama ushuhuda mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Baada ya yote hayo, Mtume Muhammad (s.a.w) aliitwa kwenda kwenye ulimwengu wa milele.

Kwa sasa, anausubiria *Ummah* wake kwenye *Mahshar*, yaani uwanja wa ufufuko, kwenye *Swirat* na mto wa *Kawthar*.

Utuombe, Ewe Rasulullah!
Tuunge mkono, Ewe Rasulullah!
Utukaribishe, Ewe Rasulullah!

❀

Siku ya Jumatatu tarehe 12 ya Rabi al-awwal, ulimwengu ulipata Baraka kwa kuzaliwa kwake.

Siku ya Jumatatu tarehe 12 ya Rabi al-awwal ndiyo siku ambayo Mwenyezi Mungu alimpa Mtume kazi ya kutangaza ujumbe Wake kama Mtume. Abu Qatada anasimulia kama ifuatavyo:

24. Ibn Sa'd, al-Tabakât, II, 271; al-Bayhaqi, Dalâil al-nubuwwah, VII, 219.

"Mtume Muhammad aliulizwa kuhusu kufunga siku za Jumatatu. Alijibu akasema:

"Hii ni siku niliyozaliwa na ni siku niliyopewa Utume."[25]

Vilevile, ni siku ya Jumatatu 12 ya Rabi al-awwal, alipoingia Madina na kuasisi dola mpya ya kiislamu, itakayoendelea kuwepo daima.

Na mwisho, siku ya Jumatatu tarehe 12 ya Rabi al-awwal, alihamia Akhera.

Katika kuonesha Utukufu wa siku hii, matukio ya kuzaliwa kwake, Hijra yake kutoka Makkah kwenda Madina, na safari yake kutoka katika ulimwengu huu kwenda kwenye ulimwengu wa Akhera, yote hayo yalitokea Jumatatu tarehe 12 ya Rabi al-Awwal. Huu ni uthibitisho wa Utukufu wa mwezi huu. Ishara za Uzuri wa Mwenyezi Mungu (*Jamaal)* na Utukufu wa Mwenyezi Mungu (*Jalaal)* huonekana mno wakati huu. Katika ulimwengu wa ndani, furaha ya kusherehekea pamoja na machungu ya utengano hukutana katika muungano wa mambo haya mawili yanayokinzana. Lakini, bado anausubiri Ummah wake huko Akhera.

Kwa kuondoka Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kwenda kwenye Ulimwengu wa Furaha, ulimwengu huu ulinyang'anywa uwepo wake wa kimwili. Kwa hakika, ulimwengu huu ni wenye ukaidi, kama ulivyoelezwa katika shairi la Mshairi wa Kisufi wa zama za Othmaniya, Aziz Mahmud Hudayi:

25. Muslim, Siyâm 196; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 299; Ibn Hibbân, al-Sahîh, VIII, 403; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, IV, 286.

Nani anayepata utii kutoka kwako?
Je wewe si ulimwengu bandia?
Je wewe si Ardhi ile ile,
Iliyomchukua Muhammad Mustafa?[26]

26 Hudâî Mahmud, Kulliyyât-ı Hudâî, (Istanbul, 1338), uk. 109.



Maisha Ya Mfano Na Nafasi Yake Katika Mitume

"Nuru juu ya nuru." (Qur'an, al-Nur, 24:35)

Mtindo wa maisha ya Mtume (s.a.w) ni mfano bora wa kuigwa na kila mwanadamu. Ni mfano bora wa kiongozi wa dini. Ni mfano bora wa kiongozi wa dola. Ni mfano bora wa kuigwa kwa wale wanaoingia katika bustani ya upendo wa Mwenyezi Mungu. Ni mfano bora kabisa wa shukrani na unyenyekevu kwa wale wenye kutunukiwa na Mwenyezi Mungu. Ni mfano bora wa ustahmilivu na subira katika nyakati na mazingira magumu kabisa. Ni mfano bora wa ukarimu na wa kutopenda kujikusanyia mali. Ni mfano bora kuitendea wema na kuijali familia. Ni mfano bora wa kuwaonea huruma wanyonge, wapweke na watumwa, na ni mfano bora wa kuwasamehe wakosefu.

kama wewe ni tajiri, basi tafakari juu ya unyenyekevu na ukarimu wa Mtume Muhammad (s.a.w) aliyezivuta nyoyo za viongozi walioitawala Arabia yote!

Kama wewe ni miongoni mwa wanyonge, angalia na jifunze namna Mtukufu Mtume (s.a.w) alivyoishi mjini Makka chini ya utawala dhalimu na ukandamizaji wa waabudu masanamu.

Kama umepata ushindi, fikiria juu ya Mtume mwenye ujasiri na kuridhika ambaye, aliwashinda maadui katika vita vya Badr na Hunayn.

Lakini – Mungu aepushie mbali – kama utakuwa umeshindwa, mkumbuke Mtume (s.a.w) aliyekuwa akitembea kwa uvumilivu baada ya kujeruhiwa na akiwa amewapoteza masahaba zake katika vita vya Uhud katika kutekeleza maagizo ya Mwenyezi Mungu.

Kama wewe ni mwalimu, utafakari mfano wa Mtume (s.a.w) aliyefundisha amri za Mwenyezi Mungu kwa kufikisha nuru yake kwa ulaini na usikivu kwa wanafunzi wake wa Suffa (Ashab al-Suffa) waliokuwa katika shule Msikitini Kwake.

Kama wewe ni mwanafunzi, vuta picha ya mfano wa Mtume (s.a.w) akiwa amekaa mbele yaMalaika Mkuu, Jibril Mwaminifu (*Jibril al-Amin*).

Kama wewe ni mhubiri au kiongozi wa kiroho (*murshid*), sikiliza sauti ya Mtume (s.a.w), akitoa cheche za hekima kutoka moyoni mwake kwenda kwa masahaba wake.

Kama huna mtu wa kukutetea na kukusaidia kueneza neno la haki na kuliinua, basi yatazame maisha ya Mtume (s.a.w) aliyetangaza neno la haki kwa watu wajinga na kuwaita kwenye uongofu katika kipindi ambacho alikuwa hana msaada wowote mjini Makka.

Kama umewashinda maadui zako, ukaivunja ngome yao, kama umezivunja imani potofu na kuitangaza haki, basi tafakari mfano wa Mtume (s.a.w) siku alipoifunga Makka. Aliingia katika mji huu Mtukufu kama kamanda aliyeshinda, lakini akiwa mwenye unyenyekevu mkubwa, alikuwa amekaa juu ya ngamia kana kwamba yuko katika hali ya kusujudu; kwa hali hiyo alikuwa akielezea shukrani zake kwa Mwenyezi Mungu.

Kama unamiliki shamba na ukataka kuratibu mambo ya shamba lako, jifunze kwa Mtume (s.a.w) alipofanya uteuzi makini wa watu wanaoweza kumudu na kuendesha mashamba ya Banu Nadir, Khaybar na Fadak baada ya kuyaweka chini ya himaya yake.

Kama weweni mpweke, huna ndugu, basi mfikirie yatima huyu aliyekuwa kipenzi na mtoto pekee wa Abdullah na Aminah.

Kama wewe ni kijana, yatafakari kwa undani maisha ya Mtume (s.a.w), kijana aliyetarajiwa kukabidhiwa jukumu la Utume, akichunga kondoo wa Abu Talib mjini Makka.

Kama wewe ni mfanyabiashara unajiandaa kutoka na mizigo ya bidhaa, tafakari juu ya uzoefu wa mtu huyu Mtukufu zaidi alivyotoka na msafara wa biashara kutoka Makka kwenda Damascus, Syria.

Kama wewe ni jaji, hakimu au mwamuzi, kumbuka uadilifu na busara za Mtume (s.a.w) wakati akitatua mgogoro baina ya makabila mbalimbali katika kadhia ya kuweka Jiwe Jeusi (Hajar al-Aswad) kwenye ukingo wa Kaaba na kuepusha mauaji ambayo yangetokea, kwa sababu walikaribia kuuawana kuhusu nani anayestahili kuliweka jiwe hilo mahala pake.

Yageuze macho yako tena kwenye historia na mtazame Mtume (s.a.w) kwa mara nyingine akiwa amekaa katika msikiti wa Madina akitoa hukmu mbalimbali katika namna ya uadilifu wa hali ya juu na kutenda haki sawa baina ya maskini dhaifu na tajiri mwenye kuheshimika.

Kama wewe ni mume, yatazame kwa umakini maisha safi, ukarimu na hisia za Mtume (s.a.w) kama mume wa

mfano. Kama wewe ni mzazi, jifunze mfano wa baba wa Fatimah al-Zahra, na isome tabia ya babu wa Hasan na Husayn.

Sifa yoyote utakayokuwa nayo, na mazingira yoyote yale yatakayokukabili, usiku au mchana, utamkuta akiwa kama mwalimu kamili na muongozo wako mzuri kila wakati na kila mahali.

Mtume ni mwalimu aliyekamilika, ambaye kwa kufuata mfano wake unaweza kurekebisha makosa yako yote, ukafuta ghasia zote katika maisha yako na kurejesha nidhamu na mpangilio mzuri katika maisha yako. Kwa kuifuata nuru na muongozo wake, unaweza kuzishinda shida za maisha na kupata furaha ya kweli.

Kwa hakika, maisha yake ni shada la maua lenye maua na mawaridi maridadi na maridhawa yenye manukato adimu na yenye uzuri wa juu kabisa.

❀

Kama unashuhudia haki ikienea ulimwenguni, kama kuna upendo unaowaunganisha matajiri na masikini, kama matajiri katika jamii wanaamiliana na maskini kwa ukarimu kwa kuwapa msaada wakati muafaka, kama wenye nguvu wanawalinda wanyonge, kama wenye afya wanawasaidia wagonjwa, kama wenye mali wanawajali yatima na kuwalisha wajane, basi tambua kuwa mazuri yote haya yamerithiwa kutoka kwa mitume na wafuasi wao.

Kwa hakika hilo linaonekana kwa urahisi mno katika maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w). Hii ni kwasababu yeye ndiye kilele cha utume. Hata makafiri wasiokuwa na upendeleo wamelazimika kuukubali na kuuthibitisha ukamilifu wake. Mwanahistoria wa Kiingereza, Thomas Carlyle,

anaelezea maoni yake juu ya Mtume (s.a.w) katika kitabu chake kiitwacho, *On Heroes, Hero-Worship and the Heroic in History,*[27] alipochagua watu wenye ubora wa tabia, akili, ukubwa na uhodari katika nyanja mbalimbali na kuyachambua maisha yao na kazi zao.

Kwa mfano, Carlyle ameainisha wale wanaostahili kuwa washairi bora, kamanda bora, n.k. Bwana Carlyle, Mkristo aliyekiri imani yake katika kitabu chake, amemwelezea na kumchambua Mtume Muhammad(s.a.w) kama mtume bora kati ya mitume wote.

Katikati mwa karne hii huko Lahey, Uholanzi, kundi la wanazuoni na wanafikra wakubwa waliwachagua watu mia moja waliowaona kuwa ni bora kabisa katika historia ya ulimwengu, na hawakusita kumchagua Mtume Muhammad (s.a.w) kuwa nambari moja kabisa katika orodha hiyo.

Ubora wa kweli ni ule unaoshikiliwa na mtu ambaye anakubalika na kutambuliwa na hata wapinzani wake. Maadili na hekma za Mtume Muhammad (s.a.w) zinakubalika hata na wale wasioiamini dini aliyokuja nayo. Hii ni kwa sababu shakhsia ya kipekee ya Mtume Muhammad (s.a.w) ilikusanya ukamilifu wa kimaadili na wa kitabia unaokubaliana na mazingira mbalimbali kwa namna mbalimbali. Mfano wa maisha yake (*sirah*) ndio pekee unaoweza kutumika kama ruwaza au kielelezo kinachotakiwa kufuatwa na watu wa kada mbalimbali na hali mbalimbali za maisha. Hakika yeye ndiyo msingi wa malezi ya wanadamu ulimwenguni koto. Huangaza nuru kwenye njia ya wale wanaotafuta nuru. Muongozo wake ni nuru yenye kuwaangazia wale wanao-

27. Carlyle, Thomas, On Heroes, Hero-Worship and the Heroic in History; University of Nebraska Press, 1966.

tafuta njia ya haki; ni nuru isiyompoteza mtu. Hakika yeye ndiye muongozo pekee kwa wanadamu wote.

Watu waliokaa katika vikao vyake kwa ajili ya kupata muongozo wake ni mfano wa ulimwengu ambao ndani yake kuna watu wa aina zote. Mataifa yote, licha ya tofauti katika lugha, rangi na jinsia, viwango vya kijamii na kiutamaduni, yaliungana katika vikao hivyo. Vikao hivyo havikuwa na kizuizi wala kumbagua mtu. Vikao hivyo vilikuwa karamu ya hekma na maarifa ambavyo havikubagua rangi ya mtu, bali viliamiliana na wanadamu kwa uanadamu wao. Hivyo, hapakuwa na tofauti yoyote baina ya mnyonge na mwenye nguvu.

Watazame wafuasi wa bwana wetu, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w). Utawaona watu wafuatao waliokuwa wakiheshimika sana: Najashi, mfalme wa Abyssinia; Farwa, kiongozi wa Ma'an; Zulkilah, kiongozi wa Himyar; Daylami wa Firuz; Marakabud aliyekuwa miongoni mwa machifu wa na viongozi wa Yemen; Ubayd na Jafar aliyekuwa miongoni mwa magavana na watawala wa Umman.

Kwa upande mwingine, pembezoni mwa wafalme na viongozi hao mashuhuri, utawaona watumwa na masikini, watu wasiokuwa wa kuwasiadia, kama Bilal, Yasir, Habbab, Ammar na Abu Fukayha, pia wajakazi na wanawake wasiokuwa na mtu wa kuwasaidia, kama Sumayya, Lubayna, Zinnira, Nahdiyya na Umm Abis.

Kati ya maswahaba wake Watukufu, kulikuwa na watu wenye akili bora kabisa, uelewa wa hali ya juu na fikra angavu na madhubuti, pia watu mahiri katika stadi nzuri sana; watu waliokuwa na ufahamu wa kina wa siri za ulimwengu na waliokuwa na uwezo wa kuongoza nchi mbalimbali kwa hekma na uwezo wa hali ya juu.

Wafuasi wa Mtume (s.a.w) walitawala miji na majimbo mbalimbali. Watu walipata furaha kupitia kwao, wakaonja ladha ya haki na uadilifu. Wafuasi wake walieneza amani na utulivu. Kutokana na Mtume, watu waliishi kwa upendo na kuamiliana kama kaka na dada.

Lafayette, aliyeasisi misingi ya mapinduzi ya Ufaransa ya mwaka 1789, aliidurusu mifumo yote ya kisheria kabla ya tangazo la Azimio la Haki za Binaadamu na kuubaini ubora wa sheria ya Kiislamu, jambo lililomfanya atamke wazi:

"Ewe Muhammad! Hakuna aliyeonesha kiwango ulichofikikia katika kuasisi haki na uadilifu!"

❀

Tabia na nguvu ya kiroho Mtume (s.a.w) vilikuwa na uwezo mkubwa sana kiasi cha kuinyanyua juu jamii iliyokuwa ya kishenzi, watu waliokuwa hawajui historia ya mwanadamu, akaipaisha juu kwenye daraja na hadhi ya kuwa maswahaba; hii ni daraja ambayo wengine hawawezi kuifikia. Aliwaleta pamoja chini ya dini, bendera, sheria, utamaduni, ustaarabu na serikali moja.

Aliwabadilisha wasiosoma na wasiokuwa na utaratibu kuwa wasomi; aliwabadilisha washenzi kuwa wastaarabu, wahalifu na wakosa adabu kuwa watu wenye kumtambua Mwenyezi Mungu. Aliwafanya wawe wanadamu wa kipekee walioishi kwa kumheshimu na kumpenda Mwenyezi Mungu.

Jamii ambayo haikuwa imetengeneza hata mtu mmoja ambaye ni kielelezo cha mfano kwa karne kadhaa sasa ilitengeneza watu wengi waliopambwa kwa nuru na uongofu. Na waliibeba nuru yao kwenda kona za mbali za ulimwengu;

kila mmoja alibeba mwenge wa imani, maarifa na hekma. Nuru iliyokuwa imeshuka jangwani ikasambaa kwa watu wote. Malengo ya kuumbwa kwa ulimwengu yakatambulika na kufikiwa.

Japokuwa aliziteka nyoyo za watu kama mwalimu bora, nafasi aliyoifikia katika kipindi kifupi ambacho hata wafalme wa ulimwengu huu hawawezi kuipata, aliendelea kuishi maisha yake ya awali yaliyojaa unyenyekevu, na hakujali wingi wa mali ambazo sasa zilikuwa zikipatikana kwa urahisi. Aliendelea kuishi kama masikini katika makazi yake yaliyojengwa kwa matofali ya tope. Alilala kwenye godoro jembamba lililojazwa majani ya mtende. Alivaa mavazi ya wastani na ya staha. Kiwango chake cha maisha kiliendelea kuwa chini ya kile cha watu masikini. Wakati mwingine, hakuwa na chakula na ilimpasa kufunga jiwe tumboni mwake ili kutuliza njaa, huku, wakati huo huo, akionesha shukrani kwa Mwenyezi Mungu. Aliendelea kuomba na kuabudu kwa unyenyekevu japokuwa alishasamehewa makosa yake yote yaliyotangulia na ya baadaye. Aliutumia usiku kuswali kiasi kwamba hadi miguu yake ilivimba. Aliwapa masikini msaada pindi tu walipohitaji. Alikuwa chanzo cha furaha kwa masikini na wale wote waliokuwa wapweke. Alitumia muda mwingi kukaa pamoja na wanyonge na kuwafariji wasio na msaada, bila kujali Utukufu wake. Aidha, aliwalinda zaidi kuliko wengine kwa ukarimu na wema wake usiokuwa na mwisho.

Siku alipoikomboa Makkah, mji ambao watu walimuona kuwa mtu mwenye nguvu na madaraka makubwa, mwananchi mmoja alimsogelea. Alimuomba huku akitetemeka:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!Nifundishe Uislamu!"

Kwanza alimtaka yule bwana atulie kwa kumkumbusha udhaifu katika maisha yake mwenyewe:

"Tulia ndugu yangu! Mimi si mfalme wala chifu! Mimi ni yatima wa jirani yako wa zamani (akimaanisha mama yake) aliyekuwa akila nyama kavu!"[28]

Kwa maneno haya, aliipatia historia kilele cha unyenyekevu, hatua ambayo hakuna yeyote aliyeifikia.

Siku hiyo hiyo, Abu Bakr, aliyekuwa rafiki yake kule pangoni wakati wa Hijra, alimleta baba yake kwa Mtume huku akiwa amembeba mgongoni kwa sababu alikuwa mzee sana na hakuweza kutembea. Alitaka baba yake ausikie moja kwamoja ujumbe wa Mtume (s.a.w) .

Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Ewe Abu Bakr! Kwa nini umemsumbua baba yako hali ya kuwa ni mzee? Kwani ningeshindwa kumfuata kwake?"[29]

❀

Mataifa mengi yaliingia kwa hiari chini ya ulinzi wa dola yake. Dola yake ilisambaa Arabia yote. Alikuwa na uwezo wa kufanya chochote apendacho lakini aliendelea kuwa mnyenyekevu. Alieleza kuwa hakuwa na mamlaka juu ya kitu chochote; bali kila kitu kinadhibitiwa na uwezo wa Mwenyezi Mungu. Mara kwa mara, alikuwa akifikiwa na mali nyingi. Misafara ya ngamia ilifurika Madina ikiwa imebeba mali. Mali yote hiyo alikuwa akiigawa kwa masikini naye akaendelea kuishi maisha ya unyenyekevu kama mwanzo. Alisema:

28. Ibn Majah, At'imah 30; al-Hakim, al-Mustadmk, II, 506; al-Tabarani, al-Mu'jam al-Awsat, II, 64.
29. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 349; Ibn Hibban, al-Sahih, XVI, 187; al-Hakim, al-Mustadrak, III, 48.

"Ikiwa nitamiliki dhahabu sawa na mlima Uhud, sitaiweka zaidi ya siku tatu, isipokuwa kwa ile ntakayolipia madeni yangu."[30]

Siku kadhaa zilikuwa zikipita bila moto kuwaka nyumbani kwa Mtume (s.a.w). Muda mwingi alilala akiwa na njaa.

Siku moja, Umar alikuja nyumbani kwa Mtume (s.a.w) . Alikitazama kwa makini chumba cha Mtukufu Mtume (s.a.w). Chumba kilikuwa kitupu. Kulikuwa tu na godoro lililotengenezwa kwa majani ya mtende. Mtume (s.a.w) alilitumia kulalia. Majani yale makavu kwenye godoro yaliacha alama mwilini mwa Mtume. Kulikuwa na unga wa shayiri kwenye kona ya chumba. Mbele yake, kulikuwa na kiriba cha maji. Hapakuwa na kitu kingine zaidi ya hivyo mle chumbani. Hizi ndizo zilizokuwa mali zake; na hiki ndicho kipindi Arabia yote iliunyenyekea utawala wake. Umar alishusha pumzi nzito alivyoona hali ile. Hakuweza kujizuia kulia. Wakati machozi yalipoanza kutiririka kutoka machoni mwa Umar, Mtukufu Mtume (s.a.w) alimuuliza:

"Kwa nini walia, Ewe Umar?"

Umar akajibu:

"Kwa nini nisilie? Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Wafalme wa Roma na Iran wanaogelea katika raha! Lakini, Rasulullah analala kwenye godoro lililotengenezwa kwa majani ya mtende!"

Mtume Muhammad (s.a.w) alimfariji Umar na kumwambia:

30. Bukhari, Tamanni 2; Muslim, Zakdt 31; Ibn Majah, Zuhd 8; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 256.

"Ewe Umar! Mwache Kaisari na mfalme wa Iran (Kisra) wafurahie ulimwengu huu! Hakika furaha ya peponi inatutosha!"[31]

Katika tukio jingine alisema:

"Ulimwengu huu una lipi kwangu? Uhusiano wangu na ulimwengu huu ni sawa na msafiri anayesafiri wakati wa kiangazi, akapumzika chini ya kivuli cha mti, kisha akaamka na kuendelea na safari yake."[32]

Mwelekeo wake wa maisha ulikuwa mwelekeo uliokamilika. Maisha yake ni mfano kamili kwa wafuasi wake, wawe maskini au matajiri, wanyonge au wenye nguvu.

Wakati anafariki dunia, hakuacha *dirham* au *dinar* hata moja, mtumwa au kondoo. Aliacha nyumbu mweupe wa kike, upanga na sehemu ya ardhi huko Fadak, ambayo alitoa kama sadaka. Hii ina maana kuwa kuwa hakuacha mali yeyote. Aidha, alihofia kuwa Waislamu wangejaribu kuwapa sadaka watu wa nyumba yake, aliwakataza wasipokee .

Mifano hii inaonesha kuwa mtu huyu ambaye hakusoma wala kuandika, ambaye alizaliwa katika ulimwengu usiostaarabika ni kiongozi wa kweli wa nyakati zote, zamani, sasa na baadaye, na mfano wake hauwezi kufikiwa na yeyote.

Mali, starehe, ufalme, raha au umaarufu havikuwa na thamani yoyote kwake. Alipokuwa akipambana kuweka msingi wa imani ya Mungu mmoja(*tawhid*), utajiri na fahari ya ulimwengu huu kwake havikuwa chochote zaidi ya umaridadi usio na maana.

---

31. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 298; al-Tabarani, al-Mu'jam al-Kabir, X, 162.
32. Tirmidhi, Zuhd 44; Ibn Mâjah, Zuhd 3; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 301.

Bibi Aisha (r.a) anasimulia kuwa alitembelewa na mwanamke mmoja wa Kiansari. Alipoona kuwa kitanda cha Mtume (s.a.w) kilikuwa na godoro la kawaida, lililokuwa limekunjwa na kuwekwa pembezoni mle chumbani, alikimbia hadi nyumbani kwake akaleta godoro zuri, lililotengenezwa kwa sufi. Baadaye, Mtume (s.a.w) alipoona godoro lake limebadilishwa na kuwekwa godoro zuri zaidi, alionesha kukataa na kumwambia mkewe, Aishah:

"Ewe Aisha! Rudisha hili godoro kwa mwenyewe! Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, kama ningetaka, Mwenyezi Mungu angenipa milima yenye dhahabu na madini ya fedha ikanitumikia."[33]

Mfano huu unatosha kabisa kuelezea jinsi ambavyo Mtume (s.a.w) hakushikamana na ulimwengu huu hata kidogo.

Pamoja na sifa hizi adhimu, moja kati ya sifa zake kubwa kabisa ni upendo wa ahali ya juu aliokuwa nao kwa *ummah* wake, ambayo imeelezewa vizuri katika aya ifuatayo:

"Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe, yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni, anakuhangaikieni sana. Kwa waumini ni mpole na mwenye huruma." (Qur'an, Tawba, 9:128)

Kiwango kidogo cha Shakhsia tukufu ya Mtume (s.a.w) kinachojulikana na watu ni ncha ndogo tu ya mlima wa barabu; shakhsia yake ni kilele cha ruwaza na mfano wa tabia ya mwanadamu. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba Mtume kama "*us-watul hasanah*", yaani mfano bora uliokamilika unaotakiwa kufuatwa na wanadamu wote.

33. Ahmad ibn Hanbal, Kitâb al-Zuhd, p. 53; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, II, 173; Ibn Abî 'Âsim, Kitâb al-Zuhd, I, 14.

Hivyo, alimnyanyua Mtume (s.a.w) kwa kumpitisha kwenye hatua mbalimbali, akaanza kwa kumfanya kuwa "yatima" , hatua inayohesabika kuwa ni daraja ya chini kabisa ya uwezo na nguvu katika jamii, na kisha akampandisha juu kupitia hatua zote za maisha, mpaka kwenye kiwango cha juu kabisa cha madaraka na uwezo, nayo ni utume na uongozi wa dola.

Lengo la kumnyanyua hatua kwa hatua ni kuwawezesha watu wa aina tofauti katika jamii waweze kumuona Mtume kama mfano mzuri wa tabia na wao waweze kuiga, kulingana na uwezo wao na vipawa vyao. Watu wetu, walioielewa nukta hii vizuri, walizalisha aina ndogo (*ism-i tasghir*) ya jina Muhammad, na kulitumia kama jina la muhimu kwa kila mtu. Aina hii ya jina Muhammad kwa Kituruki ni Mehmetjik, lenye maana ya Muhammad mdogo. Nomino Mehmetjik (Muhammad mdogo) inaleta akilini taswira ya ruwaza ndogo ya Mtume (s.a.w) kwa kila mwanadamu, hususan kwa wale wanaomuamini Mwenyezi Mungu Mmoja na kumtii. Wakati huo huo, dhana hii inamhamasisha kila mtu kuwa kama Muhammad (s.a.w) kulingana na vipawa vyake mwenyewe.

❀

Hata alipokuwa mtoto, hakuna dosari yoyote iliyoonekana katika shakhsia za Mtume Muhammad (s.a.w) – tofauti na watu wengine waliokuwa waliodai kuwa miongozo na viongozi wa watu, hasa wanafalsafa. Shakhsia yake haikukua na kukamilika hatua kwa hatua, kama ilivyo kwa viongozi wengine. Haya yalikuwa matokeo ya kadari na msaada kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Hata kipindi cha utoto alionesha tabia bora zenye ukamilifu wote, jambo lililoonesha sifa ya jukumu ambalo angekabidhiwa hapo baadaye.

Mawazo chanya au hasi ya wanafalsafa, ambao akili zao hazikuongozwa na ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kuhusu amani na maelewano ya kijamii yamebaki katika majalada ya kurasa za vitabu vyao, huku mawazo yao machache yaliyopata bahati ya kutafsiriwa kwa vitendo hayakudumu kabisa bali yalitoweka na kusahaulika. Aidha, wanafalsafa walishindwa kuwa kama mfano au vielelezo halisi katika maisha yao wenyewe au kutafuta mifano kutoka kwa watu wengine waliowaainisha katika misingi yao kuhusu ukamilifu wa tabia ya mwanadamu.

Lakini kwa upande wa tabia ya Mtume (s.a.w), ilikuwa kigezo halisi cha maadili na mkusanyiko bora wa vielelezo. Kwa mfano, mwanafalsafa Nietzsche alieleza mtazamo wake kuhusu watu wenye uwezo kupita kiasi, lakini alishindwa kuidhihirisha dhana hii ya mwanadamu wa ajabu kwa vitendo halisi vinavyotokea katika maisha ya kila siku. Kwa hiyo, imebaki kama nadharia tu. Lakini kwa upande wa maadili ya Kiislamu, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitumika na ataendelea kutumika kama muongozo kwa mwanadamu kwa matendo yake yote kama mwanadamu, ambayo ni kilele cha ubora na ukamilifu.

Aristotle, kwa upande mwingine, ameainisha kanuni na sheria za maadili. Lakini, huwezi kupata mtu hata mmoja aliyepata furaha kwa kuitumia falsafa ya Aristotle. Hii ni kwa sababu nyoyo za wanafalsafa wengi hazipitii kwenye mchakato wa utakaso, kama ilivyo kwa mitume, na maneno na matendo yao hayajakamilishwa kwa msaada wa ufunuo. Kwasababu hiyo, mifumo yao inabaki katika vyumba vya mkutano na kwenye kurasa za vitabu tu, na si katika maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Bwana wetu, Mtume Muhammad (s.a.w), kabla ya kuka-

bidhiwa jukumu la utume, aliaminiwa sana na watu waliomjua kama "mkweli" na "mwaminifu". Alianza kazi yake baada ya kuwa na utambulisho huo.

Watu walijua sifa zake nzuri, uzuri na ukamilifu wake kabla ya utume wake na walimpenda. Watu wake, waliompa sifa ya al-Amin (mwaminifu), waliukubali uamuzi wake bila pingamizi lolote walipoangukia katika mzozo wa jinsi ya kulirejesha Jiwe Jeusi mahali pake wakati wa ukarabati wa Kaabah.

Mtume (s.a.w) alijiepusha sana katika maovu yote na ukiukaji wa haki za wengine. Kundi pekee alilojiunga kabla ya utume ni *Hilf al-Fudul*, yaani Mapatano ya Wema. Hii ni kwa sababu *Hilf al-Fudul* lilikuwa kundi lililojitolea kupigunia haki, na msingi wa maamuzi yake yalikuwa kama ifuatavyo:

"Kama haki za mwenyeji wa Makkah au mgeni zitakiukwa, mhalifu atakabiliwa haraka, na tutakuwa upande wa Yule aliyedhulumiwa mpaka uovu ulipizwe. Tutahakikisha haki, uadilifu na maelewano ya jamii vinaimarishwa."

Makubaliano hayo dhidi ya uonevu na ukiukwaji wa haki yalimvutia sana Mtume (s.a.w), hata akasema baada ya kuwa Mtume:

"Nilikuwepo katika nyumba ya Abdullah ibn Jud'an pamoja na wajomba zangu. Nisingekuwa na raha kama ningepewa ngamia wekundu (akimaanisha utajiri wa ulimwengu huu). Nitajiunga na kundi hilo hata nikialikwa leo kujiunga nalo."[34]

Mfano huu na mingine mingi isiyokuwa na kikomo inayoonesha uadilifu, huruma na ukarimu katika maisha

34. Ibn Sa'd, al-Tabakât, 1,129; Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabaxviyyahh, 1,133-134; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 190-193; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VI, 367.

ya Mtume (s.a.w) ni mifano inayotakiwa kufuatwa na wanadamu wote hadi siku ya mwisho. Kama ambavyo jicho lina uwezo wa kupambanua mwanga wenye nuru, ukweli wa mshumaa huu unaoangaza juu ya ulimwengu hauwezi kukanushwa, angalau hata katika ulimwengu wa ndani. Ni kutokana na ukweli huo kwamba, wasomi wengi wasiokuwa Waislamu waliukubali kwa dhati kabisa ubora na mafanikio yake baada ya kufanya tathmini ya kiuadilifu. Miongoni mwao ni Thomas Carlyle, kama tulivyoashiria kabla, anaelezea katika kitabu chake cha *On Heroes, Hero-Worship and the Heroic in History*[35], kuwa kuzaliwa kwa Mtume kuliakisi ujio wa nuru kutoka katika kiza.

Ensaiklopidia maarufu ya *Britannica* pia imethibitisha ubora wake kwa kutamka kuwa hakuna mtume au mwanamageuzi mwingine yeyote wa dini aliyefikia mafanikio yaliyofikiwa na Mtume Muhammad (s.a.w).

Mwandishi Stanley Lane-Poole, anakiri kuwa siku Muhammad (s.a.w) alipowashinda maadui zake ni siku ile ile aliyoshinda vita kubwa kabisa ya maadili dhidi ya nafsi yake mwenyewe, baada ya kuwasamehe Maqurayshi na watu wote wa Makkah.

Hali kadhalika, mwandishi Arthur Gilman alibaini Utukufu wa Mtume wakati wa kiukomboa Makkah. Uzito way ale aliyotendewa na watu wa Makkah ungemfanya alipize kisasi. Lakini, alilikataza jeshi lake kumwaga damu ya aina yoyote. Alionesha huruma kubwa na kubaki kuwa mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu.

35. Tazama ukurasa wa 51?.

Mtume (s.a.w) kama alivyotazamwa na makafiri

Mtume Muhammad (s.a.w) aliwavutia waabudu masanamu wa kiarabu kwa uaminifu wake katika zama za ujinga (*al-Jahliyya*). Hata Abu Jahl, adui mkubwa wa Uislamu, siku moja alimwambia Mtume : "Ewe Muhammad! Sikuiti mwongo, ila sipendi dini uliyoileta..."[36]

Wapinzani wake wakubwa waliukubali uaminifu wa Mtume (s.a.w) nyoyoni mwao, lakini kwa nje walimpnga kutokana tu na kiburi chao.

Qur'an imelielezea hili kama ifuatavyo:

"Tunajua ya kwamba yanakuhuzunisha wanayo yasema, Basi hakika wao hawakukanushi wewe, lakini hao madhalimu wanazikataa ishara za Mwenyezi Mungu." (Qur'an, An'am, 6:33)

Heraclius, mfalme wa Warumi wakati huo, aliyewashinda Waajemi mwaka 628 AC, alipokea barua kutoka kwa Mtume wakati akiwa Syria. Barua hiyo ilikuwa ikimlingania, kumuita na kumkaribisha katika Uislamu. Heraclius alionesha kuvutiwa na barua ile badala ya kukasirika.

Alitaka kuuliza na kupata taarifa na habari zaidi kuhusu dini hii mpya. Kwa maana hiyo, aliagiza kwamba watu wanaotoka katika ardhi ya Mtume huyo mpya (s.a.w) wapelekwe kwake. Wakati huo, Abu Sufyan, ambaye alikuwa adui mkubwa wa Mtume, alikuwa Syria akiongoza msafara wa wafanyabiashara wa Makkah. Ilikuwa ni mwaka wa sita Hijiria na kulikuwa na makubaliano ya amani kati ya Makafiri wa Makkah na Mtume (s.a.w). Askari wa Heraclius, waliokuwa wanawatafuta watu kutoka Makkah ili kuwapa habari

36. Tirmidhi, Tafsîr Sûrah 6,1; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 345.

za Mtume mpya, walikutana na Abu Sufyan na wenzake na kuwapeleka kwa mfalme.

Wakati huo Heraclius na watu wake walikuwa Ilya au Bayt al-Maqdis. Heraclius, akiwa amekaa pamoja na viongozi wa Kirumi, aliwakaribisha na kuongea nao kupitia mkalimani. Heraclius aliuliza:

"Nani ambaye ni ndugu wa karibu wa mtu huyu anayedai kuwa yeye ni mtume?"

Abu Sufyan akasema:

"Mimi ni ndugu yake wa karibu." Heraclius akaagiza:

"Msogezeni karibu yeye na wenzake! Nitakapozungumza naye wenzake wakae jirani naye."

Akamgeukia mkalimani wake na kumwambia:

"Waambie kuwa nitamuuliza huyu bwana baadhi ya maswali kuhusu Mtume mpya. Ikiwa atasema uongo wanatakiwa wanijulishe kuwa anasema uongo."

Alipokuwa anasimulia kisa hiki, Abu Sufyan alisema "Ninaapa kwa Mwenyezi Mungu, kama si khofu ya kuumbuliwa na wenzangu, ningeweza kumsemea uongo." Abu Sufyan anasimulia maongezi kati yake na Heraclius kama ifuatavyo:

Swali la kwanza alilouliza Heraclius lilikuwa:

"Ni ipi Nasaba yake?"

Nikajibu:

"Nasaba yake inaheshimika sana kati yetu!"

"Kuna yeyote kati yenu aliyewahi kudai utume kabla yake?"

"Hapana", nikajibu.

Akauliza:

"Je, kulikuwa na mfalme yeyote miongoni mwa wazazi wake au babu zake?"

Nikajibu:

"Hapana."

Akauliza:

" Je, wafuasi wake ni wa tabaka la watu wajuu au la watu wa chini?"

Nikajibu:

"Kutoka tabaka la watu wa chini."

Akauliza:

"Je, idadi ya wafuasi wake inaongezeka au inapungua?"

Nikajibu:

"Idadi yao inaongezeka."

Akauliza:

"Kuna yeyote kati yao aliyeiacha dini hii mpya kwa kutoipenda?"

Nikajibu:

"Hapana."

Akauliza:

"Mliwahi kumtuhumu kusema uongo kabla ya jambo hili?"

Nikajibu:

"Hapana."

Aliendelea kuuliza zaidi:

"Amewahi kuvunja ahadi?"

Nikajibu:

"Hapana, anatimiza ahadi zake, lakini sasa hivi tumefanya naye makubaliano ya amani kwa kipindi fulani na hatujui atafanya nini."

(Abu Sufyan anasema, "Hiki ndicho kitu pekee ambacho nilikichomeka katika majibu yangu ili kumtia kasoro.")

Heraclius akauliza

"Mumewahi kupigana nae vita?"

Nikajibu:

"Ndio."

Heraclius akauliza:

"Matokeo ya vita hivi yalikuwaje?"

Nikajibu:

"Wakati mwingine tulimshinda, wakati mwingine alitushinda."

Akauliza:

"Je, anawaamrisheni kufanya nini?"

Nikajibu:

"Anatutaka tumuamini Mungu mmoja tu, bila kumshirikisha chochote na kuacha kuabudu masanamu waliyoyaabudu babu zetu. Anatuamrisha kuswali, kuwa waaminifu na wasafi, kuilinda heshima yetu na kuimarisha uhusiano mzuri na wakaribu kwa ndugu zetu ."

Kisha Heraclius akamwambia mkalimani:

"Mwambie niliulizia nasaba yake akasema kuwa anatokana na nasaba inayoheshimika sana kati yao. Mitume wote wanatoka na nasaba zinazoheshimika sana katika jamii zao.

Nikauliza kama kuna mtu aliyewahi kuja na madai ya utume kama hayo, akajibu hapana.

Nikauliza kama kulikuwa na mfalme katika mababu zake; akasema hapana. Kama angelikuweko, ningeshuku kuwa alitaka amiliki taji la ufalme.

Nikauliza kama alishawahi kumuona akiongopa kabla ya utume, akajibu hapana. Nina uhakika kuwa mtu ambaye hawaongopei watu hawezi pia kuongopa kuhusu Mungu.

Niliuliza kuhusu wafuasi wake, kama wanatoka katika tabaka la watu wa juu au tabaka la watu wa chini. Akasema wanatoka katika tabaka la watu wa chini. Inajulikana vyema kuwa wafuasi wa mitume wanatoka katika tabaka la watu wa chini katika jamii.

Nikataka kujua kama idadi ya wafuasi inaongezeka au inapungua. Akasema kuwa wanaongezeka.

Sifa mojawapo ya dini ya kweli ni kwamba wafuasi wake huwa wanaongezeka katika hatua ya awali.

Nikauliza kama kuna mtu aliyeiacha dini hii mpya baada ya kuikubali. Akajibu hapana. Hivi ndivyo jinsi furaha ilivyo pindi raha ya imani ikiingia moyoni na kuota mizizi.

Niliuliza kama amewahi kuvunja ahadi; akajibu hapana. Mitume wako hivyo, kamwe hawavunji ahadi.

Nikauliza huwa anataka wafuasi wake wafanye nini. Akajibu kuwa anawaamuru kumuamini Mungu mmoja, na wasimshirikishe chochote, na pia anawataka wawe wanaswali, kuwa waaminifu, na kuishi maisha ya heshima.

Kama alichokisema ni kweli, muda si mrefu utawala mtu huyu atafika mpaka kwenye ardhi hii niliyosimama sasa. Nilijua kuhusu ujio wa Mtume, lakini sikujua kama atatoka kati yenu. Kama ningekuwa pamoja naye, ningemuosha miguu yake."

Kisha Heraclius akaulizia barua iliyoletwa kwake na mjumbe Dihya. Barua ikaletwa na kusomwa mbele yake. Ndani ya barua kuliandikwa yafuatayo:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma na Mwenye kurehemu.

"Kutoka kwa Muhammad, mtumishi na mjumbe wa Mwenyezi Mungu, kwenda kwa Heraclius, kiongozi wa Warumi

"Amani iwe kwao wale wote wanaofuata njia sahihi.

"Nakulingania kwenye Uislamu. Ingia katika Uislamu, utapata wokovu na Mwenyezi Mungu atakulipa mara mbili. Lakini kama ukikataa utalipwa kwa yale yatakayofanywa na raia wako pia.

"Sema:Enyi watu wa kitabu, Njooni kwenye neno lililo sawa

baina yetu na nyinyi, Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote, walatu sifanyane sisi kwa sisi kuwa waola, walezi badala ya Mwenyezi Mungu. Na wageukao basi semeni shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu." (Qur'an, Ali Imran, 3:64)

Abu Sufyan anasema

"Baada ya Heraclius kusema kile alichokisema na baada ya barua kusomwa, kelele zilisikika na sauti zilipazwa. Hivyo walitutoa nje."

Nikawaambia wenzangu:

"Nguvu ya Muhammad inakuwa. Hata wafalme wameanza kuusikiliza ujumbe wake. Tazama hata mfalme wa Bani Asfar (Warumi) anamuogopa!.. . Kuanzia hapo nikawa na imani na uhakika kuwa siku moja atafanikiwa. Mwishowe, Mwenyezi Mungu akanibariki kuwa Muislamu ."[37]

Kwa mtazamo wetu, msimamo wa mfalme wa Rumi, Heraclius kuhusu alichokisikia, haukutokana na sababu binafsi pekee.

Uharibifu na uliofanywa ndani ya dini ya Kikristro, ambayo kwa asili ilikuwa ni dini ya kweli na inayoamini kuwepo kwa Mungu mmoja tu, ni jambo jipya lililokuwa limezushwa. Vita ya kupigania ikoni, iliyodumu kwa karne nyingi, ndiyo ilikuwa imeisha na makanisa yakajazwa picha namasanamu. Ukristo ukajitenga mbali na imani ya Mungu MMoja, na kujisalimisha moja kwa moja kwenye imani ya Utatu. Kutokana na uharibifu walioufanya wa imani sahihi, Uislamu ukaletwa kurejesha "imani ya kweli". Licha ya

37 Bukhârî, Jihâd 102; Muslim, Jihâd 74.

uharibifu huo, walikuwepo baadhi ya watu wengine walioendelea kubaki na imani yao ya kumuamini Mungu Mmoja. Kwa mfano, wahamaji waliohamia Abissinia kwa sababu ya manyanyaso mazito mjini Makkah, walikutana na mfalme Najashi, ambaye alikuwa ameendelea kuwa mfuasi wa imani ya Umoja wa Mungu. Alichora hata msitari ardhini kwa fimbo yake na kusema:

"Tofauti kati ya imani yangu na kile mnachoongea ni kidogo zaidi ya upana wa mstari huu."

Mfalme Najashi alikuwa katika madhehebu ya Arian, yaliyodumisha itikadi halisi ya Ukristo wa mwanzo. Na inawezekana pia hata Heraclius alikuwa na itikadi hiyo. Lakini hakuna ushaidi kama alisilimu. Ikumbukwe kwa mara nyingine kuwa suala la imani ni Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kwa upande mwingine, tukio hili linaonesha kuwa hata wale ambao hawakuukubali ujumbe wake walikiri na kuutambua uaminifu na ukamilifu wa tabia njema za Mtume (s.a.w). Kabla ya kuhamia Madina, yaani Hijra, Mtume Muhammad alikuwa amepewa amana zenye thamani kubwa sana na makafiri wa Makkah ili awatunzie.

Alipoamua kuihama Makkah, alimteua Ali azirudishe amana hizo kwa wenye nazo katika mji wa Makkah kwa niaba yake.

❀

Mshairi Kamal Adib Kurkcuoglu anatoa wosia na kuwaasa wale walioghafilika ambao wanaacha kufuata tabia maridhawa za Mtume- ambazo miongoni mwake zimetajwa hapo juu.

Ole wako, ole wako, ukianguka kutoka katika jicho la moyo!
Ni adhabu tosha ya ulimwengu huu na akhera
Kwa wale wasiokuwa na utambuzi wa kiroho!

Mwenyezi Mungu atujalie tuwe kati ya wafuasi wake wanaomtii kwa upendo na kuiga sifa zake. Alikuwa kilele cha rehma na ukarimu. Alijitahidi kwa moyo wote kuwaongoa watu. Lakini walimlaani na kumpiga mawe. Radiamali yake kwa waliyomfanyia ni kuwaombea dua njema. Zayd ibn Haritha aliyeshangazwa na hili, alimuuliza:

"Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Wamekuumiza… ila bado unawaombea."

Akajibu:

"Ningefanya nini zaidi? Nimeletwa kwa reham, sijatumwa kwa ajili ya ghadhabu..."[38]

Hili halitoi ushahidi kuwa Mtume Muhammad alikuwa katika kilele cha utoaji, usafi wa moyo, hurumana ukarimu?

Watu waliowachukulia Krishna na Buddha kama miungu, Yesu kama mwana wa Mungu, na Fir'aun na Nimrod kama miungu, na wale walioabudu wanyama, au nguvu za asili kama vile moto, maji na hewa, wangemkubali kwa furaha kama "mungu" wao. Lakini, alitangaza waziwazi kuwa *"Mimi ni mwanadamu kama nyinyi . Isipokuwa nimeletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu mmoja…"* (Qur'an, Kahf, 18:110)

Aliongeza neno *abduhu,* lenye maana mja wake, mwanzo wa sentensi (*shahadah*) inayotamkwa katika kuukubali utume wake kwa sababu alitaka kuhakikisha kuwa Umma wake haupotei.

38. Muslim, Birr 87; Abu Ya'lâ, al-Musnad, XI, 35.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliweka wazi kuwa yeye hana mamlaka makuu. Kwa mfano, siku moja alisema:

"Hakuna atakayeingia peponi kwa thawabu tu za matendo yake."

Kila mmoja alishangaa. Wakauliza:

"Hata wewe, Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?"

Akajibu:

"Ndiyo, hata mimi.. . ! Labda kwa huruma ya Mola Wangu! Sitaweza kuingia peponi ila pale Baraka, Rehma na msamaha wake vitakaponifunika; matendo yangu pekee hayatatosha kuniokoa.. . !"[39]

Mfumo wa misingi hii ni neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambayo haiwezi kuingiliwa na wanadamu.

Ujumbe huu ni ujumbe safi na wakustajabisha, uliojaa uaminifu na utii. Ili kupata maana sahihi ya Qur'an na Sunnah, ni lazima kuwa karibu na kina kirefu cha moyo na tabia za Mtukufu Mtume Mtume (s.a.w).

Hakuna akili iwezayo kuzielezea kikamilifu sifa zake. Hakuna awezaye kuzielewa kikamilifu tabia zake na uhalisia wa maisha yake. Wanazuoni, wanafalsafa, Masultani wa nyoyo, hata malaika mkuu Jibril waaliochukulia kuwa karibu naye ni heshima na ni chanzo kikubwa kabisa cha furaha.

Ujumbe na kazi za mitume wote waliomtangulia zilikuwa katika muda na sehemu fulani, isipokuwa ujumbe

39. Bukhârî, Riqâq 18; Muslim, Munâfiqûn 71-72; Ibn Mâjah, Zuhd 20; Dârimi, Riqâq 24; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 235.

na kazi ya Mtume Muhammad (s.a.w). Aliletwa na Mwenyezi Mungu kuwa kiongozi Mkuu kwa wanadamu wote. Kwa kuwa mfumo adhimu wa tabia za mitume waliopita hazikutufikia, kusudio la ujumbe wa Mtume Muhammad (s.a.w) ni kuzikusanya pamoja kazi za ujumbe wa mitume wote waliotangulia, kuanzia kwamtume wa kwanza, na kwa sababu hiyo, Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyesimamia tabia zake, kila kitu kinachomhusu, na kutufikia kwa njia ya nyororo za wasimulizi wenyewe kuaminika. Usambazaji huu utaendelea kuwepo mpaka siku ya mwisho. Sababu ya kufanya hivi ni ili kila mtu aweze kumchulia kama mfano hai *(uswa hasanah).*

Waarabu walikuwa wakiapa kwa vitu wanavyovithamini mno. Japokuwa Mwenyezi Mungu hakuwahi kufanya hivyo kwa mitume wengine, katika Qur'an Tukufu ameapa kwa maisha ya Mtume (s.a.w) : *La a'mruk*! Mshairi wa Kiuthmaniya Shaikh Ghalib anakielezea kiapo hiki kama ifuatavyo:

Ewe kiongozi wangu! Wewe ni sultani wa mitume, wewe ni mfalme adhimu.

Ewe kiongozi wangu! Wewe ni chemichemi ya milele ya faraja kwa wanyonge.

Ewe kiongozi wangu! Wewe ni kiongozi wa wanadamu wote mbele ya Mwenyezi Mungu.

Ewe kiongozi wangu! Mwenyezi Mungu aliapa kwa maisha yako, "la a'mruk!"

Ewe kiongozi wangu! Wewe ni Ahmad, Mahmud na Muhammad!

Ewe kiongozi wangu! Wewe ni sultani wetu uliechaguliwa na Mwenyezi Mungu.

Sifa nyingine ya Mtume wetu adhimu (s.a.w) ni kuwa katika Qur'an Tukufu, Mwenyezi Mungu hakuzungumza naye kwa kutumia jina la Muhammad, bali alizungumza naye kwa "Ewe Nabi!", "Ewe Rasul!", "Ewe Muzammil!", "Ewe Muddathir!". Mitume wengine waliitwa kwa kutumia majina yao kama "Ewe Adam!", "Ewe Nuhu!", "Ewe Ibraham!", "Ewe Musa!", "Ewe Daudi!", "Ewe Issa!", "Ewe Zakariya!", "Ewe Yahya!" Utofautishaji huu unatuonesha upekee wa Mtume Muhammad (s.a.w).

Usisahau kumtolea salamu kwa *salawat* na *salam*! Kwa maana utauhitajia uombezi wake (*shafaah*) siku ya Kiyama, siku ya hesabau.



Sifa Na Tabia Adhimu Za Mtume Wa Rehma

(S.A.W)

“Ewe Mwenyezi Mungu ! Nipe wepesi katika kazi yangu kuliko uzito na uifanye kuwa na mwisho wenye baraka.” (Dua)

Katika historia, Mtume pekee na mtu ambaye maisha yake yote yameandikwa kwa undani kabisa ni Muhammad Mustafa (s.a.w). Matendo yake, maneno yake na hisia zake zote zimeandikwa na kuchukuliwa kuwa ukweli salama na sahihi wa kihistoria.

Maisha yake yatakuwa mfano kwa vizazi vijavyo, hadi siku ya mwisho. Kwenye Surah al-Qalam ndani ya Qur'an Tukufu, imeelezwa: *"Na hakika wewe una tabia Tukufu."* (Qur'an, Qalam, 68:4)

Hakuwa tu mwalimu aliyefundisha Qur'an kwa maneno; bali alikuwa pia mfano hai aliyefanya kwa vitendo yale yote yaliyoandikwa katika Qur'an Tukufu. Jabir anasimulia kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) anasema:

"Mwenyezi Mungu, Mtukufu, alinituma kuja kukamilisha tabia njema."[40]

Abdullah ibn Salam, mwanazuoni wa kiyahudi wa zamani aliyeslimu, alipokutana na Mtume (s.a.w) alitamalakiwa na nuru na hali ya kiroho aliyoiona usoni mwake. Alivutiwa sana na hali hiyo, akasema:

40. Muwatta, Husn al-khuluq 8; al-Bayhaqi, al-Sunan al-Kubra, X, 191; al-Qudat, Musnad al-Shihdb, II, 192; al-Tabarani, al-Mu'jam al-Awsat, VII, 74.

"Mtu mwenye wajihi wa aina hii hawezi kuwa muongo."[41] Kwa utambuzi huo, akasilimu.

Usafi wa Moyo wa Mtume wa Rehma (s.a.w)

Kama tulivyoeleza mapema kabisa, Mtume (s.a.w) ni tunu kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mfano kamili kwa wanadamu wote. Yeyote anayetafuta furaha anaweza kufuata mfano wake kwa kiwango anachoweza. Matendo yote ya Mtume (s.a.w) ni mfano halisi kwa wale wote wanaohitaji kwa dhati kuishi Kiislamu. Aidha, Kuna mambo ambayo ni lazima kuyazingatia unapotaka kufaidika na Dhati na maisha ya Muhammad (s.a.w):

1. Baadhi ya matendo yanaweza kufanywa isipokuwa na mitume tu kutokana na uwezo wa kipekee walio nao . Watu wengine hawawezi kuwaiga mambo hayo. Kwa hakika, hata Mtume (s.a.w) aliwaasa watu wake kuhusiana na jambo hili. Kwa mfano, mara kwa mara alikuwa akiswali usiku hadi miguu yake inavimba, na kufunga siku kadhaa mfululizo bila kupumzika.

2. Baadhi ya matendo yalikuwa maalumu kwa Mtume (s.a.w) peke yake: kwa mfano kuoa wake zaidi ya wanne na kukataa kupokea sadaka, aidha yeye mwenyewe au na uzao wake hadi siku ya mwisho.

Kuna mafunzo makubwa ambayo tunatakiwa tujifunze katika kugawa haraka ngawira za fungu lake zilizopatikana wakati wa mapigano. Alikuwa makini sana kwa hili katika maisha yake yote na hadi pumzi yake ya mwisho:

41. Tirmidhi, Qiyamah 42; Ibn Majah, Iqamah 174; Darimi, Salat 156; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 451.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa anaumwa sana na muda wa kukutana na Mola wake ulikuwa umewadia. Siku moja alimgeukia mkewe, Aishah (r.a) na kumwambia awagawie masikini dinar sita au saba alizokuwa nazo. Muda mchache baadaye, akaziulizia zile dinari. Alipogundua kuwa Aishah alisahau kuzitoa sadaka kwa sababu ya kushughulishwa na kazi ya kumhudumia, akasema apewe zili dinari, akaziweka kiganjani mwake kisha akasema:

"Muhammad, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, hatarajii kukutana na Mola wake bila ya kuzigawa dinari hizi kwa masikini.. ."

Kisha akazigawa kwa familia tano masikini za Kiansari katika mji wa Madina. Akasema:

"Sasa ninajisikia huru."[42]

Baada ya hapo, akasinzia.

Ubaydullah ibn Abbas anasimulia yafuatayo:

"Siku moja Abu Dharr aliniambia:

'Ewe mpwa wangu! Nitakusimulia kisa kimoja. '

Kisha akanisimulia kisa kifuatacho:

'Siku moja nilikuwa pamoja na mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Alinishika mkono na kusema:

'Ewe Abu Dharr! Kama milima ya Uhud ingegezwa kuwa dhahabu kwa ajili yangu, ningezitumia kwa njia ya Mwenyezi Mungu na nisingeacha hata *qirat*[43] moja wakati wa kufa kwangu. '

42. Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, VI, 49,86,182; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 491; al-Humaydî, al-Musnad, 1,135.
43. Qirat ni kipimo kidogo kabisa cha uzito, ambacho ni sawa na gramu moja ya sasa. Qirat ilikuwa sawa na punje tano za shayiri. .

Nikasema:

"Ewe, mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ni *qirat* au *qantar*[44] ambayo hutapenda kuicha nyuma?

Akasema:

'Ewe Abu Dharr! Ninapunguza, wewe unaongeza. Ninataka Akhera, wewe wataka dunia! Nisingeacha hata *qirat, qirat, qirat.'"*

Alirudia neno *qirat* mara tatu .[45]

Hali hii adhimu ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) unawakilisha kigezo cha juu kabisa. Wale wnaotakiwa kuifuata hawalazimishwi kufikia kiwango hicho. Kwa hakika, itakuwa tatizo kama ummah wa kislamu utajaribu kufuata kila mfano katika uhalisia wake kabisa. Aidha, hilo lipo nje ya uwezo wa mwanadamu. Hekma ya jambo hili inamhusu Mtume pekee yake.

Hayo yaliyotajwa sio matendo pekee yanayomhusu Mtume pekee yake. Mfano mwingine ni sheria inayohusu kugawa vitu alivyoviacha. Hili pia linamhusu yeye na wengine hawatakiwi kuiga.

Alisema, "Sisi ni mitume, hatuachi urithi wa mali"[46] na alikigawa kila alichomiliki. Hii haikuwa na maana kuwa ni sheria kila mtu afuate.

---

44. Qantar ni aina nyingine ya kipimo. Kama tukichukulia qirat kuwa ni sawa na garamu, tunaweza kusema qantar ni sawa na kilogramu.
45. Bukhârî, Buyû 100; Muslim, Zakât 31; Abû Dâwûd, Witr 23; Dârimî, Riqâq 53; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 467.
46. Bukhârî, Khumus 1; Muslim, Jihâd 54; Abû Dâwûd, Imârah 19; Tirmidhî, Siyar 44; Nasâî, Fay' 9; Muwatta, Kalâm 27; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, 1, 4.

Vivyo hivyo, inajulikana kuwa Mtume (s.a.w) alisema, "tunu ya makafiri katika hii dunia ni umasikini."[47] Alijivunia umasikini wake. Sifa hii pia ilimhusu yeye peke yake. Isifikiriwe kuwa Mtume alihamasisha umasikini. Kinyume chake alisema pia "Mkono utoao ni bora kuliko mkono upokeao."[48] Kwa msingi huu, tunaweza kusema kuwa alikuwa anawahamasisha watu kuchuma mali kwa njia halali ili waweze kuwa watoaji.

Hivyo, taratibu zinazohusu umaskini hazihamasishi umaskini, bali zinamhamasisha mtu kuuridhia Mpango wa Mwenyezi Mungu, na pia zinatufundisha kumtegemea na kujisalimisha mbele ya utashi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

3. Kuishi kwa kufuata msingi wa *zuhd* (kuipa kinyongo dunia) na *taqwa* (kujiepusha na mambo yanayotia shaka) ni sifa kubwa inayomfanya mja awe karibu na Mwenyezi Mungu. Lakini si kila mtu analazimishwa kufuata maisha kama hayo; hii inategemea uwezo na kipawa cha mtu. Wakati mifumo yote ya kijamii inapohamasisha ukuaji wa kitamaduni kwa uwazi na uthabiti, hakuna mgogoro wa lazima kati ya unyumbukaji wa kiutamaduni na utimilifu wa kiroho na kimaanawi. Hivyo, japokuwa *zuhd* na *taqwa* zinapinga raha za ulimwengu huu, kuzifuata kwa ngazi ya jamii hakutakiwi kusababisha uharibifu katika mabadiliko ya kijamii, ambapo jamii zenye nguvu ya kiroho zitatawaliwa na maadui zao wa kidunia. Kanuni ya jumla inasema kuwa yatupasa kuyapima maendeleo kwa msingi wa mabadiliko ya kila siku, kama ili-

47 al-Daylamî, al-Firdaws, II, 70.

48. Bukhârî, Vasâyâ 9; Muslim, Zakât 94; Abû Dâwûd, Zakdt 28; Tirmidhî, Zuhd 32; Nasâî, Zakât 50; Muwatta, Sadakah 8; Dârimî, Zakât 22; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 67.

vyoelezewa katika hadith isemayo "si miongoni mwetu Yule ambaye siku zake mbili zimebaki kuwa sawa."[49] Hapa tunaona uthibitisho kuwa kanuni hii haipingani na misingi ya *zuhd* na *taqwa*, ambayo msingi wake ni kutopendelea starehe na furaha ulimwengu huu. Hii ni kwa sababu kutopendelea maisha ya dunia hakuwi katika ngazi ya nje, bali huwa katika ngazi ya kiroho na kiakili. Kama anavyosema Jalaladdin Rumi, (Mwenyezi Mungu aitakase roho yake):

"Maana ya dunia ni kule kutotambua uwepo wa Mwenyezi Mungu! Sio kuhusu pesa, wanawake, au mavazi. Lielewe hili vizuri."[50]

Kutokana na mtazamo huu, kumiliki mali na kuwa tajiri hakupingani na *zuhd* na *taqwa* madamu mhusika hatakuwa mkwasi na kuziweka mali moyoni mwake. Kwa upande mwingine, utajiri na pesa kidogo vinaweza kugeuka kuwa masanamu kama zikipendwa sana kiasi cha kuweka makazi moyoni. Katika mitume, maisha ya Nabii Suleiman (a.s) na yale ya maswahaba, Abu Bakr, Uthman, Talha na Abd ar-Rahman ibn Awf, Mwenyezi Mungu awawie radhi wote, ni mifano mzuri wa mizania hii.

Mara chache, mwonekano wa nje wa *taqwa* na *zuhd* unaweza kutokana na mahitaji ya kimaada kuliko kutoipenda sana dunia. Katika hali kama hiyo, *taqwa* itaukubali umasikini kwa furaha kwa kile kilichokadiriwa na Mwenyezi Mungu. Lakini, kama badala ya kuukubali kwa njia hiyo, mtu akakataa uwepo wake halisi, hiyo haitakuwa tafsiri sahihi ya *taqwa*. Kwa mfano, ijapokuwa wakati mwingine Mtume

49. al-Bayhaqî, Kitaâb al-Zuhd al-kabîr, II, 367; al-Daylamî, al-Fırdaws, III 611; Abû Nu'aym al-Isbahânî, Hilyah al-Awliyâ, VIII, 35.
50. Can, Şefik, Mesnevi Teremesi, (Istanbul, 1997), v.11, uk. 55.

alifunga jiwe tumboni ili kuondoa njaa, mfano huu unaonesha kuwa njia bora ya kushukuru ni kushirikiana na wengine kwa hiari na uhuru. Hii ndiyo njia bora ya uchamungu na kujizuia (zuhd). Kuficha mali na kufanya ubakhili kwa hoja ya kufanya taqwa ni aina ya ulaghai na hivyo haiwezi kuwa taqwa ya kweli.

Kwa mtazamo huu, tunaweza kuona kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) mtu mnyoofu na mwenye taqwa zaidi kuliko watu wote. Alikuwa akiishi kama maskini kwa sababu ya taqwa yake.

Bibi Aishah (r.a) anasema:

"Mtume Muhammad alikufa bila kula mkate wa shayiri kwa siku mbili mfululizo."[51]

Anas (r.a) anasimulia kuwa:

"Muda mwingine Mtume (s.a.w) alikubali mialiko ya chakula cha mkate wa shayiri na mafuta uliokaribia kuharibika. Kutokana na unyenyekevu wake, alihudhuria kwenye mikusanyiko hiyo bila wasiwasi wowote. Adiha, aliweka rehani ngao kwa Myahudi. Lakini kwasababu ya utoaji wake wa sadaka na misaada hakuweza kuikomboa."[52]

Hata hivyo, Mtume (s.a.w) alikataza kujinyima vyakula na vinywaji halali kwa hoja ya uchamungu. Alikuwa akila na kunywa vilivyokuwa halali. Lakini wakati huo huo, hakuwa akilijaza tumbolake licha ya chakula hicho kuwa halali. Alimwambia bwana mmoja aliyeenda mbweu mbele yake: "acha

51. Bukhârî, Aymân, TL; Muslim, Zuhd 20-25; Nasâî, Dahâyâ 37; Ibn Mâjah, At'imah, 48; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 98.
52. Bukhârî, Jihâd 89; Tirmidhî, Buyû 7; Nasâî,Buyû 58; Ibn Mâjah, Ruhûn 1; Dârimî, Buyû 44; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 236.

kwenda mbweu! Wale ambao wanajaza matumbo yao kupita kiasi katika ulimwengu huu ndio wale watakaohangaika njaa kwa muda mrefu."[53]

Hadith nyingine inaeleza kuwa:

"hamna aliyelijaza chombo hatari kuliko tumbo lake. Hakika, vitafunio vichache tu vinamtosha mtu kuwa imara. Kama atakula zaidi, anatakiwa abakishe theluthi kwa ajili ya chakula, theluthi kwa ajili ya vinywaji na theluthi kwa ajili ya kupumulia."[54]

Hii ni njia kati na kati katika kula na kunywa. Huu ni mfumo wa hatua za aina yake unaolenga kudhibiti ulafi wa binadamu. Kwa mtazamo huu, shule ya Mtukufu Mtume (s.a.w) iliwafundisha masikini na matajiri, wakiwemo watawala wenye vyeo tofauti katika jamii, kwa njia nzuri, wawe na hali ya kutosheka, na nyoyo zao zilipata furaha kiasi kwamba walimheshimu. Katika shule hii ya Mtume, kulikuwa na matajiri wengi walioishi kwa unyenyekevu kana kwamba walikuwa masikini, na masikini wengi waliomshukuru Mwenyezi Mungu kama vile walikuwa matajiri. Matajiri na watawala wengi waliokuwa na kazi ya kukusanya sadaka walipata mafunzo katika shule hiyo.

Katika historia ya Uislamu, Visa vya makhalifa waliobeba chakula mgongoni mwao kuwapelekea masikini, na kuwapikia vyakula ni visa vinavyojulikana sana.[55] Kushtaki-

53. Tirmidhî, Sifatu'l-qiyâmah 37; Ibn Mâjah, At'imah 50; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, IV, 249; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, V, 27.
54. Tirmidhî, Zuhd 47; Ibn Mâjah, At'imah 50; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 132; al-Hâkim, al Mustadrak, IV, 135; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 449.
55. Suyûtî, Tarikh al-khulefû, p. 91-92.

wa kwa Fatih Sultan Mehmed kulikotokana na malalamiko ya mhandisi mmoja wa Kigiriki na yeye kuheshimu maamuzi ya mahakama yaliyompa haki *dhimmi* (raia wasiokuwa Waislamu anayeishi katika dola ya Kiislamu) ni mfano mmoja tu katika ishara za Baraka na huruma kwa watu iliyotokana na shule ya taqwa ya Mtume (s.a.w).

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.aw.) ameeleza *zuhd* katika namna nzuri kabisa:

"*Zuhd* katika ulimwengu huu sio kuifanya halali kuwa haramu, wala sio kujitenge na mali. Bali *zuhd* katika ulimwengu huu ni kutegemea kilicho mikononi mwa Mwenyezi Mungu kuliko kutegemea kile kilicho mikononi mwako na nitafanya subira wakati wa dhiki na kutarajia thawabu zake."[56]

Mtukufu Mtume (s.a.w) ni mfano bora kwa wanadamu wote katika *zuhd* na kuridhika kwake. *Zuhd* ndiyo inayoupa moyo na mwili wa mtu maisha ya kuvutia na furaha kwa kuyadhibiti matamanio kayaya ya kupenda starehe za dunia, kwa kutodanganyika na raha za muda mfupi za ulimwengu huu, kwa kutopenda vitu vingine zaidi ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kuacha yale yote yanayomtoa kwenye ibada na yasiyokuwa na manufaa na faida yoyote katika maisha ya Akhera. Kinyume chake, kuupenda ulimwengu huu ni janga lililojaa maumivu na wasiwasi ambao huzimaliza nguvu ya moyo na mwili. Mtume Muhammad (s.a.w) anasema:

"Kutoipenda dunia (*Zuhd*) huupa moyo na mwili utulivu na faraja . Kuipenda dunia kunaongeza huzuni na maumivu.. ."[57]

---

56. Tirmidhî, Zuhd 29; Ibn Mâjah, Zuhd 1 ; al-Tabarânî, al-Mu'iam al-Awsat, III, 57; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, VII, 218.
57. Ahmad ibn Hanbal, Kitâb al-Auhd, p. 47; al-Qudâî, Musnad al-

Hadith nyingine inatoa ushauri ufuatao: "Onesha kutokuipenda hii dunia na Mwenyezi Mungu atakupenda; onesha kutokuvipenda vya watu na watu watakupenda!.. ."[58]

Zuhd ni njia ya kwanza inayoshauriwa kufuatwa dhidi ya majanga ya ulimwengu huu. Hadith moja inasema:

"Hakuna ubor wa weupe juu ya weusi. Hakuna rangi iliyobora kuliko nyingine. Ubora hupatikana kwa *taqwa* tu."[59]

Vilevile akasema:

"Ufunuo haukunilazimisha kulimbikiza mali wala kuwa mfanyabiashara. Uliletwa kwangu 'ili kueneza Utukufu wa Mola wenu, kuwa kati ya wanaonyenyekea kwa Mwenyezi Mungu na kumtumikia pia. '"[60]

Hadith nyingine inatoa wosia ufuatao:

"Unaposimama kwa ajili ya kuswali, Swali kama vile unaswali swala yako ya mwisho. Usiseme lolote utakalojutia kesho. Usitamani vile watu wanavyotamani kwa mghafala."[61]

Siku moja aliulizwa:

"Ni yupi mwanadamu aliye mkamilifu?"

Shihâb, I, 188; al-Bayhaqî, Shu'ab alÎmân, VII, 268 [Imesimuliwa pia na Omar kama hadith mawkuf]

58. Ibn Mâjah, Zuhd 1; al-Hâkim, al-Mustadrak, IV, 348 ; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr,Vl, 193; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, VII, 344
59. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 158; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, IV, 289.
60. Ibn Abî 'Âsim, Kitâb al-Zuhd, I, 391; al-Daylamî, al-Firdaws, IV, 95; Abû Nu'aym al-Isbahânî, Hilyah al-Awliyâ, II, 131; Ibn 'Adiyy, al-Kâmil fî aldu'afâ, III, 68.
61. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 412; Ibn Mâjah, Zuhd 15; al-Tabarânî,al-Mu'jam al-Kabîr, IV, 154.

Akajibu:

"Watu wasafi ni wale wanaojitakasa dhidi ya dhambi, shaka, ulaghai, kusema urongo na uhasidi."[62]

Mtume Muhammad alikuwa makini sana kuhusu kilicho halali na haramu. Alijiepusha pia na vile vya kutia mashaka. Mjukuu wake wa kiume, Hasan, aliyekuwa na umri mdogo, alikuwa amekaa msikitini akitazama jinsi tende za zakat zilivyokuwa zinagaiwa. Ghafla akaweka tende moja mdomoni mwake. Mtukufu Mtume (s.a.w) akamuonya:

"Tema! Tema! Tema hiyo tende! Haujui kuwa hatuli sadaka?" Alimfanya mjukuu wake ateme ile tende.[63]

Mawlana Jalaluddin Rumi, (Mwenyezi Mungu aitakase roho yake), anasema kuhusu chakula cha halali:

"Chakula ni kama mbegu. Matunda yake ni fikra/mawazo na makusudio."

"Chakula kinachokupa matamanio na hamasa kubwa, na hamu ya kufanya ibada na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu ni halali; na chakula kinachokupa uvivu wa kufanya ibada na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu na kuupa ugumu moyo wako ni haramu ."

"Ongeza idadi ya vyakula vya halali katika maisha yako! Jiepushe na vyakula vya Haramu na vyenye kutia shaka ili uweze kupata ladha ya kumuabudu, kumtii Mwenyezi

62. Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 76; Ibn Abî Shaybah, al-Musannaf, VI, 167; Ma'mar ibn Râshid, al-Jâmi', XI, 191.
63. Bukharî, Zakât 60; Muslim, Zakât 161; Nasâî, Tahârah 105; Muwatta, Sadakah 13; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 200.

Mungu na kufikia kwenye hali ya ukinaifu na umakini wa moyo."[64]

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika Qur'an: *"Hakika wamefanikiwa waumini ambao ni wanyenye kevu katika ibada zao."* (Qur'an, Mu'minun, 23:1-2)

❀

Mtazamo ulioenea katika jamii yetu ni kuwa dini ni imani ambayo lengo lake pekee ni kumpa mtu furaha huko Akhera. Lakini, dini sio taasisi yenye lengo la kumpa mtu furaha ya akhera tu; dini ina lengo pia la kutengeneza mazingira ya tulivu na usalama kwa wanadamu kwa kuweka utaratibu maalumu katika maisha ya kijamii.

Usiku mmoja, Umar (r.a)i, kama kawaida, alikuwa akitembea mitaa ya Madina. Ghafla, akasimama aliposikia mazungumzo ya bila kutarajia kati ya mama na binti yake. Mazungumzo hayo yalimvutia sana. Mama alikuwa anamwambia binti yake:

"Ongeza maji kwenye maziwa ya kuuza kesho."

Binti yake akamwambia:

"Mama! Hujasikia kuwa Khalifa amekataza kuzimua maziwa?"

Mama yake akashikwa na hasira na kupaza sauti:

"Mwanangu! Unafikiri Khalifa atajuaje kama tumezimua haya maziwa usiku wote huu?"

Yule binti, ambaye moyo wake ulikuwa na uhai wa

64. Rûmî, Jalâladdin, Mathnawî Ma'nawî, (Tehran, 1378) v.I, 1645-48; Can, §efik, Mesnevi Tercemesi, (Istanbul, 1997), v.II, uk.120.

kumuogopa Mwenyezi Mungu hakuridhishwa na udanganyifu wa mama yake. Aliendelea kukataa:

"Mama! Acha tukubali kuwa Khalifa haoni, je vipi kuhusu Mwenyezi Mungu? Unafikiri kuwa naye haoni? Ni rahisi kuwadanganya watu lakini ni vigumu kumdanganya Mwenyezi Mungu ambaye anaona na kusikia kila kitu."

Mwenyezi Mungu amuwie radhi binti huyo. Amir al-Mu'minin, kiongozi wa waumini, alitambua kuwa ingawa alikuwa binti wa kawaida, alikuwa na utambuzi wa kipekee juu ya Mwenyezi Mungu. Alitaka awe mkwe wake na amuozeshe kwa mwanawe wa kiume. Ni kutokana na silsila hii safi alizaliwa Umar ibn Abdulaziz, anachukuliwa kuwa khalifa wa tano katika makhalifa waongofu.

Tukio hili linaonesha kuwa kuheshimu mipaka ya halali kunatosha kuleta furaha na kumuinua mwandamu kwenye daraja ya ukamilifu. Kinyume chake, kutotosheka na halali, kutochunga mipaka na kujiingiza kwenye haramu au mambo yenye kutia shaka ni jambo lisiloendana na mja mwenye utiifu. Mtume Muhammad (s.a.w) anasema kuhusiana na vitu vyenye kutia shaka, ambavyo haijulikani wazi kama ni haramu au la:

"Acha kile ulicho na shaka nacho na uchukue kile usichokuwa na mashaka nacho."[65]

Hata hivyo, haitakuwa sahihi kuitafsiri vibaya kanuni hii kwa kuvuka mipaka na kufikia hatua ya kuyaacha hata yale ya halali au kwa kuleta utata kuhusu mambo ya halali.

Uislamu unataka uwastani na njia ya kati na kati katika

65. Bukharî, Buyû 3; Tirmidhî, Qiyâmah 60; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 153.

suala hili, kama ilivyo kwa masuala mengine. Lengo la Uislamu sio kumuwekea mipaka mwanadamu; bali lengo la Uislamu ni kumfanya mwanadamu aishi maisha ya utulivu, furaha na yenye uthabiti. Siri ya jambo hili hufikiwa kwa kuimarisha amani ya moyo itokanayo na chemichemi zote za uzuri. Hili linawezekana kwa kusikia, kuhisi na kuzifanyia kazi tabia na sifa safi za moyo wa Mtukufu Mtume (s.a.w) .

❀

Mtume Muhammad (s.a.w) hakuwa na dhambi. Lakini aliendelea kuswali usiku hadi miguu yake ikavimba na aliendelea kusoma Qur'an hadi alipochoka. Alimpenda, alimshukuru, alimwogopa, na kumkumbuka Mwenyezi Mungu kuliko mwingine yeyote.

Swala ni makutano kati ya mja na Mola wake. Ni chanzo cha furaha isiyo na kikomo kwa wanaompenda Mwenyezi Mungu Mtukufu. Waja huswali swala za sunna kwa lengo la kuendelea kupata ladha ya ibada.

Ndani ya swala kuna kujisalimisha. Hii ndiyo sababu kwanza nafsi haipendi kuswali. Sifa hii tu inatosha kuonesha kuwa Uislamu ni dini ya kweli na kwamba swala ni aina ya hali ya juu kabisa ya ibada.

Wale wote wanaoendeshwa na nafsi zao huwa hawaikurubii swala, ilhali wale wasioweza kukivuka kizuizi cha nafsi zao hushikamana na swala. Swala ya kweli ni baraka waliyopewa watu wachache tu.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu analithibitisha hili kama ifuatavyo:

"Watu wawili wanaweza kuswali eneo moja, lakini tofauti iliyopo kati yao ni sawa na tofauti iliyopo kati ya ardhi na mbingu."[66]

Swaumu na funga ya Mtukufu Mtume (s.a.w), Nuru ya Ulimwengu, nayo pia ni mfano bora kwa umma wake.

Mtume Muhammad mara nyingi alianza kufunga kabla hajala chochote. Muda mwingine alifunga mfululizo bila kula jioni. Maswahaba wake walipotaka kufanya kama yeye aaliwaambia:

"Hamna uwezo wa kufanya kama mimi."[67]

Ibn Abbas (r.a) anasimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akikaa masiku kadhaa mfululizo bila kula, na familia yake pia haikupata kitu cha kula. Hata walipokula, chakula chao kilikuwa mkate wa shayiri tu.[68]

Anas ibn Malik (r.a) anasimulia kuwa siku moja Bibi Fatimah alimletea Mtume (s.a.w) mkate aliomuandalia. Akauliza:

"Nini hiki?"

Fatimah akajibu:

"Mkate mzuri niliopika, sikuweza kula bila kukugawia."

Fahari ya ulimwengu akajibu:

"Huu ni mlo wa kwanza ambao baba yako atakula tangu siku tatu zilizopita."

---

66. Abu Sa'îd al-Shâshî (d. 335), Musnad al-Shashî, I, 86.
67. Bukhârî, Sawm 20; Muslim, Siyâm 55; Muwatta, Siyâm 37; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 128.
68. Ibn Sa'd, al-Tabaqât al-Kubra, I, 400.

Kwa mujibu wa Abu Hurayra, wakati mwingine mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa akifunga jiwe tumboni ili kupunguza ukali wa njaa.[69]

Thamani kubwa ya funga hutokana na lengo lake, ambalo ni kuapambana na *"nafs"* na kuidhibiti kwa hisia endelevu ya ibada.

Hijjah, kwa upande mwingine ina lengo la kutoa mafunzo katika *tawakkul*, kumtegemea Mwenyezi Mungu wa Ibrahim na Ismail (Rehma na amani ziwafikie), kumpiga mawe adui wa ndani aitwaye "nafs", na adui wa nje aitwaye *"shaytan"*; kuacha tofauti zote za kitabaka kwa kuvaa vazi moja linalofanana na sanda na kutafuta kimbilie kwa Muumba; kujawa na khofu kwa kuliona tukio linalofanana na tukio la Siku ya Kufufuliwa, kuzileta pamoja jamii za Waislamu kutoka mbali; na kuimarisha undugu wa imani.

Mfano bora wenye kuvutia ni Hijja na Hotuba Mwisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa ajili ya Hijjah ambazo ummah wake utazifanya hadi siku ya mwisho!

Kwenye hotuba yake ya mwisho, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitengeneza "mgawanyo wa upendo". Njia muhimu ya haki kati ya Waislamu ilionyeshwa na" muunganiko wa upendo".

Taratibu za Hijjah huyageuza macho ya mtu kuyatazama maisha ya kimaanawi na kiroho; ibada hii adhimu imejaa ishara na maajabu ya upendo, ambayo

Umar (r.a) aliacha kulibusu jiwe jeusi, al-Hajar al-Aswad kwa hofu ya kuwabughudhi Waislamu wengine.

Vitendo na mawazo haya wakati wa Hijjah kunamleta

69. Ibn Sa'd, al-Tabaqât al-Kubra, I, 400.

mtu kwenye hali ya ana kwa ana ya kujiuliza na kuakisiwa katika maisha ya baadaye ya watu husika. Lengo pekee la amali hizi ni kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Maeneo Matakatifu ambayo Hijjah hufanyika ni mabustani ya kiroho ya ulimwengu Mtukufu .

Arafat ni mahala pa msamaha na kimbilio.

Muzdalifa ni mahala ambapo rehma hupata kuonekana, mahala palipotajwa kwenye Qur'an kama *al-Mash'ar al-Haram*.[70]

Mina ni mahala pa kujinyenyekeza na kumtegemea Mwenyezi Mungu ambapo Ibrahim, Ismail, na mama yetu Hajar walimshinda *Shaytan*.

Ka'bah ni mahala tunapozielekeza nyuso zetu wakati wa swala kwa amri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Qur'an: *"Nawe sujudu na ujongee."* (Qur'an, Alaq, 96:19) Wakati huo huo, ni sehemu ambayo Waislamu wote ulimwenguni huelekeza nyuso zao wakati wa kuswali. Ni sehemu yanapopatikana mapigo ya moyo wa ulimwengu wa Kiislamu.

Mji wa Mtume (s.a.w), sehemu tunayoitembelea baada ya Makkah, ni sehemu ambayo moyo hufikiwa daraja za juu baada ya kupambwa na ishara za upendo. Mtukufu Mtume (s.a.w) ndiye mtu pekee ambaye Mwenyezi Mungu alimuita "kipenzi changu".

Kwa mujibu wa Imam Malik, eneo lenye kaburi la Mtume ndiyo tukufu zaidi ulimwenguni baada ya Ka'bah. Hii ni kutoka na kuwa ndiye aliyekuwa muongozo kwa wa wanadamu wote.

70. Qur'an, Baqara, 2:198.

Ardhi hii Tukufu imekuwa ikipewa chakula cha kiroho na watu wenye imani tangu enzi za Adamu na kumwagiliwa kwa machozi yao. Maeneo haya, ambayo yamekuwa kama chemichemi za wahyi wa mitume, yamejaa kumbukumbu muhimu katika historia ya mitume.

Kwa mukhtasari, amali ya Hijja ni ibada muhimu, ambayo, kama matendo mengine ya wajibu, humuongoza mja kwenye ukamilifu wa kidini.

Hijjah ni ibada inayoiwezesha roho ya mja kupata utulivu, mazingira ya kiasili, rangi na utambulisho. Ni iabda iliyojaa ishara za kimaanawi ambapo moyo hutakaswa na kusafishwa kwa mvua ya Baraka za kiroho na hatimaye kuufikia ukweli wake.

❀

Zaka ni kodi ya kidini iliyofaradhishwa juu ya wale wenye kipato cha kutosha ili kuwapa masikini.

Hii ni muhimu ili kufanya mali nyingine zilizobaki ziwe halali kwa mmiliki. Mali hupata kuhamishwa kidogo kidogo kwenda kwa maskini. Ugawaji huu wa utajiri unasaidia kuleta usawa, uadilifu na uelewano katika jamii.

Kinazingatiwa katika Zaka sio pato la mwaka, bali ni mali ya ziada aliyo nayo mtu husika. Kwa hiyo, pesa au bidhaa isiyotumika katika uwekezaji hutolewa. Kwa njia hii Uislamu unatoa msukumo kwa jamii kukusanya mali yote kutoka katika vitu na fedha.

Hekima iliyopo kwenye *zaka* na sadaka ni kutoa suluhisho halisi la ukuaji usiokuwa na kikomo wa mali kulundikana kwa mtu mmoja ambao unaweza kugeuka kuwa donda ndugu. *Zakat* ni mfumo ambao husaidia kukuza uhusiano

na upendo wa dhati kati ya watoaji zaka na wapokeaji. Kwa maneno mengine, *zaka* ni haki ya masikini ya kutoka kwa matajiri, ni jambo linaloimarisha upendo baina ya pande mbili. Hili limeelezewa katika Qur'an, kama ifuatavyo:

"Na katika mali ipo haki ya mwenye kuomba na asiyeomba." (Qur'an, Zariyat, 51:19)

Adab (adabu za kiislamu) ni jambo muhimu sana. Mtoaji anatakiwa amshukuru yule anayepokea kwasababu masikini wanawafanya matajiri waweze kutekeleza ibada ya wajibu na kupata thawabu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Sadaka inayotelewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ni hifadhi na kinga dhidi ya maradhi na matatizo mengine.

Qur'an inaelezea umuhimu wa kutoa *zaka* na sadaka kwa kuseama kuwa, *"Mwenyezi Mungu anazikubali sadaka…..."* (Tawba: 104) Vivyo hivyo, hadith imeeleza, "Sadaka humfikia kwanza Mwenyezi Mungu kabla ya kufika mikononi mwa masikini."[71]

Wakati wa kutoa sadaka ni muhimu kuepuka kiburi, majivuno, dharau na kujionesha. Vinginevyo, kinachotolewa hakitapokelewa na Mwenyezi Mungu, badala yake kitapotelea mikononi wa wanadamu na hakuna kitakachofika Akhera. Mtume Muhammad (s.a.w) alitoa mfano mzuri wa maisha ya kujizuia na raha za dunia na katika kutoa sadaka.

Mama yetu Aishah (r.a) anasema:

"Kamwe vyakula viwili havikuingia katika tumbo la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wakati mmoja ndani ya siku moja. Alipokula nyama, hakula kitu kingine tena.

71. al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, IX, 109; al-Harawî, al-Arba'în fî dalâil al-Tawhîd, I, 74; al-Daylamî, al-Firdaws, II, 2.

Vivyo hivyo, alipokula tende au mkate, hakuongeza kitu kingine."[72]

Abu Nadr anasimulia yafuatayo:

"Nilisikia kuwa mama yetu Aishah alisema:

'Siku moja tulikuwa tumekaa na mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Baba yangu, Abu Bakr, akatuletea mguu wa kondoo. Ndani ya giza lile la usiku, tulijaribu kukata nyama. Mmoja akasema: 'hakuna mshumaa au taa?' Nikasema: 'kama tungekuwa na mafuta, tungekula nyama.'[73]

Mtume Muhammad (s.a.w) alipenda sana kutoa sadaka. Siku moja alimwambia Bilal:

"Ewe Bilal! Toa sadaka! Usiogope kuwa mmilki wa kiti cha Enzi ataipunguza mali yako kwa sababu ya kutoa sadaka."[74]

Kwa hiyo, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa hapendi kujilimbikizia mali. Hii ni kutokana na kuwa alitaka kuishi kama "mtume mtumishi", kama ilivyoelezewa katika hadith ifuatayo:

"Niliambiwa nichague kuwa kati ya mtume mja au mfalme. Malaika Jibril alinidokeza kuwa niwe mnyenyekevu. Kwa hiyo, nikachagua kuwa mtume mja na kuomba kuwa "nishibe siku moja na siku moja niwe na njaa."[75]

Mtume Muhammad (s.a.w) alikataa kuingia nyumbani kwa binti yake Fatimah (r.a) kwa sababu aliipamba nyumba yake, na akamwambia:

---

72. Ibn Sa'd, al-Tabaqât al-Kubrâ, I, 405.
73. Ibn Sa'd, al-Tabaqât al-Kubrâ, I, 405.
74. Ma'mar ibn Râshid, al-Jâmi', XI, 108; al-Bazzâr, al-Musnad, IV, 204; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, III, 86; al-Bayhaqî, Shabul-Îmân, II, 118.
75. İbn Hibban, al-Sahîh, XVI, 280; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ,VII, 48, 49.

"Si sahihi kwetu kuingia katika sehemu zilizopambwa."[76]

Mtume Muhammad (s.a.w) hakujivuna kwa sababu ya maisha ya kumcha Mwenyezi Mungu aliyokuwa akiishi. Alikuwa akihesabu baraka za Mwenyezi Mungu juu yake huku akionesha unyenyekevu wa hali ya juu kwa kusema "*la fakhr*"[77], (sijifakharishi).

Unyenyekevu wa Mtume wa Rehma

Mara nyingi kusifiwa na kupongezwa sana na watu humfanya mtu kuwa kiburi. Vitu hivi viwili huwaaribu watu wengi. Ijapokuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa mwanadamu bora kuliko watu wote na kusifiwa sana na Mwenyezi Mungu, aliwaomba maswahaba zake yafuatayo:

"Niiteni 'mja na mjumbe wa Mwenyezi Mungu'."[78]

Abu Usamah (r.a) anasimulia kuwa:

'Hotuba ya Mtume (s.a.w) ilitoka katika Qur'an. Aliendelea kufanya *dhikr* na kuifupisha hotuba huku kuirefusha swala yake. Hakuona aibu kutembea na masikini, kinyume chake alifurahia kufanya hivyo."[79]

Anas (r.a) anasimulia kuwa:

"Mtume (s.a.w) alifanya *dhikr* mara kwa mara. Alifanya

76 Abû Dâwûd, At'imah 8; Ibn Mâjah, At'imah 56; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 220-222.

77 Tirmidhî, Manâqib 1; Ibn Mâjah, Zuhd 37; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, 1, 5, 281.

78 Bukhârî, Anbiyâ 48; Dârimî, Riqâq 68; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 23.

79 Nasâî, Jum'a 31; Dârimî, Muqaddimah 13; Ibn Hibban, al-Sahîh, XIV,333; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 671.

utani mara chache sana. Alipanda punda, alivaa nguo zilizotengenezwa kwa sufu ngumu, alikubali mwaliko wa watumwa, aliwatembelea wagonjwa na alihudhuria mazikoni. Siku ngome ya Khaibar ilipotekwa, alikuwa amepanda punda akiwa na kamba iliyotengenezwa kwaa majani ya mtende. Kadiri Mwenyezi Mungu alivyokuwa akimpa ushindi ndivyo alivyozidi kuwa mnyenyekevu na mwenye shukurani."[80]

Jarir (r.a) anasimulia kuwa:

"Bwana mmoja alikuja mbele ya Mtume (s.a.w) siku Makkah ilipokombolewa. Bwana yule akaanza kutetemeka baada ya kuona haiba ya kiroho na kimwili ya Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) alipomuona vile, alimwambia yule bwana kwa sauti ya upole:

"Tulia, usiwe na wasiwasi! Mimi si mfalme. Mimi ni mtoto wa mwanamke wa kabila la Quraysh ambaye alikuwa akila nyama iliyokaushwa."[81]

Amir ibn Rabi'a (r.a) anasimulia:

"Siku moja, nilikuwa nikienda msikitini pamoja na Mtume. Kamba ya kiatu chake ilikatika njiani. Nikataka niitengeneze. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikataa kunipa ile kamba na kisha akasema:

'Huu ni upendeleo (unaomfanya mtu awe juu ya wengine), sipendi upendeleo huu'."[82]

---

80. Tirmidhî, Janâiz 32; Ibn Mâjah, Zuhd 16; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 506.
81. Ibn Mâjah, At'imah 30; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 506; al-Tabarânî, al-Mujamu l-Awsat, II, 64.
82. al-Bazzâr, al-Musnad, IX, 263; Abû Dâwûd al-Tayâlisî, al-Musnad, I,156; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, III. 174; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, III, 275.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu(s.a.w) aliwapa muongo wanadamu wote ili waweze kupata furaha ya milele.

Hii ilikuwa kama zawadi kutoka kwake kwa sababu hakuhitaji malipo yoyote kwa huduma hiyo kubwa aliyoitoa kwa ajili ya watu.

❀

Lengo hasa la dini ni kutengeneza watu safi wenye utambuzi na hisia ya ndani kabisa. Hili hutokea kwa kutengeneza utambuzi wa kumuabudu Mwenyezi Mungu. Ukomavu huu hufikiwa kwa msisimko unaotokea ndani ya moyo kama ilivyoelezwa katika aya ifuatayo:

"Hakika Waumini ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposomewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao mlezi." (Qur'an, Anfal, 8:2)

Neno la Kiarabu linalotumika kumaanisha mwanadamu ni *"insan"* lenye uhusiano na neno*"nisyan"* (usahaulifu) na *"uns"* (urafiki). Kinyume cha*"nisyan"* ni *"dhikr"* (kukumbuka), lililorudiwa zaidi ya mara 250 katika Qur'an Tukufu. Pindi mbegu ya dhikr inapopandikizwa katikati ya moyo, moyo huo huanza kumtambua na kumuabudu Mwenyezi Mungu. Siku zote wapendaji hawawasahau wale wanaowapenda.

Daima huwaweka katika nyoyoni na ndimi zao. Nyoyo zinazotamani kufurahia maisha na uhai wa imani hudumisha *dhikr* isiyokuwa na kikomo. Huzama katika tafakuri kuhusu uumbwaji wa ardhi na dunia wakiwa wanatembea, wakiwa wamekaa au wakiwa wamelala, kama inavyoelezewa katika aya ifuatayo katika Qur'ani:

"Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwambingu na ardhi, wakisema Mola wetu mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka,

Umetakasika!Basi tukinge na adhabu za moto'." (Qur'an, Aali Imran, 3:191)

Moyo usiokuwa na utambuzi na utakaso huo hauwezi kuwa na shauku na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ilivyoelezewa katika aya ifuatayo:

"Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu!" (Qur'an, Zumar, 39:22) Aya hii inaonesha kuwa wale wote wanaojiweka mbali na *dhikr* hupoteza heshima na hadhi ya kuwa wanadamu.

Wanadamu wamebeba sifa ya kuwa wenye kufanya ibada. Kwa hiyo, wanaweza kuabudu vitu au wakamuabudu Mola wao. Kumuabudu Mwenyezi Mungu kunawalinda wanadamu dhidi ya kuwa watumwa wa vitu au matamanio binafsi.

Mwenyezi Mungu, Mtukufu ametuasa kuhusu hili katika aya ifuatayo:

"Je umemuona aliyefanya matamanio yake kuwa ndiye Mungu wake?" (Qur'an, Jathiya, 45:23)

Kuweka matamanio na mipango ya muda mrefu ndani ya akili ili kuyafanikisha baadaye, mipango inayoangalia ulimwengu huu pekee na kuusahau ulimwengu ujao, humpeleka mwanadamu kwenye mwisho wenye uchungu. Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema:

"Tahadhari! Msifanye matamanio yenu na mipango yenu ya baadaye ikaongezeka kiasi kwamba ikawafanya msahau kifo! Vinginevyo nyoyo zenu zitakuwa ngumu. Fungueni macho yenu! Kinachosubiriwa kiko karibu sana!"[83]

83. Ibn Mâjah, Muqaddimah 7; Ma'mar ibn Râshid, al-Jâmi', XI, 116; al-

Salman al-Farisi aliyenufaika sana kutokana na ushauri wa Mtume (s.a.w) anasema: "Vitu vitatu hunifanya nicheke na vitu vitatu hunifanya nilie." Anaelezea kuwa miongoni mwa vitu vilivyokuwa vikimshangaza na kumchekesha ni mtu aliyekuwa anajiwekea mtarajio ya muda mrefu haliyakuwa kifo kinamsubiri.

Vile vile Mtukufu Mtume (s.a.w), anasema: "Japokuwa nguvu za mtu mzee hudhoofika, lakini tamaa na matamanio yake kuhusu matarajio ya baadaye *(tul al-amal)* huendelea kuimarika."[84] Hadith hii inaonesha kuwa tamaa na matamanio ya maisha yajayo ni vikwazo viwili ambavyo hakuna moyo wa mwanadamu unaoweza kuviepuka. Hata mwili ukizeeka na kuwa dhaifu wanadamu wanatamani kuwa wadogo, kwa sababu roho zao zina sifa ya kutokufa. Hivyo, daima wanadamu hutaka kuendelea kuwa wadogo na wanajutia kupoteza ujana wao pindi wanapozeeka. Matokeo yake wanakuwa watumwa wa tamaa isiyokuwa na mwisho.

Kama ambavyo udongo mkavu hufyonza maji ya mvua yanayoudondokea, nafsi ya mwanadamu hutamani kuzifyonza raha zote za dunia. Lakini wanadamu hawarudishi fadhila, kama ardhi ifanyavyo kwa mvua kwa kutoa matunda. Kwa kushindwa kwao kutoa matunda ya sadaka nyoyo zao huwa ngumu kwa sababu ya ukosefu wa uadilifu na kuwa watumwa wa manufaa ya duniani.

Lengo la kuumbwa kwa sifa mbaya ndani ya maumbile ya mwanadamu ni ili kumpima na kumtahini. Kwa sababu

Qudâî, Musnad al-Shihâb, II, 263; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, VIII, 31.

84. Bukhârî, Riqâq 5; Muslim, Zakât 114.

hii, aya ifuatayo katika Qur'an inasema, *"Na kwa nafsi na kwa aliyeitengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, Hakika amefanikiwa aliyeitakasa, Na hakika amekhasiri aliyeiviza."* (Qur'an, Shams, 91:7-10)

Daraja ya juu ya wanadamu, ambao wameumbwa na uchangamano mgumu na utambuzi wa hali ya juu, hufikiwa kwa kumtii Mwenyezi Mungu tu na kwa kuyatumia maisha yao katika kuzilinda nafsi zao dhidi ya mauovu.

Shambulio la Tabuk lilikuwa na changamoto nyingi. Maswahaba walitembea mamia ya kilometa wakati wa kwenda na wakati wa kurudi nyumbani. Walipokaribia Madina, hata sura zao zilibadilika kwa sababu ya njaa; ngozi zao ziligandamana kwenye mifupa, nywele na ndevu zao zilikuwa zimechakaa. Mtume Muhammad (s.a.w) akasema: " sasa tumetoka katika vita ndogo kwenda vita kubwa!.." Maswahaba waliuliza kwa mshangao mkubwa: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Kuna vita ngumu zaidi kuliko hii ambayo tumetoka kupigana?" Mtume Muhammad (s.a.w) akasema: "Sasa tunakwenda katika vita kubwa (vita dhidi ya nafsi)..."[85]

Vita dhidi ya nafsi hufundishwa kupitia malezi na mafunzo ya moyo. Lengo la vita hii ni kuinua na kukuza maadili na kumsaidia mwanadamu kufikia kwenye daraja ya ukamilifu, yaani *al-insan al-kamil.*

Siri hii yaweza tu kugundulika kupitia ukweli utokanao na Muhammad (s.a.w). Mwanadamu anaposhindwa kugundua sababu ya kuumbwa kwa ulimwengu huu, ulimwengu

85. al-Bagdâdî, Tarîkhu Bagdâd, XIII, 523; [Baadhi ya matoleo ya hadith hii yamesimuliwa kutoka kwa IbRahîm ibn Abi 'Abla kama hadith maktuu, Tazama; al-Mizzî, Tahdhîb al-Kamâl, II, 144; al-Zahabî, Siyar a'lâm al-nubalâ, VI, 325].

hummeza. Asiyetambua kwa nini amekuja hapa duniani huishi bila kuujua muundo adhimu mwanadamu. Wala hataweza kulitambua lengo la Mwenyezi Mungu kumuumba mwanadamu. Atashindwa kuelewa maana ya kuwa khalifa wa Mwenyezi Mungu Ardhini. Lakini wale wanaofanya jitihada za kuwa makhalifa wa Mwenyezi Mungu ardhini hugeuka kuwa jicho la Mola na sikio Lake.[86] Lengo lao katika maisha ni kuungana na Mwenyezi Mungu.

❀

Katika ulimwengu huu, baadhi ya vitu haviwezi kuelezewa kikamilifu na akili ya mwanadamu pekee. Hata maneno yetu nayo yanahitaji maneno mengine kuyaelezea. Tunapojaribu kuelezea jambo lisiloelezeka kwa kutumia njia zisizoeleweka, je tunakuwa hatusahau kwamba Mwenyezi Mungu pekee ndiye asiyeelezeka hasa na akili za mwanadamu? Mwenyezi Mungu ndiye pekee aisiyeelezeka kabisa katika ulimwengu huu. Tunaweza tu kumjua kwa kiwango tunachopata upendo na hekma, na kwa kiwango chetu cha kujisalimisha kwake.

Uwezo wa akili una mipaka. Ni kwa kutumia moyo ndipo tunapoweza kwenda nje ya mipaka ya akili, mahali ambapo kuna siri mbalimbali za ulimwengu. Nabii Ibrahim (a.s) alilielezea hili kama ifuatavyo. Alisema: *"Nimesilimu, nimenyenyekea kwa Mola wa walimwengu wote."* (Qur'an, Baqara, 2:131)

Imamu Ghazzali anasimulia uzoefu wake kuhusu suala hili kama ifuatavyo: "Niliinyoosha akili yangu mpaka ilipokaribia kufyetuka. Nikabaini kuwa ina kikomo. Haiwezi

86 Bukhârî, Riqâq 38; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 256; Ibn Hibban, al-Sahîh, II, 58; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, III, 346.

kuendelea hadi kwenye kitu cha mwisho kabisa ikiwa peke yake. Nilihisi uchizi na nilikaribia kupoteza akili zangu. Mwishowe, nilikimbilia kwenye Baraka ya kiroho ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Kila kitu kikawa wazi. Nikagundua siri na kusalimika."'[87]

Vivyo hivyo, Ibrahim (s.a.w) alisema: *"Ninakwenda kwa Mola wangu mlezi yeye ataniongoa!"* (Qur'an, Saffat, 37:99)

Naye Mawlana Jalaluddin Rumi pia anaelezea ukomo wa akili kama ifuatavyo : "Akili humpeleka mtu kwa daktari. Baada ya hapo, mtu anatakiwa akisalimishe kwa daktari."[88]

Kwa ufupi, tunalosema hapa ni kuwa siri za Mtume ziko nje ya kiwango cha uelewa wa akili ya mwanadamu.

Staha, Huruma na Uungwana katika Maisha ya Mtume wa Rehma

Kwa mujibu wa ripoti zisizohesabika kutoka kwa maswahaba, Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa mtu bora kabisa kuliko wanadamu wote kwa tabia na staha. Mara zote alitabasamu. Kulikuwa na mnga'o na nuru iliyotokeza usoni mwake.

Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa na moyo safi kiasi kwamba siku moja alipomwona bwana mmoja akitema mate chini, uso wake mtukufu ukawa mwekundu na kisha akainama. Maswahaba wakakimbia na kufunika yale mate. Kisha mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akaendelea na safari yake.

87. Ghazali, Abû Hâmid, al-Munqiz min al-Dalâl, (Beirut, 1988), uk. 60.
88. Rûmî, Jalâladdin, Mathnawî Ma'nawî, (Tehran, 1378), v.IV, 3323.

Mtume Muhammad (s.a.w) anasema kuwa mavazi safi ni kiashirio cha thamani ya juu ya Muislamu mbele za Mwenyezi Mungu. Aliusia kuvaa mavazi meupe. Alipendelea nguo yenye rangi nyeupe. Hii ni kwa sababu, nguo nyeupe ni safi, nzuri na iliyobarikiwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ambaye aliusia kuvaa mavazi nadhifu na kuchukia mavazi machafu, hakupenda nywele zisizokuwa maridadi wala ndevu chafu. Kwa mfano, siku moja mtu mwenye nywele na ndevu chafu ambazo hazijachanwa alikuja msikitini kwa Mtume . Huku akiashiria kwa mkono wake, alimpa Yule bwana ujumbe wa kuzitunza nywele pamoja na ndevu zake. Yule bwana akafanya kama alivyoagizwa na Mtume (s.a.w) akasema: "Huoni kuwa hivyo umependeza kuliko kuonekana kama shetani mwenye nywele na ndevu chafu?"[89]

Siku moja, Mtume (s.a.w) alimuona bwana mwingine mwenye nywele na ndevu chafu. Kwa mshangao, akauliza: "Kwa nini bwana huyu haoshi wala kuchana nywele zake?"[90]

Umar ibn Khattab (r.a) anasimulia kuwa:

"Fedhuli wa Kibedui alibisha hodi kwa Mtume Muhammad (s.a.w) mara tatu kwa sauti ya juu. Mara zote, Mtume (s.a.w) aliendelea kumstahi licha ya ufedhuli wake na akamuitika, 'karibu tafadhali'. ""[91]

Siku nyingine, alimwambia bwana mmoja aliyekuja akiwa amevaa nguo chafu:

"Una pesa? Vipi kuhusu kipato chako?"

---

89. Muwatta, Shar 7; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, V, 225.
90. Abû Dâwûd, Libas 13; Nasâî, Zînah 60; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, ID, 357
91. Tirmidhî, Zuhd 50; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 239; Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, VI, 344; al-San'ânî, al-Musannaf, I, 206.

Yule bwana alipomwambia kuwa alikuwa na pesa na kipato kizuri, Mtume akamwambia: "Kama Mwenyezi Mungu amekupa mali, anapenda akuone na athari ya mali hiyo!"[92]

Katika hadith nyingine anasema: "Mwenyezi Mungu anafurahi kuona athari za mali alizompa mja wake."[93] Matukio haya yanaonesha vizuri kabisa jinsi usafi wa moyo na maisha ya nje vinavyokamilishana katika Uislamu.

Ili kujilinda na kiburi na majivuno, Muislamu anayevaa nguo mpya anatakiwa atambue kuwa ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu na aombe dua kama Mtume (s.a.w) alivyofanya:

"Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenivika nguo hizi ijapokuwa sikuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Ewe Mwenyezi Mungu! Ninakuomba baraka tele kwa nguo hizi na kwa kazi ninayofanya nikiwa nimezivaa. Ninajilinda kwako dhidi ya shari ya mavazi haya na shari inayoweza kutendeka kutokana na kazi ya mavazi haya..."[94] Kwa kuomba hivyo, Mtume (s.a.w) alitaka kutumia kila kitu katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Vile vile, Mtume Muhammad (s.a.w) alionya dhidi ya moto wa jahannamu kwa kueleza kuwa wale wote wanaovaa kwa kiburi, majigambo, dharau na kujiona, watavaa vazi la aibu siku ya mwisho.

---

92. Nasâî, Zinâh 54; Tirmidhî, Birr 63; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 137; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XII, 234.
93. Tirmidhî, Adab 54; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 311; al-Hâkim, al-Mustadrak, IV, 150.
94. Abû Dâwûd, Libas 1; Tirmidhî, Da'avât 55; Ibn Mâjah, At'imah 16.

Abdullah ibn Amr, (r.a), anasimulia kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) hakuwahi kutumia maneno machafu kama yanayotumika katika lugha za kila siku.

Mtume (s.a.w) anasema, "Mambo yanayoonekana madogo kuhusu heshima, yale mnayoyachukulia kirahisi rahisi, yatakuwa muhimu sana siku ya hukumu." [95]

Siku moja Abu Dharr al-Ghifari alimwita Bilali "mtoto wa mwanamke mweusi." Pindi Mtukufu Mtume (s.a.w) aliposikia, alimwambia Abu Dharr al-Ghifari: "Ewe Abu Dharr! Hakika bado umebeba athari za zama za ujinga, zama za *Ujahliyya*."[96] Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliwahudumia wageni wake yeye mwenyewe, kama heshima kwao. Hakuvunja kanuni za uungwana hata alipokuwa mtoto. Alijulikana kwa huruma na ukaribu wake kwa masikini, mayatima, wajane na watu wasiokuwa na ndugu wa kuwasaidia.[97]

Anas (r.a) anasema: "Nilimtumikia Mtume Muhammad (s.a.w) kwa miaka kumi. Hakuwahi kunikemea kwa kuniuliza, 'kwa nini umefanya hivi?' pale ninapofanya kosa."[98]

Huruma yake iliwafikia hata mateka wa vita. Aliamuru watendewe wema.

❀

Huruma ya Mtume (s.a.w) iliwajumuisha viumbe wote. Alipomwona mtoto, uso wake ulijawa na furaha na ali-

95 Tirmidhî, Birr 61; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, X, 193; Ma'mar ibn Râshid, al-Jâmi', XI, 146; al-Qudâî, Musnad al-Shihâb, I, 274.

96 Bukhârî, Imân 22; Muslim, Aymân 38; Abû Dâwûd, Adab 124; Tirmidhî, Tafsir Surah 22,1; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 161.

97 Bukhârî, Nafaqât 1; Muslim, Zuhd 41-42.

98 Muslim, Fadâil 51; Abû Dâwûd, Adab 1; Dârimî, Muqaddimah 10.

wabeba watoto wa maswahaba zake mikononi mwake na kuwakumbatia. Hakusita kuwasalimia watoto, alicheza nao na kuwafanyia utani. Alipoona kundi la watoto wakiwa wanakimbia alijiunga na kuanza kukimbia nao.

Mtume huyu aliyetumwa kama Rehma kwa ulimwengu, alikuwa akiwachukua watoto juu ya ngamia wake pindi alipokutana nao. Anas (r.a) anaelezea mwenendo wake kama ifuatavyo: "Sikuwahi kuona mtu anayeheshimu haki za familia yake na watoto zaidi ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w)."[99]

Aishah (r.a) anasimulia kuwa siku moja, Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa akicheza na wajukuu zake. Bedui mmoja alipokuja na kuona vile akashangaa. Akauliza: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Je, huwa unawabusu watoto? Sisi huwa hatubusu watoto wetu. Na wala huwa hatuchezi nao." Kiongozi wetu (s.a.w) akamwambia:

"Kama Mwenyezi Mungu ameondoa huruma na hisia katika moyo wako, nikufanyie nini?"[100] Maneno haya yanaonesha msimamo wa Uislamu katika kuamiliana na watoto.

Mtume Muhammad (s.a.w) alimuweka mtoto wa Zayd, Usamah, na mjukuu wake, Hasan, kwenye magoti yake na wakati akiwakumbatia, alisema: "Ewe mola wangu! Wape Rehma na furaha watoto hawa! Kwasababu ninapenda wapate Rehma na furaha."[101]

---

99. Muslim, Fadâil 63; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 112; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XV, 400; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, II, 263.
100. Bukhârî, Adab 18; Muslim, Fadâil 64; Ibn Mâjah, Adab 3; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 56, 70.
101. Bukhârî, Adah, 18; Muslim, Fadâil 64.

Alikataza pia kuwalaani watoto. Hizi ni baadhi ya dalili ya huruma yake isiyokuwa na kikomo kwa watoto.

Mtoto akilia wakati mama yake anaswali, Mtume alimruhusu mama yake afupishe swala ili ambembeleze kwanza mtoto hadi anyamaze.[102]

Aliswali usiku kucha, huku akilia kwa ajili ya Ummah wake.[103] Alijitolea maisha yake yote ili kuwaokoa wanadamu dhidi ya moto wa jahannamu.[104] Hizi ni baadhi ya ishara za huruma yake kubwa.

Mwenendo wa Mfano kwa Watu

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa bora wa kuigwa, si tu kwa maneno yake, bali zaidi kwa matendo yake. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa mfano bora kwa watu katika nyanja zote za maisha. Alimheshimu kila mtu. Huruma yake kwa kila kiumbe haikuwa na kikomo. Hakuacha kuwafanyia wema na ukarimu hata makafiri.

Jabir ibn Abdullah anasimulia, "Siku moja, watu walikuwa wamebeba maiti. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akasimama. Nasi pia tukasimama. Baadaye, tukasema:

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Ilikuwa maiti ya Myahudi!"

Akajibu:

---

102. Bukhârî, Azan 65; Muslim, Salât 191; Abû Dâwûd, Salât 123; Tirmidhî, Salât 159; Nasâî, Imamah 35; Ibn Mâjah, Iqamah 49; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 109.
103. Muslim, Îmân 346; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 127; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XVI, 217.
104. Bukhârî, Riqâq 26; Muslim, Fadâil 17.

"Je, yeye sio mwanadamu?"[105]

Alikuwa rehma kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, alikuwa ishara ya jina la Mwenyezi Mungu la *al-Rahman,* aliyetumwa kwa ulimwengu wote. Maisha yake yalikuwa mfano halisi wa kanuni ya "vipende viumbe kwa ajili ya Muumba."

Siku moja Maswahaba, kutokana na mateso waliyotendewa na makafiri, walimtaka Mtukufu Mtume (s.a.w) aombe dua kuwalaani maadui wa Uislamu. Katika kuwajibu, Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema:

"Sikuja kwa ajili ya kulaani; nimekuja kama Rehma."[106]

Dua aliyowaombea maadui zake wakubwa ilikuwa kama ifuatavyo: "Ewe mola wangu! Hawajui wafanyalo! Wape uongofu!"[107]

Abdullah Ibn Ubayy alikuwa kiongozi wa wanafiki wa Madina. Yeye na wafuasi wake, wlimsaliti Mtume (s.a.w) siku ile muhimu sana kwa kujitenga na jeshi la Waislamu wakati wakielekea katika vita ya Uhud. Pia, alimsaliti Mtume (s.a.w) na umma wa Kiislamu katika matukio mengine mengi.

Kutokana na hekma ya Mwenyezi Mungu, mtoto wa Abdullah alikuwa tofauti na baba yake, alikuwa muumini wa kweli. Wakati Abdullah ibn Ubayy alipofariki, mwanae alikuja kwa Mtume kumuomba kanzu yake ili akaifadhi maiti ya baba yake, kwa matumaini kuwa atapata Baraka kutokana na kanzu hiyo. Mtukufu Mtume (s.a.w) hakumvunja moyo

105. Bukhârî, Janâiz 50; Muslim, Janâiz 81.
106. Muslim, Jihad 104; Abu Yaia, al-Musnad, XI, 35; al-Bayhaqi, al-Sunan al-Kubrd, III, 352; al-Tabarani, al-Mu'jam al-Awsat, III, 223.
107. Bukhârî, Anbiyâ 54; Muslim, Jihâd 104; Ibn Mâjah, Fitan 33; Ibn Hibban, al-Sahîh, III, 254.

swahaba wake, alimpa kanzu yake ili akaihifadhi maiti ya mnafiki ambaye pia mhusika mkuu katika tukio la *Ifk*, tukio la kashfa dhidiya bibi Aisha (r.a), mke wa Mtukufu Mtume (s.a.w).[108]

Je, inawezekana kutafuta mfano hai sawa na huo wa utu na wema katika historia ya ulimwengu?

Muhammad (s.a.w) alikuwa mfano bora kabisa wa huruma. Siku moja alikuwa akiswali, akamsikia Bedui mmoja akiomba dua: "Ewe mola wangu! Mbariki Muhammad na mimi tu, na si wengine!" Baada ya kumaliza swala, Mtume akamwambia: "Unafanya yaliyo makubwa kuwa madogo."[109]

Mtume (s.a.w) hakuwa mtu wa zama na watu walioishi karibu naye tu. Alisimama katika nafasi ambayo aliweza kuwaunganisha wanadamu wote chini ya bendera ya upendo, huruma na furaha, kwa kuwaunganisha katika nuru ya Uislamu na kwa kuyabadilisha mazingira ya nyoyo ngumu, mazingira ya umimi na ubaguzi. Mafanikio aliyoyapata katika eneo hili ni ukurasa unaong'aa zaidi katika historia ya mwanadamu.

Kwa mtazamo huu, alikuwa mwalimu na mlezi bora kabisa kwa wanadamu wote kutokana na malezi ya kimungu aliyoyapata. Madhalimu, walikuwa wakiwazika mabinti zao wakiwa hai na kuwatendea unyama watumwa wao, walipata uongofu chini ya kuba la rehma yake. Malezi haya yalikuwa na athari kubwa mno kiasi kwamba baadhi ya watu hawa

108. Bukhârî, Janâiz 23; Muslim, Munafiqun 4; Abû Dâwûd, Janâiz 1; Nasâî, Janâiz 40; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad II, 18.

109. Bukhârî, Adab 27; Ibn Majah, Taharah 78; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 239.

walipata utimilifu na maadili yaliyowawezesha kuwa watu bora na wenye kuheshimika mno ulimwenguni.

❀

Mtume wetu Muhammad (s.a.w) aliwasaidia watu wote bila ubaguzi na kulingana na mahitaji yao. Tukio lifuatalo linaakisi mwenendo huu.

Siku moja Bedui alimjia Mtume ili ampe msaada. Alimpa kila alichokuwa nacho na kumuuliza: "Je umeridhika?"

Bedui huyo ambaye hakuwa na haya akajibu: "Hapana! Haujanipa vya kutosha!"

Hapo, baadhi ya maswahaba walikasirishwa na ile tabia na walitaka kumgombeza. Lakini, Mtukufu Mtume (s.a.w), aliwakataza kufanya hivyo. Alimchukua yule Bedui hadi nyumbani kwake. Akampa yule Bedui sadaka nyingi zaidi na kumuuliza:

"Je hizi zitakutosha?"

Mara hii yule Bedui alikuwa na furaha. Akajibu: "Ndio! Mwenyezi Mungu akupe Baraka tele kwa niaba yangu, familia yangu na ndugu zangu!"

Kisha, Mtume (s.a.w), alitaka kuondoa hisia mbaya iliyokuwepo kati ya Bedui na Maswahaba wake, akamwambia:

"Umesema ulichoweza kusema pale mwanzo kwasababu ulifikiri tulichokupa kilikuwa hakikutoshi. Kwa sababu hii, maswahaba wangu wanaweza kuwa wamekufikiria vibaya. Kwahiyo tutakaporudi kwao rudia kama ulivyosema ili hisia zao mbaya ziondoke nyoyoni mwao."

Waliporudi pale walipokuwa maswahaba, Bedui

alimgeukia Mtume (s.a.w) na kumwambia: "Mwenyezi Mungu akupe Baraka tele kwa niaba yangu, familia yangu na ndugu zangu!!"

Baada ya yule Bedui kuondoka, Mtume (s.a.w) aliwageukia maswahaba wake na kuwaambia : "Tukio hili lililotokea kati yangu mimi na huyu Bedui ni sawa na tukio la mtu ambaye ngamia wake amemtoroka. Pindi kundi la watu walipomkimbiza ngamia yule ili kumkamata, ngamia yule alizidi kuingiwa na hofu. Kisha mmiliki wa ngamia yule akawaita wale watu: "Tafadhali niacheni mimi na ngamia wangu! Namjua kuliko mnavyomjua nyinyi na namtendea wema kuliko mnavyomtendea nyinyi." Akamfuata ngamia wake peke yake. Akaokota tende na kumpa yule ngamia. Yule ngamia akasogea na kumfuata. Akaweka shogi juu ya yule ngamia, akapanda na kuondoka. Vivyo hivyo, kama ningewasikiliza pindi yule Bedui aliposema kile alichoweza kusema, Bedui yule masikini angekwenda katika moto wa jahannamu."[110]

Kauli hii ni muhimu sana kutokana na ujumbe iliyoubeba kuhusu malezi ya mwandamu. Ni muhimu sana kuzingatia saikolojia ya mwanadamu. Kisha njia inayoelekea kwenye moyo wa mtu husika hupata kugunduliwa.

Mtu anayetaka kufikia lengo lake hana budi kupita katika njia hizi. Vinginevyo, jududi yake ya kutoa mafunzo na malezi itazaa matokeo hasi na kuongeza tabu na mashaka.

Funzo lingine tunalojifunza katika tukio hili ni kama ifuatavyo: wanadamu hughilibiwa na wema na ukarimu kwa

110. al-Marwazî (d.294), Ta'zim qadr al-salât, II, 931; al-Haythamî, Majma'alzawâid, IX, 160.

sababu wameumbwa wadhaifu. Mtu akifanyiwa ukarimu, kama akiwa adui yako, atapunguza uadui; kama sio adui au rafiki yako hugeuka kuwa rafiki; na kama ni rafiki yako basi huzidi kuwa rafiki wa karibu.

Wahenga wetu wanasema: "Ukarimu wa hata kikombe cha kahawa hukumbukwa kwa shukurani kwa miaka arobaini."

Staha na Adabu za Mtume wa Rehma (s.a.w) kwa Masikini

Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na huruma na upole wa hali ya juu kwa masikini ili kufidia ukosefu wa mali waliokuwa nao. Abdullah ibn Amr anasimulia kisa kifuatacho:

"Siku moja, Mtume (s.a.w) alikuja msikitini. Masikini walikuwa wamekaa kwenye kona moja. Alienda kukaa pamoja nao kama ishara ya kuonesha heshima aliyokuwa nao kwao. Aliongea nao na kuwaambia: 'Habari njema kwa masikini wahamiaji! Wataingia katika bustani za pepo miaka arobaini mapema zaidi kuliko matajiri. Hesabu ya maskini siku ya hukumu itaisha haraka kuliko ile ya matajiri kwa sababu hawana mali wala fedha'."[111]

Mara kwa mara, Mtume (s.a.w) alikuwa akiomba dua ifuatayo kutokana na wasiwasi wake kuhusu mzigo mzito wa hesabu siku ya Kiyama:

"Ewe mola wangu! Nifanye niishi kama masikini. Nijaalie nife kama masikini. Nifufue kati ya watu masikini."[112]

---

111. Tirmidhî, Zuhd 37; Dârimî, Riqâq 118; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 63; Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, III, 443; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VII, 12.
112. Tirmidhî, Zuhd 37; Ibn Mâjah, Zuhd 7; al-Hakim, al-Mustadrak, IV, 358; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VII, 12

Mitume wote wataingia peponi. Lakini, kila mmoja ataulizwa kuhusu neema walizopewa na ujumbe walioaminiwa kuufikisa kwa ummah wao. Aya ifuatayo katika Qur'an anaelezea kuwa kila mtu, hata mitume wataulizwa:

"Na kwa yakini tutawauliza wale waliopelekewa ujumbe napia tutawauliza hao Wajumbe." (Qur'an, Araf, 7:6)

kwa mfano, Nabii Suleiman (s.a.w) ataingia peponi baada ya mitume wengine wote kwa sababu alipewa utajiri na ufalme, kwa hiyo hesabu yake itachukuwa nuda mrefu sana.

Kulikuwa pia na maswahaba wa Mtume (s.a.w) waliokuwa matajiri pia. Walisifiwa na Mtukufu Mtume kwa kuzitoa mali na nafsi zao katika njia ya Mwenyezi Mungu. Pia Mwenyezi Mungu aliwapa habari njema katika aya ifuatayo: *"Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu wanaua na wanauawa. Hii ni ahadi aliyojilazimisha kwa haki katika Taurati, na Injili na Qur'an, Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu?Basi furahini kwa biashara yenu mliofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa."* (Qur'an, Tawba, 9:111)

❀

Miongoni mwa watu waliokuwa na mali rafiki wa karibu sana wa Mtukufu Mtume, Abu Bakr, ambaye licha ya utajiri wake aliishi maisha ya unyenyekevu. Ametajwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'an kama "wa pili kati ya wawili."Aliheshimika sana kati ya wafanyabiashara wa Kiquraysh. Kwa mujibu wa bibi Aishah (r.a), Abu Bakr alipofariki dunia hakuacha *dirham* (fedha) wala *dinar* (dhahabu). Aliacha tu ngamia na mtumwa aliyejua kutengeneza upanga.

Katika wosia wake kwa binti yake, alisisitiza kuwa mtumwa huyu akabidhiwe kwa Umar, Khalifa wa pili baada yake. Alitumia utajiri wake kwa njia yenye faida, kwa kuitumia katika kumhudumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na alitumia fedha zake kwa ajili ya dini. Katika miaka ya mwanzo ya Uislamu, ambacho kilikuwa kipindi kigumu sana, alitumia mali zake kuwanunua na kisha kuwaacha huru watumwa wa Kiislamu ambao walikuwa wanateswa vikali na wamiliki wao wa kikafiri kwa kuukubali Uislamu.

Utajiri wake haukumzuia kuishi maisha ya kujizuia na raha za dunia, au *zuhd*. Kinyume chake, kwa kutumia mali yake kikamilifu, alikuwa mmoja wa mifano mikubwa ya namna ya kuishi maisha ya kuipa kinyongo dunia licha ya utajiri wake. Kwasababu hii mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliuheshimu utajiri wake na kumwambia:

"Tumelipa vyote tulivyopata kutoka kwa watu isipokuwa vya Abu Bakr. Msaada wake kwetu ni mkubwa sana kiasi kwamba Mwenyezi Mungu ndiye atakayemlipa kwa hili siku ya hukumu. Sijafaidika na mali ya mtu kama nilivyofaidika na mali ya Abu Bakr. Kama ningeambiwa nichague rafiki basi ningemchagua Abu Bakr."[113]

❀

Mtume Muhammad (s.a.w) anasema: "Wanadamu wote ni sawa kama meno ya chanuo isipokuwa wanatofautiana katika kumcha Mungu."[114]

113. Tirmidhiî Manâqib 15; Ibn Mâjah, Muqaddimah 11; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 253, 366; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XV, 273.

114. âl-Qudâî, Musnad al-Shihâb, I,145; al-Hatib al-Bagdadi, Tarikhu Bagdad, VII, 57; Ibn 'Adiyy, al-Kamilfial-du'afa, III, 248; Ibn Hibban, al-Majrrlhin,I, 198; Ibn Hagar al-'Asqalani, Lisdn al-mizdn, II, 42.

Hapo mwanzo, Maswahaba walikuwa wamegawanyika kikabila, rangi, mtwana na mtumwa, tajiri na masikini. Walikuwa wamegawanyika katika matabaka na kila mmoja alikuwa tayari kumwaga damu ya mwenzie. Lakini baada ya kupata neema ya kuukubali Uislamu waliishi katika mazingira ya undugu uliojaa upendo chini ya Baraka kubwa ya msingi mkuu ulioelezwa katika hadith hii. Tukio lifuatalo litaelezea zaidi juu ya hili.

Baada ya kukombolewa kwa Makkah, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alifanya uamuzi wa kuwashambulia Warumi kwa mara ya pili. Alimchagua Usamah mtoto wa Zayd kuwa kamanda wa jeshi. Usamah alikuwa na miaka ishirini na moja na alikuwa ni mtoto wa mtu aliyewahi kuwa mtumwa. Safari ya kuondoka kwa jeshi ilichelewa kwa sababu ya kifo cha Mtukufu Mtume (s.a.w).

Lakini khalifa mpya, Abu Bakr, akaliagiza jeshi liendelee na kazi yake kama ilivyopangwa na Mtukufu Mtume (s.a.w) kabla ya kifo chake. Baadhi ya maswahaba wakubwa wa Mtume na masharifu wa Kiquraysh walifuatana na kamanda huyu mdogo mwenye miaka ishirini na moja. Hata Abu Bakr, licha ya kuwa Khalifa, alimsindikiza hadi mwisho wa Madina huku akitembea kwa miguu. Usamah akateremka juu ya farasi wake na kumtaka Abu Bakr apande juu ya farasi huyo. Lakini, alijibu kama ifuatavyo:

"Ewe Usamah! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu amekuchagua wewe. Acha miguu yangu ipate vumbi katika njia ya Mwenyezi Mungu!"[115]

115. Ibn Kathîr, al-Bidâyah wan-nihâyah, III, 309.

Kama tunavyoona, wale walitunukiwa heshima ya kulelewa kwenye mikono ya Mtukufu Mtume (s.a.w) kamwe hawakubaguliwa kwa kupewa majina kama vile mtumwa, masikini, tajiri, mtwana, kijana, mzee, na kadhalika. Majina haya yalitupwa mbali na badala yake muumini yeyote alikuwa huru kupanda daraja kutegemea na ikhlasi na sifa za kimaanawi na kiroho.

Ma'rur ibn Suwayd anasimulia kisa kifuatacho:

"Nilimwona Abu Dharr akiwa na nguo mpya. Mtumwa wake pia alikuwa amevaa nguo mpya. Nilimuuliza sababu. Akanisimulia kuwa Mtume (s.a.w) alisema:

'Watumwa ni ndugu zenu ambao Mwenyezi Mungu amewakabidhi kwenu kama amana ili wawahudumie. Yeyote kati yenu ana nduguye anayemhudumia, basi ampe ndugu yake huyo chakula chake mwenyewe na amvike kama kile avaacho yeye mwenyewe. Asimpe kazi iliyo nje ya uwezo wake. Kama atafanya hivyo, basi amsaidie.'"[116]

Siku moja, mjumbe wa Mwenyezi Mungu, alimkumbuka mtumwa mweusi na kumuulizia:

"Kitu gani kimempata mtu yule? Sijamuona kwa muda."

"Alikufa, Ewe mjumbe wa Mwenyezi Mungu," wakajibu. Mtukufu Mtume (s.a.w) akawawalaumu: "Kwa nini hamkuniambia?"

Ndipo Maswahaba walipomueleza nini kilichompata mtumwa yule. Hawakuona kama jambo lile ni la muhimu na walifikiri kuwa ni jambo la kawaida tu. Mjumbe wa

116. Bukhârî, Imân 22; Muslim, Aymân 40; Abû Dâwûd, Adab 124; Tirmidhî, Birr 29; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 58, 161.

Mwenyezi Mungu (s.a.w) akawaambia: "Nionyesheni kaburi lake!" Kisha akaenda pale kaburini na kuswali swala ya maiti.[117]

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu(s.a.w) alikuwa akifurahi kwa kuwaachia huru watumwa na kuwanyanyua kwenye daraja ya watu wengine. Mfano mzuri wa hili ni uhusiano wake na Zayd ibn Haritha, ambaye alikuwa zawadi kwakwe kutoka kwa bibi Khadija (r.a). Alimwacha huru Zayd na kumpa haki ya kuchagua kati ya kubaki naye au aende kwa wazazi wake. Lakini Zayd akamchagua Mtume (s.a.w) japokuwa alikuwa akipitia nyakatingumu, akipata mateso na propaganda za Maquraysh dhidi yake. Baadaye, swahaba huyu alifikia daraja ya juu kati ya maswahaba kiasi kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w) alipomchagua kuwa kamanda wa jeshi katika vita vya Tabuk dhidi ya Warumi. Alifikia daraja ya kufa kishahidi katika vita hii na kuvirithisha vizazi vingine maisha yanayong'aa kama nyota.[118] Kwa kifupi, maisha yake yalikuwa kama maisha ya Nabii Yusuph(s.a.w) aliyeinuliwa kutoka utumwani hadi kwenye ufalme.

Kamwe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakukubali kuwanyanyasa watumwa. Alisema kuwa:

"Wale wanaowanyanyasa watumwa wao hawawezi kuingia peponi."[119]

Huruma ya Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa watumwa ili-

117. Bukhârî, Salât 72; Muslim, Janâiz 71; Abû Dâwûd, Janâiz 57; Ibn Mâjah, Janâiz 32; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 353, 388.

118. Ibn Hagar al-'Asqalâni, al-Îsâbah fi tamyîz al-sahâbah, II, 598-601; Ibn Abdilbarr, al-İstî'âb fî ma'rifatil-ashâb, II, 542-546.

119. Tirmidhî, Birr 29; Ibn Mâjah, Adab 10; Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, I, 7; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, IX, 124; Abû Ya'lâ, al-Musnad, I, 94.

fikia hatua kwamba hakutaka kuwaita kwa majina ya "mtumwa" au "kijakazi", bali aliwausia na kuwaamuru Waislamu wawaite kwa majina ya "mwanangu"au "binti yangu".[120]

Yeye mwenyewe alikuwa akiwatembelea watumwa, kuongea nao, kuwatembelea wagonjwa miongoni mwao, kuitikia mialiko yao na alihudhuria mazikoni.

Abu Daud anasimulia kuwa yafuatayo yalikuwa maneno ya mwisho ya Mtume (s.a.w) : "Ichungeni sana swala! Muogopeni Mwenyezi Mungu kwa watumwa mnaowamiliki!" (Abu Dawud, Adab, 124)

Maswahaba wote walikuwa na lengo la kutekeleza kikamilifu tabia bora za Mtukufu Mtume (s.a.w). Tukio lifuatalo linaonesha hisia za utiifu, uaminifu na ukarimu aliokuwa nao Umar (r.a). Aslam, mmoja kati ya Maswahaba, anasimulia:

"Siku moja, nilikwenda sokoni na Umar ibn al-Khattab (r.a). Binti mmoja alimjia Umar (r.a) kwa nyuma na kumwambia:

'Ewe, *Amir* wa waumini ! Mume wangu amekufa na kuacha watoto. Wallah, hawawezi kufanya chochote. Hawawezi hata kujihudumia. Hawana ardhi ya kulima, wala mnyama kwa ajili ya maziwa. Ninahofia kuwa umasikini na njaa vitawaua kama wanyama wa mwituni. Mimi ni binti wa Huffaf ibn Ayma al-Ghifari. Baba yangu alikuwepo wakati wa mkataba wa Hudaybiya...' Umar (r.a) aliposikia maneno hayo, alisema: 'Hiyo ni heshima kubwa!'

120. Bukhârî, Itk 17; Muslim, Alfaz 13,15; Abû Dâwûd, Adab 75; Ahmad b.Hanbal, al-Musnad, II, 316, 423.

Kisha akaenda mahali wanyama kwa ajili ya *zakat* walipokuwa wamewekwa. Akambebesha ngamia shupavu magunia mawili makubwa ya chakula. Kati ya magunia haya mawili, aliweka chakula zaidi na baadhi ya nguo. Akampa yule mwanamke ile kamba ya ngamia na kumwambia:

'Mchukue huyu ngamia. Kabla haujamaliza hivi, Mwenyezi Mungu atakufungulia mlango wa baraka.' Alimuombea dua.

Mtu mmoja aliyekuwa pembeni yake akasema:

'Ewe, *Amir* wa waumini! Umempa vitu vingi sana yule mwanamke!'

Umar akajibu kwa kusema:

'Baba yake alikuwa pamoja na Mtume (s.a.w) kwenye mkataba wa Hudaybiya. Wallah, nilishuhudia mwenyewe, baba yake na kaka yake wamezingira ngome na kuiteka. Walipoiteka ile ngome, nasi pia tulipata fungu letu kutokana na ngawira zile. '[121]

Tukio lifuatalo ni mwale wa nuru inayoakisi tabia ya moyo wa Umar (r.a) ilivyokuwa.

Katika Maswahaba, Aslam anasimulia kuwa "Siku moja usiku tulikuwa tunakagua kilima cha *Waqim* huko Madina. Tulimwona mwanamke mwenye watoto ndani ya nyumba moja. Watoto walikuwa wanalia. Kulikuwa na sufuria lenye maji jikoni. Umar (r.a) akamuuliza yule mwanamke kwanini watoto walikuwa wanalia. Akajibu: 'Kwasababu ya njaa'.

Macho ya Umar yalijawa na machozi baada ya kubaini kuwa hamna chochote kilichokuwa kinachemshwa zaidi

121. Bukhari, Magâzî 35.

ya mawe. Hii ndio mbinu aliyoitumia mwanamke yule kuwadanganya watoto ili walale. Alienda kwenye ghala ambalo mazao kwa ajili ya sadaka yaliwekwa. Akaweka unga kwenye gunia kubwa na kulibeba begani na kuipelekea familia ile. Nilitaka kumsaidia lakini akakataa na kunimbia,

'Ewe, Aslam! Nitalibeba. Nitaulizwa kuhusu watoto hawa Siku ya Kiyama.'

Tuliporudi nyumbani kwa mwanamke yule, Umar alishiriki katika kupika pia. Mkono mmoja alichochea moto na mwingine alikoroga supu. Niliona moshi ukifika hadi kwenye ndevu zake jinsi alivyokuwa anapika. Kisha aliwapakulia watoto chakula. Watoto waliposhiba alikaa pamoja nao. Alikuwa anatisha kama simba. Niliogopa kusema chochote. Alikaa hadi watoto walipoanza kucheka na kucheza.

Kisha akasimama na kusema:

'Ewe, Aslam! Je unajua kwanini nimekaa nao? Nilipowaona walikuwa wanalia. Sikutaka kuwaacha bila kuwaona wakicheka. Nilipowaona wakicheka nilifarijika.' Tunatakiwa tukumbuke kuwa matajiri wenye shukurani, wanyenyekevu, wakarimu wanaotenda kulingana na mahitaji ya wanadamu, Mwenyezi Mungu amewapa heshima sawa na maskini wenye subira wanaoishi kwa utu na heshima. Ukarimu na huruma huwapeleka watu kwenye furaha Akhera kwa kuwalinda na masaibu ya ulimwengu huu. Vile vile habari njema zinawasubiri wale wenye kustahmili maumivu ya subira.

Hadith ifuatayo inaelezea vizuri jinsi ya kuwa na shukurani na jinsi ya kuwa mvumilivu; mambo haya mawili yanatakiwa kutekelezwa katika nyanja mbalimbali za maisha ili kufikia ukamilifu wa moyo.

"Ninampenda muumini ambaye shughuli zake zinaambatana na tabia njema. Sifa hiyo hawezi kuwa nayo isipokuwa muumini. Huwa anashukuru anapopata baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, jambo ambalo ni kheri kwake. Vile vile, anapopatwa na tatizo huonesha uvumilivu, jambo ambalo pia ni kheri kwake."[122]

Siku moja, Mtume (s.a.w) alipokuwa amekaa Madina, watu wa kabila moja masikini walikuja. Walikuwa hawana viatu. Ngozi zao ziligandamana na mifupa yao kwa sababu ya njaa. Mtukufu Mtume (s.a.w) alishikwa na huzuni sana alipoona hali zao na rangi yake ilibadilika. Alimwambia Bilali (r.a) atoe adhana na kuwakusanya maswahaba. Kutoka kwa maswahaba zake alichangisha mchango kwa ajili ya kabila hilo, akawasaidia.[123]

Katika jamii utawaona masikini, matajiri na watu wa tabaka la kati. Katika aya za Qur'an na mafundisho ya Mtukufu Mtume (s.a.w), unapata kanuni za Kiislamu zinazoelezea uhusiano wa makundi haya. Masikini mvumilivu na tajiri mwenye shukurani ni makundi mawili yaliyosifiwa na Mwenyezi Mungu na Mtukufu Mtume (s.a.w).

Jukumu la matajiri ni kutoa sadaka katika yale waliyopewa na Mwenyezi Mungu, na ni jukumu la masikini kuonesha uvumilivu kwa kile Mwenyezi Mungu alichowanyima. Abdurrahman ibn Awf, Abu Bakr na watu wa aina yao ni mfano bora wa matajiri wenye kushukuru. Vivyo hivyo, Abu Dharr al-Ghifari, Abu al-Darda na watu aina yao ni mfano wa masikini wenye uvumilivu. Mfumo wa maisha

122. Muslim, Zuhd 64; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 16; Ibn Hibbân, al- Sahîh, VII, 155.

123. Muslim, Zakât 69, 70; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 358, 361.

ya makundi yote mawili ulikuwa sawa kwa sababu mtazamo wao wa maisha ulitafsiriwa na kanuni ya "mali zote ni milki ya Mwenyezi Mungu."

Kwasababu hii, Uislamu haupingani na masikini au matajiri wema, bali unawapa habari njema za kupata pepo wapo wataendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Kwa sababu ya uwepo wa watu maskini, Mwenyezi Mungu hutoa na baraka kwa jamii. Kwasababu ya masikini, Mwenyezi Mungu husaidia jamii kwa wingi. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema kuhusiana na suala hili:

"Mwenyezi Mungu anausaidia ummah huu kwa sababu ya dua za masikini, swala zao na ikhlasi yao."[124]

Kutokana na ukweli huu, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akianza vita kwa dua za maskini wa Kiislamu kwa sababu alitegemea ushindi kutokana na ikhlasi yao. Alipoiona hali umaskini wa watu wa Suffa, alisema:

"Lau mngejua mlichoandaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu, mngeomba umasikini wenu uongezeke."[125] Aliwasifu na kuonesha umuhimu alioutoa kwa masikini.

Vile vile, kwa kuzingatia matatizo ya kiuchumi waliyokuwa nayo Waislamu, alisema: "Mwanadamu hana haki zaidi ya nyumba moja kumpa hifadh, mkate wa kumlisha, nguo ya kujisitiri na maji kwa ajili ya kunywa."[126]

---

124. Bukhârî, Jihâd 76; Abû Dâwûd, Jihâd 70; Tirmidhî, Jihâd 24; Nasâî, Jihâd 43; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I,173.
125. Tirmidhî, Zuhd 39; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 502; al-Bazzâr, al-Musnad, IX, 205; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, XVIII, 310.
126. Tirmidhî, Zuhd 30; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 62; al-Kissî, Musnad 'Abd ibn Humayd, I, 46; al-Hâkim, al-Mustadrak, IV, 347; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, V, 157.

Vile vile Alieleza kuwa maskini ndio watakuwa wa kwanza kunywa maji ya mto Kawthar na Mwenyezi Mungu anawapenda wale wote wenye uvumilivu na wale wote wenye kumtegemea Mwenyezi Mungu licha ya umasikini wao.[127]

Aidha, Mtume Muhammad (s.a.w) anasema, "Wapo wengi kati yenu wenye nywele na ndevu ziszokuwa maridadi na muonekano wa kimasikini. Lakini wakiomba wanaomba dua, Mwenyezi Mungu huzikubali dua zao na kamwe hata waangusha. Bara ibn Malik ni miongoni mwao."[128]

❀

Bara, ambaye alikuwa ni kaka wa Anas, alikuwa hana mahali pa kuishi wala chakula. Chakula chake ilikuwa shayiri iliyomtosha kuishi. Watu wauoupokea umasikini kwa furaha ni miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu anaowakubalia dua zao.

Maswahaba walijua kilichosemwa na Mtume (s.a.w) kuhusu Bara, walimuomba Bara awaombee dua kwa sababu walikuwa karibu kushindwa vita wakati wa utawala wa Umar. Aliomba dua na kusema:

"Wallah! Kesho mtapata ushindi na mimi nitakufa kishahidi!..."

Hakika, siku iliyofuata Waislamu walishinda na Bara akapata rehma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, al-Rahman, kwa kuwa shahidi, kitu ambacho alikisubiri kwa hamu kwa

127. Tirmidhî, Qiyâmah 15.
128. Tirmidhî, Manâqib 54; Ma'mar ibn Râshid, al-Jâmi', XI, 306; al-Bazzâr,al-Musnad, V, 404; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, I, 264.

muda mrefu. Hivyo, tunaweza kuona muujiza mwingine zaidi wa Mtume (s.a.w).[129]

❀

Maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w) yamejaa miujiza, uaminifu, utiifu, wema, huruma na heshima. Siku moja alimwambia mkewe Aishah:

"Ewe Aishah! Onesha huruma kwa masikini! Waweke karibu yako ili Mwenyezi Mungu pia akuweke karibu naye siku ya hukumu!..."

Alimuusia kama ifuatavyo:

"Ewe Aishah! Usimuondoshe maskini kutoka mlangoni mwako mikono mitupu; jilinde na moto wa jahannam hata kwa kipande cha tende!"[130]

Jinsi Mtume wa Rehma alivyoilea jamii Hatua kwa Hatua

Uislamu ni mfumo unaoendeleza jambo hatua kwa hatua. Hivyo, hauikatai mifano mizuri ya desturi za zamani; badala yake huziendeleza zile sehemu nzuri katika desturi husika na kuzirekebisha zilizokuwa mbaya. Uislamu hauoni madhara yoyote katika kutunza vipengele chanya vya mambo ya kale kwa vigezo vya wazi ilivyoviweka. Kwa kutumia vigezo hivi, Uislamu umejaribu kuihusisha desturi fulani badala ya kuitupilia mbali.

Wale tu wanaojiamini wao na kazi yao ndio wenye kuweza kufanya mabadiliko ya hatua kwa hatua yatakayoku-

129. Ibn Abdilbarr, al-Istî'âb, 1,154; Ibn Hagar al-'Asqalânî, al-Isâbah, I, 281.
130. Tirmidhî, Zuhd 37; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VII, 12.

wa jumuishi kwa haraka na yatakayobadilisha mfumo wa kijamii. Aina hii ya utekelezaji wa hatua kwa hatua hauwi mzigo wa ghafla kwa jamii. Matokeo yake ni kwamba, athari mbaya zinazoweza kutokea hudhibitiwa mapema. Mfano mzuri wa hili ni jinsi Uislamu ulivyoondoa utumwa. Uislamu uliibadilisha desturi ya utumwa na kuifanya kuwa utambulisho wa kawaida. Uislamu uliiweka desturi ya utumwa ndani ya misingi mizuri katika namna ambayo hatimaye ingepelekea desturi hiyo kufutika kabisa.

Uislamu ulihifadhi utumwa kwa jina tu na kwa muda mchache, kwa lengo la kuumaliza kabisa. Hivyo basi, kuushutumu Uislamu kuwa unatetea utumwa ni kutokana na ujinga na ushabiki wa wanaotoa hizo tuhuma. Katika sheria ya Kiislamu, ili kusamehewa baadhi ya dhambi, lazima mtu amwache huru mtumwa. Baada ya kuweka sheria hizi, Uislamu ukawanyanyua watumwa kutoka katika mikono ya wamiliki wao. Ikabaki tofauti ndogo sana kati ya mtu huru na mtumwa. Mtume (s.a.w) ndiye aliyekuwa wa kwanza kutumia kanuni ya kushiriki chakula kimoja na mtu kuvaa nguo sawa na mtumwa wake. Desturi ya utumwa, ambayo hapo kabla ilikuwa desturi ya ukandamizaji, ikapoteza sifa yake baada ya Uislamu kusisitiza kuwa haki za watu wote ziheshimiwe.

Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwaamuru wamiliki wa watumwa wawaelimishe na kuwasaidia waweze kuoa baada ya kuwaachia huru. Alionya kuwa wale wote wanaowatendea vibaya watumwa wao hawataingia peponi.

Alihamasisha kuwacha huru watumwa na kusema kuwa ni moja kati ya ibada kubwa kabisa. Siku moja, alimshuhudia Abu Dharr akimtendea vibaya mtumwa wake bila kujua. Alihuzunika sana na kumuuliza Abu Dharr:

"Ewe Abu Dharr! Je, bado una mambo ya zama za ujinga kabla ya kuja dini ya kweli?" Akaendelea kusema: " usiwatendee ubaya viumbe wa Mwenyezi Mungu! Kama hawakuridhishi waachie huru . Usiwape kazi ngumu na ukifanya hivyo basi wasaidie."[131]

Bwana mmoja alimwozesha mtumwa wake kwa binti ambaye pia alikuwa mtumwa. Lakini, baadaye akataka waachane. Yule mtumwa akamlalamikia Mtume, Mtume akamwambia yule mmiliki wa mtumwa:

"Haki ya kuoa na kuacha si yako; acha usiingilie!"[132]

Mara kwa mara Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa akiwataka maswahaba wake kusamehe makosa ya watumwa wao. Siku moja, binti mmoja mtumwa alipopoteza pesa aliyokuwa amepewa na mmiliki wake kwa ajili ya kununulia unga. Alishindwa kurudi nyumbani kwasababu aliogopa kuadhibiwa. Alikaa njiani huku akilia. Mtukufu Mtume (s.a.w) alipomsikiliza, alimpa pesa kiasi kama kile alichopoteza na kumrudisha nyumbani kwa sababu hakuwa na hakikika na jinsi ambavyo mmiliki wake angemtendea. Akawashauri wawe na huruma. Kutokana na ushauri na wosia waliopewa na Mtume wale maswahaba wakamsamehe yule binti.

Nukta nyingine muhimu tunayotakiwa kuizingatia ni kwamba Uislamu uliukubali uhalali wa utumwa kwa sababu ya kuwepo kwa vita ambazo ilikuwa ngumu kuzikomesha.

131. Bukhârî, Îmân 22; Muslim, Aymân 38; Abû Dâwûd, Adab 124; Tirmidhî, Birr 29; Ibn Mâjah, Adab 10; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 36.

132. Ibn Mâjah, Talak 31; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VII, 360, 370; al-Daraqutni, al-Sunan, TV, 37; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, XI, 300.

Miongoni mwa matokeo yaliyotarajiwa katika vita ni uwepo wa mateka na watumwa. Kwa kuwa Uislamu unajipambanua kwa huruma na upole, unahamasisha kuwatendea sawa watumwa na watu waliohuru. Zayd, licha ya ukweli kuwa aliachiwa huru na Mtukufu Mtume (s.a.w), aliamua kuishi na Mtume mpaka mwisho wa uhai wake na alikataa kurudi kwa wazazi wake.

Mtume Muhammad (s.a.w) anasema,

"Mpe anayekupikia sehemu katika chakula hicho! Mwache akae karibu yako! Kula pamoja naye! Kama hauwezi kufanya hivyo, chukua kipande cha mkate chovya kwenye bakuli kisha mlishe na umpe chakula. Mwenyezi Mungum Mtukufu amewateua kama watumishi na watumwa wenu. Kama angetaka angeweza pia kuwafanya nyie muwe watumishi wao!"[133]

Kwa kuwa walikuwa wanaogopa kukiuka haki za binadamu, maswahaba wengi waliwaachia huru watumwa wao. Kitendo hicho kinaonesha ni jinsi Uislamu ulivyowapa wanadamu hadhi isiyokuwa na kifani.

Muamala wa Mtume wa Rehma (s.a.w) kwa Wanawake

Katika zama za kabla ya Uislamu, wanawake walikuwa wakitendewa katika namna ambayo hadhi ya uanauke wao ilikiukwa na kuumizwa. Masuria walionekana kama chombo cha starehe na walitendewa katika namna inayoshusha utu wao. Kwa kuhofia kuwa watoto wa kike watakuwa malaya,

133. Kwa hadith nyingine sawa na hiyo, tazama: Bukhârî, Îmân 22; Muslim, Aymân 38; Abû Dâwûd, Adab 124; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, VIII, 36.

watoto wa kike walizikwa hai na wazazi wao bila huruma yoyote. Kutokana na kuwa na mioyo migumu, ulifanywa uhalifu zaidi ya huo ili kujikinga na majanga; yote hayo yalitokana na ujinga. Mwenyezi Mungu amielezea tabia hiyo kama ifuatavyo:

"Na mmoja wao akibashiriwa kwa msichana, uso wake unasawijika, naye kajaa chuki. Anajificha asionekane na watu kwa ubaya wa aliyobashiriwa!Je, akae naye juu ya fedheha hiyo au amfukie udongoni?Tazama uovu wa wanavyo hukumu." (Qur'an, Nahl, 16:58-59)

Kwa amri ya Mtume Muhammad, haki za wanawake zilianzishwa. Wakawa mifano ya staha na heshima katikajamii. Asasi ya umama ilipata heshima. Kutokana na hadith inayosema "Pepo iko chini ya nyayo za akina mama,"[134] wanawake wakapata hadhi waliyostahili kuwa nayo kwa heshima ya Mtume Muhammad.

Mfano ufuatao wa hurumailiyooneshwa na Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa wanawake ni mzuri sana. "Wakati wa safari moja, mtumwa anaitwaye Anjasha alifanya ngamia akimbie kwa kuimba.[135] Mtume Muhammad, akifikiria jinsi mwili laini wa mwanamke yule juu ya ngamia unavyoweza kuumia, akamwambia : Ewe Anjasha! Angalia kioo! Angalia kioo!"[136]

Mtume Muhammad (s.a.w) katika hadith nyingine anas-

134. Nasâî, Jihâd 6; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 429; Ibn Mâjah,] ihâd 12; al-Qudâî, Musnad al-Shihâb, 1,102; al-Daylami, al-Firdaws, II, 116.
135. Ngamia hupenda sauti na nyimbo nzuri. Waendesha ngamia huwaimbia ili kuwafanya wakimbie haraka.
136. Bukhârî Adab 95; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 117.

ema; "Katika ulimwengu huu, wanawake na manukato yenye harufu nzuri ndivyo vinavyonifurahisha, na swala imefanywa kuwa nuru macho yangu."[137] Wanawake na manukato yenye harufu nzuri ni neema kubwa za Mwenyezi Mungu katika ulimwengu huu.

Umuhimu wa mwanamke mwema katika nyumba yenye dini na yenye amani unajulikana wazi. Japokuwa ulimwengu wa leo umebadilika, kwa asili, mwanamke aliinda mali ya familia, aliiratibu nyumba, aliuhifadhi uzao na kulinda heshima ya familia. Kwa hakika, mama ndiye aliyeijaza familia kwa furaha. Hali ya furaha ilitegemea tabasamu lake. Wasiwasi wa watoto uliisha pale wanapotazamwa na mama kwa huruma na upole. Kuna mahali penye huruma kama moyo wa mama?

Mama zetu ni viumbe waliopewa kiwango kikubwa kabisa cha huruma kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Nguvu ya mwanawake huanza pindi anapokuwa mama mwema. Hadith isemayo"Pepo ipo chini ya nyayo za mama" hiyo ndio sifa ya juu kabisa ambayo Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwapa mama zetu.

Manukato mazuri huuhuisha moyo kwa uzuri wake. Hii ni furaha ambayo hata malaika wanaifurahia. Swala ni makutano kati ya mja na Mola wake. Swala ni *miiraj* ya moyo wa muumini.

Katika hadith nyingine, Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema; "Mbora miongoni mwenu ni yule anaeitendea vizuri familia yake."[138] Mtume (s.a.w) akasema pia, "Kitu chochote

137. Nasai, 'Ishratu'n-nisa 10; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 128,199.
138. Tirmidhî, Rada 11; Ibn Mâjah, Nikah 50; Dârimî, Nikah 55; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 472.

mtu atakachotumia kwa ajili yake, yeye na mkewe na watoto wake hulipwa na Mwenyezi Mungu kama sadaka."[139] Mtume (s.a.w) ameelezea katika mafunzo hayo hapo juu kuwa familia imara hupatikana tu kwa msingi ya upendo.

Muamala wa Mtume wa Rehma Kwa Wanyama

Watu wa zama za ujahili hawakuwa na huruma na wanyama. Walikata vipande vya nyama au mikia yao wakiwa hai. Waliandaa mapigano ya kikatili kati ya wanyama. Mtukufu Mtume (s.a.w) alisitisha mambo haya ya kikatili. Tamaduni hizi za mapigano ya kuku, mapigano ya ngamia na mapigano ya mafahali yameanzia katika zama za ujahili.

Siku moja, Mtukufu Mtume (s.a.w) alimwona farasi njiani aliyepigwa chapa usoni. Alihuzunika sana na kusema; "Adhabu ya Mwenyezi Mungu imfikie mtu aliyempiga chapa farasi huyu!"[140] Akashauri kuwa kuwapiga chapa wanyama kwa lengo la kuwawekea alama ifanyike sehemu ambayo hawawezi kuumia sana.

Siku moja alimuona ngamia aliyekonda sana. Alimwambia mmiliki wa yule ngamia; "Mwogope Mwenyezi Mungu kwa wanyama hawa wasiosema! Usiwaache na njaa!"[141]

Abdullah ibn Ja'far (r.a) anasema: "Siku moja, Mtume (s.a.w) alienda shambani kwa swahaba wake mmoja. Ngamia aliyekuwa shambani alipomuona Mtume (s.a.w)alipiga kite, na machozi yakaanza kumtoka. Mjumbe wa Mwenyezi

139. Ibn Mâjah, Ticârât 1; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 279; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, X, 242; Al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, VIII, 239.
140. Bukhârî, Zabâih 25.
141. Abû Dâwûd, Jihâd 47; Ibn Khuzaymah, al-Sahîh, IV, 143.

Mungu (s.a.w) alimsogelea yule ngamia na kumshika kichwani. Yule ngamia akaacha kupiga kite. Kisha Mtume (s.a.w) alikutana na mmiliki wa shamba na kumuuliza, 'humwogopi Mwenyezi Mungu aliyekupa ngamia huyu? Amenilalamikia kuwa huwa unampiga na kumtesa.'"

❀

Mtume (s.a.w) anaelezea tofauti kati ya hali ya huruma na ukatili kama ifuatavyo:

"Mwanamke mmoja mwenye dhambi alimwona mbwa jangwani akilamba mchanga kwa ulimi wake kwa sababu ya kiu. Alimhurumia na kuchota maji kwenye kisima kwa kutumia kiatu chake na kumpa yule mbwa. Mwenyezi Mungu alimsamehe madhambi yake kwa kitendo chake hicho. Mwanamke mwingine hakumjali paka wake alimtesa na njaa kwa muda mrefu. Hakumwacha hata ale wadudu ardhini. Mwishowe, yule paka alikufa kwa njaa. Mwanamke huyu akawa miongoni mwa watu wa motoni kwa sababu ya ukatili wake!"[142]

Mtume (s.a.w) aliibadili jamii iliyojaa ujinga na kuwa jamii iliyokuja kuwa sehemu ya Zama za Furaha (asr al-sa'adah). Watu ambao hapo mwanzo walikuwa wakiwatendea vibaya wenzao na kuwazika mabinti zao wakiwa hai walibadilika na kuwa watu wenye huruma mpaka kwa wanyama. Hii ni kwasababu Mtume (s.a.w) aliheshimu hata haki ya ndege wadogo.

Abdurrahman, mtoto wa Abdullah, anasimulia,

"Tulipokuwa safarini na Mtume (s.a.w), tulimwona

142. Bukhârî, Anbiyâ 54; Muslim, Salâm 151,154; Birr 133; Nasâî, Kusuf 14.

kwale na makinda yake wawili. Tuliyachukuwa yale makinda yule kwale akaanza kuzunguka juu ya vichwa vyetu. Mtume (s.a.w) alikuja haraka na kutuambia:"Nani kamchokoza huyu ndege kwa kuchukua makinda yake? Yarudisheni kwenye kiota chake!"[143]

Kuwinda kunaruhusiwa katika sheria ya kiislamu. Hata hivyo, Mtukufu Mtume (s.a.w) aliwaonya wawindaji kuwa wazingatie msimu wa wanyama wa kuzaliana kwa lengo la kutunza uwiano wa kiikolojia. Kwa sababu uwindaji wa hovyo na usiokuwa na utaratibu utawahuzunisha watoto kwa kupoteza mama zao au waweza kuwahuzunisha mama zao kwa kupoteza watoto wao.

Hadith hizi zinaangazia ukweli kuwa huruma ya muumini wa kweli inatakiwa kupanuka zaidi na kuwafikia hata kwa wanyama wa mwituni. Kwa hiyo, imeagizwa katika Uislamu kuwa hata wanyama hatari kama nyoka na nge wauwawe kwa pigo moja tu ili kuwaepushia maumivu ya muda mrefu. Je kuwa na huruma wakati wa kuwauwa wanyama hatari si mfano wa huruma isiyo na kifani?

Katika kuzidi kuwaasa waumini wawe na huruma kwa wanyama, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa hapendi wanyama walaaniwe. K wa mfano, akiwa njiani kuelekea Batnubuwat kwa shughuli za kijeshi, bwana mmoja wa *Kiansar* alimlaani ngamia kwa kutembea taratibu sana. Mtume (S. a. w) akamwambia ateremke kwenye ngamia kisha akamwambia, "Usiandamane nasi hata kidogo ukiwa na ngamia aliyelaaniwa! Msijilaani wenyewe, watoto wenu, au mali zenu!"[144]

143. Abû Dâwûd, Jihâd, 122; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 404; Hâkim, al-Mustadrak, IV, 267; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, IV, 261.

144. Muslim, Zuhd 74, Ibn Hibbân, al-Sahîh,XIII, 52.

Hadith hii inaonesha huruma yake isiyokuwa na mipaka katika Uislamu.[145] Bayezid-i Bistami, aliyejulikana kama "Sultani wa mawalii", alijawa na hisia na huruma sana kwa kutekeleza kanuni ya kuwapenda viumbe kwa ajili ya Muumba, kiasi kwamba aliyahisi maumivu yao moyoni mwake. Kisa kifuatacho kinaonesha hisia kubwa alizokuwa nazo:

Alipokuwa akisafiri, alipumzika chini ya mti na baada ya muda alinyanyuka na kuendelea na safari. Baada ya kuondoka aligundua kuwa sisimizi waliotoka pale alipokuwa amekaa walikuwa kwenye begi lake. Alirudi mahali alipokuwa amekaa na kuwarudisha wale sisimizi kwa sababu alichukia kupeleka mbali na makazi yao.

Hili linaonesha utekelezaji kwa vitendo yaliyofanywa na Mtukufu Mtume (s.a.w). Mafundisho ya Mtume (s.a.w) yamejaa maelezo yanayojumuisha maonyo na kutoa mwongozo kuhusu jambo hili. Anasema: "Aliyenyimwa huruma amenyimwa kheri zote."[146]

Sifa kubwa inayomtofautisha Muislamu na watu wengine ni huruma. Katika "basmalah", (Bismillahi'r-Rahmani'r-Rahim, ambayo ina maana kwa jina Mwenyezi Mungu,

145. Claude Farer aliandika kuhusu athari za maadili ya Kiislamu yanayoagiza kuwahurumia viumbe wote: "Unaweza kujua iwapo nyumba unayopita ni ya Muislamu au ya Mkristo kwa kuangalia tabia za mbwa na paka wa eneo hilo.
Ukiona mbwa na paka wanataka kucheza na kutaka kuwa karibu nawe, tambua kabisa kuwa nyumba hiyo ni ya Muislamu; ukiona wanakukimbia na kujilinda dhidi yako, tambua kuwa hiyo sio nyumba ya Muislamu." Taswira hii inayotolewa na mtalii wa Kikristo, ni taswira ya wazi ya kuwapenda, kuwahurumia na kuwafanyia upole viumbe kwa ajili ya Muumba.

146. Muslim, Birr 75; Abû Dâwûd, Adah 11; Ibn Mâjah, Adah 9; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 362; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 308.

mwingi wa Rehma, mwenye kurehemu) ambayo tunarudia kabla ya kufanya jambo lolote, Mwenyezi Mungu anatukumbusha kuwa yeye ni Mwenye Huruma zaidi. Huruma ni sifa kuu ya utu wa Muislamu wa kweli.

Katika tukio lifuatalo, Fudayl ibn Iyad, aliyekuwa miongoni mwa marafiki wakubwa wa Mwenyezi Mungu, alionesha mfano wa jinsi ambavyo Muislamu anatakiwa kuwa na hisia moyoni mwake.

Walimuona akilia na kumuuliza: "kwa nini unalia?" akajibu:

"Ninalia kwa sababu namsikitikia Muislamu aliyenitendea kosa! Huzuni inatokana na wasiwasi wangu kuwa ataenda motoni kwa sababu yangu."

Matukio haya ni ishara za wazi za tabia za ndani za moyo unaofuata mfano wa Mtume Muhammad (s.a.w). Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema, "Wahurumieni walio Ardhini ili mpate kuhurumiwa na walio Mbinguni!"[147]

Muamala wa Mtume wa Rehma kwa Yatima

Hadith moja inaelezea kuwa, "Nyumba bora ni ile ambayo ina yatima anayetendewa vizuri na nyumba mbaya ni ile ambayo ina yatima anayetendewa vibaya."[148] Ndani ya Qur'an Tukufu kuna aya nyingi zinazoelezea kuhusu kutendea wema yatima. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuamrisha kuwa makini na yatima.

147. Tirmidhî, Birr 16; al-Hâkim, al-Mustadrak, TV, 277; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ,lX, 41.
148. Ibn Mâjah, Adab 6; al-Kissî, Musnad Abd ibn Humayd, I, 427; Bukhârî, al-Ababul-murfad, I, 61.

"Basi yatima usimwonee!" (Qur'an, Dhuha, 93:9)

"Mwenye kukishika kichwa cha yatima atalipwa kwa kila nywele iliyoguswa na mkono wake."[149] Mtukufu Mtume alikuwa akitilia msisitizo mara kwa mara kuhusu umuhimu wa kutekeleza majukumu haya muhimu ya kijamii.

Imesimuliwa katika hadith nyingine, "Mimi na wale wanaowatendea wema watoto wao wa kike na wa kiume, tutakuwa pamoja Peponi."[150] Aliyasema hayo huku akiviweka pamoja vidole vyake viwili.

Siku moja Mtukufu Mtume (s.a.w) aliletewa malalamiko kuhusu mtu mmoja aliyekuwa mkali. Kama tiba, alimshauri mtu yule yafuatayo:

"Akishike kichwa cha yatima na kuwalisha masikini!"[151]

Kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa yatima, hali hiyo ilimpatia hadhi na heshima duniani na akhera. Mshairi, Mehmed Aslan, amelezea vizuri hisia za yatima fulani:

Mwenyezi Mungu ndiye Mmiliki wa yatima,
Kwa hiyo ni dhambi kumuumiza yatima.
Usifikiri kuwa yatima ni dhaifu;
Machozi ndiyo silaha yake!

149. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 250, 265; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, III, 285, al-Mu'jam al-Kabîr, VIII, 202; Ibn Abî 'Âsim, Kitab alzuhd, I, 21; Ibn al-Mubârak, Kitab al-zuhd, I, 229, 230.
150. Bukhârî, Adab 24; Tirmidhî, Birr 15; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 265.
151. Ahmad ibn Hanbal, II, 263, 387; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, IV, 60.

Wosia wa Mtume kuhusu Haki za Majirani

Mtume Muhammad (s.a.w) katika mafundisho yake aliagiza kuheshimu jirani. Katika hadith moja anasema, "Jibrili aliniusia sana kuhusu haki za jirani mpaka nikahisi kuwa jirani atanirithi nitakapokufa."[152]

Katika hadith nyingine, imeelezwa kuwa, "Jirani ambaye si Muislamu ana haki moja. Jirani ambaye ni Muislamu ana haki mbili. Jirani ambaye ni ndugu na ni Muislamu ana haki tatu."[153] Haki za jirani zinajumuisha kutokuchungulia madirishani mwao, kutokuwakera kwa harufu ya chakula au kuwafanyia jambo la kuwachukiza.

Abu Dharr al-Ghifari, ambaye alikuwa miongoni mwa maswahaba masikini, anasema, "Mtume aliniamuru niweke maji mengi kwenye chakula ili niweze kumgawia na jirani yangu."[154] Abu Dharr alikuwa miongoni mwa maswahaba mafakiri. Kwa kuwa hakuwa na chakula cha ziada, njia pekee ya kuongeza chakula chake ilikuwa ni kwa kuongeza maji. Hadith hii inaonesha kuwa hata masikini hana udhuru katika kuheshimu haki za majirani.

Hadith ifuatayo ni mfano mwingine wa jinsi maswahaba walivyoheshimu haki za majirani. Ibn Umar (r.a) anasimulia tukio lifuatalo. "Kulikuwa na kaya saba, zote zilikuwa masikini. Mtu mmoja aliileta familiamoja kichwa cha kondoo kama chakula. Mkuu wa kaya alifikiri kuwa jirani yake alikuwa mwenye shida zaidi hivyo akamtumia kichwa hicho.

152. Bukhari, Adah 28; Muslim, Birr 140; Abu Dawud, Adah 123; Ibn Majah, Adah 4; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 85,160, 259.

153. Abu Bakr al-Qurashi, Makarim al-akhlaq, I, 105; Hannad al-Kufi, al-Zuhd, II, 504; al-Bayhaqi, Shu'ab al-lman, VII, 84.

154. Ibn Majah, At'imah 58 ; al-Tabarani, al-Mu'jam al-Awsat, IV, 54.

Jirani wa pili alifikiri vile vile na kumpelekea jirani wa tatu. Majirani wengine wakafikiri hivyo hivyo na kukipeleka kile kichwa kwa jirani anayefuatia hadi mwisho kikarudi kwa mwenye nacho."[155]

❀

Huruma ya mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ilitanda mpaka kwa wale walifariki dunia. Mfano mzuri ni kuhusu wale waliofariki wakiwa hawajalipa madeni yao. Daima Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kabla ya kumswalia marehemu alikuwa akiuliza kama marehemu alikuwa na madeni. Kama marehemu ana madeni ambayo hayajalipwa, alihairisha swala ya maiti mpaka madeni hayo yanapolipwa.[156]

Kwa kuwa alikuwa Mtume wa Rehma na huruma, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akijishughulisha sana kuhusu kuzuia mtu asiingie kaburini akiwa na madeni.

Muamala wa Mtume kwa Wahalifu na Mateka wa Vita

Katika Uislamu huanza kutafutwa chanzo cha uhalifu fulani kisha juhudi kubwa hufanyika kumbadilisha mhalifu. Adhabu katika sheria ya kiislamu ni kama adhabu ya wazazi kwa watoto wao. Lengo la kumwadhibu mhalifu si kumtenga na jamii ila ni kumsaidia aweze kurudi katika jamii yake.

Bwana mmoja masikini aliyeitwa Abbad ibn Shurahbil aliiba tende shambani na kuziweka mfukoni mwake. Mmiliki wa shamba lile alimwona, akamkamata na kumpiga sana.

155. al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 526; Ibn Abî Shaybah, al-Musannaf, VII, 214; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, III, 259 (Tazama pia tafsiri ya aya ya 9 ya Sûrah al-Hashr).

156. Ibn Hibbân, al-Sahîh, XI, 192; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 29.

Abbad, aliyeumizwa sana kwa tukio lile, alienda kwa Mtukufu Mtume kulalamika. Mtume Muhammad (s.a.w) akamwita mmiliki wa lile shamba na kumwambia;

"Hujui kuwa mtu huyu hana elimu? Hajui alitendalo. Je ulimuusia kwanza? Vile vile alikuwa na njaa; ungempa chakula ."[157] Mmiliki wa shamba alifadhaika sana kwa kile alichokifanya na mwisho alimpa Abbad tende na magunia mawili ya ngano.

Maelezo haya hayana lengo la kuwatetea wezi, bali yanalengo la kutibu matatizo katika jamii yanayosababisha ongezeko la wezi. Mtukufu Mtume (s.a.w) alieleza wazi kuwa angemuadhibu binti yake kwa kumkata mkono kama angefanya wizi.

Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa mwenye huruma sana kwa mateka wa vita. Aliwaambia maswahaba zake:

"Hawa ni ndugu zenu, wapeni pia kile mnachokula na kunywa!"[158]

Muamala wa Mtume kwa Maadui na Wasiokuwa Waislamu.

Abu Basra al-Ghifari, alipokuwa anaelezea maisha yake kabla ya kuingia katika Uislamu, alisema, "Nilikuja Madina na mwenyeji wangu alikuwa Mtume (s.a.w). Jioni ile, nilikunywa maziwa ya mbuzi saba. Mtume (s.a.w) hakusema lolote kuhusiana na ukwaru wangu. Usiku ule alienda kulala na njaa bila hata kuonesha dalili za kukasirika. Niliposhuhudia

157. Nasâî, Adab al-qadâ 21: Abû Dâwûd, Jihâd 85.
158. Muslim, Aymân 36-38.

maadili haya ya hali ya juu, nilivutika sana na kuamua kuingia katika Uislamu..."

Kwa kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) aliletwa kama Rehma kwa ulimwengu, huruma na upole wake viliwaenea viumbe wote. Siku moja, aliambiwa aombe dua ya kuwalaani maadui. Akajibu kwa kusema, "Sijaletwa hapa ulimwengu kwa ajili ya laana; nimeletwa kama Mtume wa Rehma."[159]

Alipokwenda Taif, washirikina wajinga na watu wenye kiburi wa mji ule walimpiga mawe. Malaika mkuu Jibrili (a.s.) alimjia na kumuuliza, "Je nikutanishe milima hii miwili na kuwaangamiza watu wa Taif wanaoishi katikati yake?" Hakuridhishwa na ushauri huu na badala yake aliiombea dua njema jamii ile iliyompiga mawe: "Ewe mola wangu! Waongoze watu hawa! Ninakuomba uzao wa Kiislamu kutoka migongoni mwao."[160] Kutokana na dua hii, hatimaye watu wa Taif waliukubali Uislamu.

Msamaha wa Mtume (s.a.w)

Mwenyezi Mungu anapenda kusamehe. Ameahidi kuwasamehe wanadamu madhambi yao ikiwa watatubu kwa dhati. Katika Qur'an, amewaasa waja wake kusamehe kwa sababu yeye ni Mwingi wa kusamehe.

Sharti la kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu ni mtu husika kuhisi majuto, kutii maamrisho ya Mwenyezi Mungu, na kuepuka yale yote aliyoyakataza. Mifano bora ya msamaha inapatikana katika maisha ya Mtume (s.a.w). Alimsamehe Hindu, aliyekula ini la ami yake, Hamza katika Vita ya Uhud.

159. Muslim, Fadâil 126; Tirmidhî, Da'awat 118.
160. Bukhârî, Badul-khalq 7; Muslim, Jihâd 111; Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, IV, 405; Ibn Hibbân, al-Sahîh, XIV, 516.

Wakati wa kukombolewa kwa Makkah baada ya kusilimu, Hindu alimjia Mtukufu Mtume (s.a.w) na kumuuliza,

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, unanifahamu?"

Mtume Muhammad, miaka mitano baada ya Uhud, alionesha kuwa bado anamkumbuka pindi alipokuwa anashangilia baada ya Hamza kuuawa.

"Nitawezaje kusahau shangwe zile?"

Lakini alimsamehe kwa ajili ya *Kalima-i Tawhid*, aliyotamka pindi aliposilimu.

Kwa upande mwingine, Mtume Muhammad aliwaambia watu wa Makkah:

"Enyi, Maquraysh! Mnatarajia niwafanye nini?" Maqurayshi wakajibu,

"Tunategemea utatusamehe. Hakika wewe ni ndugu mwenye huruma na ukarimu. Pia wewe ni mwana wa ndugu mwenye huruma na ukarimu..."

Hapo, Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema,

"Ninawaambieni kama Nabii Yusufu (s.a.w) alivyowaambia nduguze: Leo hii, hamna lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu awasamehe. Mnaweza kwenda. Mko huru."[161]

Katika hotuba nyingine, alisema, "Leo ni siku ya Rehma. Leo ni siku ambayo Mwenyezi Mungu ameongeza nguvu ya Uislamu kwa Maqurayshi."

Adui mkubwa wa Uislamu ndani ya Makkah alikuwa

161. Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, VI, 382; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, IX, 118; al-Rabi' ibn Habîb, Musnad al Rabi', I, 170; Tahâwî, Shark Ma'ânî al-Âthâr, III, 325.

ni Abu Jahl, jina ambalo kilugha lina maana ya " baba wa ujinga." Mwanae Ikrima naye alikuwa adui mkubwa wa Uislamu. Ikrima alikimbilia Yemen wakati wa kukombolewa kwa Makkah. Mkewe alisilimu na baadaye alimpeleka mumewe kwa Mtume (s.a.w), aliyempokea kwa furaha na kumwambia:

"Ewe askari farasi mtoro! Karibu!" alimsamehe bila hata kumkumbusha maovu yake dhidi ya Waislamu.[162]

Habir ibn Aswad alikuwa na adui mwingine wa Uislamu. Wakati wa kuhama kwa binti wa Mtume Zainab kutoka Makkah kwenda Madina, alimsukuma kwa makusudi juu ya ngamia wake na binti wa Mtume akaanguka chini. Binti huyo wa Mtume alikuwa mjamzito kipindi kile. Aliumia sana na mwanae alikufa. Habir ibn Aswad alifanya maovu mengi kama hayo. Baada ya kukombolewa kwa Makkah alitaka kukimbia lakini alishindwa. Alikubali kusilimu na kujua mbele ya Mtume (s.a.w), akamsamehe.[163]

Mara kwa mara, MtukufuMtume (s.a.w) alikuwa akisema, "Ewe mola wangu! Wasamehe watu wangu kwani hawajui!"[164]

Bwana mmoja aitwaye Hamamah aliukubali kusilimu na kukata uhusiano na waabudu masanamu wa Makkah. Watu wa Makkah walishtushwa na uamuzi wake huo na kwenda kwa Mtume (s.a.w) kumwambia yule bwana aendelee kufanya nao biashara. Mtukufu Mtume (s.a.w) akamtumia Hamamah barua na kumtaka aendelee kufanya biashara na

162. Ibn Hajar al-'Asqalânî, al-Isâbah, IV, 538.
163. Ibn Hajar al-'Asqalânî, al-Isâbah, VI, 524-527; Ibn AbdilBarr, al-Isîi'ab, IV, 1536.
164. Ibn Mâjah, Manâsik 56; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 14.

Maquraysh. Japokuwa waabudu msanamu waliwazingira Waislamu kwa miaka mitatu na kuwatesa kwa njaa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliwasamehe. Wote walisilimu baada ya kupokea msamaha huo usio na mwisho.

Siku moja, kundi la watu nane lilikuja kumuua Mtume (s.a.w), lakini wote walikamatwa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), aliwasamehe wote pia.

Baada ya Khaybar kutekwa, mwanamke mmoja alimpa Mtume (s.a.w) chakula chenye sumu, kisha Mtume akagundua kuwa chakula kile kilikuwa na sumu. Mwanamke yule wa Kiyahudi alikiri kosa na Mtume akamsamehe.[165] Katika Qur'an, imeelezwa kuwa *"Shikamana na kusamehe, na amrisha mema na jitenge na majaahili."* (Qur'an, Araf, 7:199)

Mtukufu Mtume (s.a.w) alionesha ukamilifu wa tabia bora kwa wanadamu kwa ikhlasi, wepesi na muamala wake wa unyenyekevu kwa watu. Tabia na maadili yake hayakuwa ya kijuujuu au sadfa, bali yalitoka katika kina cha moyo wake.

Adiyy ibn Khatim anasimulia kisa kifuatacho:

Kuna wakati kabla sijasilimu, nilikwenda kumtembelea Mtume (s.a.w). Alinikaribisha nyumbani kwake. Tukiwa njiani, bibi kizee mmoja alimsimamisha. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisubiri mpaka mwanamke yule akamaliza kuzungumza kile alichokusudia kuzungumza. Nikasema moyoni, 'Wallah! Hakika mtu huyu si mfalme.'"

165. Bukhârî, Tibb 55; Muslim, Selam 43; Abû Dâwûd, Diyat 6; Ibn Mâjah,Tibb 45; Dârimî, Muqaddimah 11; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 451.

Kisha tukaendelea na safari mpaka nyumbani kwake. Akanipa mkeka uliotengenezwa kwa ngozi iliyojazwa majani makavu na kuniambia:

"Tafadhali kaa hapa." Nikamsisitizia:

"Tafadhali kaa wewe." Lakini alirudia: "Wewe kaa!"

Nilikaa kwenye ule mkeka kwa sababu sikupenda kumkatalia. Yeye akakaa chini. Mara hii, nikajisemea:

"Wallah! Mfalme hawezi kufanya hivi." Kisha tukaanza kuzungumza. Mtume Muhammad (s.a.w) akaniambia kuwa ninatoka katika dhehebu Rakusi[166], na kwamba, japo ilikuwa hairuhusiwi kwa mujibu wa imani yangu, nilikuwa nikikusanya moja ya nne ya pato la watu kama kodi. Nilishtuka sana. Papo hapo nikatambua kuwa alikuwa mtume kwa sababu alijua siri zilizojificha.[167]

Matukio yote haya yanaonesha kwa uwazi kabisa tabia za hali ya juu za Mtukufu Mtume (s.a.w). Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa mfano hai wa misingi ya kimaadili iliyoelezewa ndani ya Qur'an Tukufu. Alisamehe mabaya yote aliyotendewa. Lakini kwa uhalifu unaofanywa dhidi ya wanajamii alikuwa akichukua hatua za haki na uangalifu katika kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Usamah, swahaba mkubwa, alimtetea mwanamke mwizi kutoka familia ya mashuhuri. Usamah alimuomba Mtume amsamehe. Uso wa Mtume (s.a.w) ulibadilika kwa huzuni na kusema kwa sauti kubwa, "Hata binti yangu fatmah angeiba ningemkata mkono ili kumuadhibu."[168]

---

166. Dhehebu lililochanganya Ukristo na dini ya Sabii.
167. Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyahh, II, 580; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 379; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, VI, 360; Ibn Abî Shaybah, al-Musannaf, VII, 342.
168. Bukhârî, Hudûd 12; Muslim, Hudûd 9; Nasâî, Kat'us-sariq 12; Abû

Ukarimu wa Mtume (s.a.w)

Ibn Abbas, (r.a), anasimulia ukarimu wa Mtukkufu Mtume (s.a.w) kama ifuatavyo: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alikuwa mkarimu kuliko watu wote. Ukarimu wake uliongezeka zaidi katika mwezi wa Ramadhani. Kamwe hakusema "hapana" kwa yeyote aliyekuja kumuomba kitu!"[169]

Sifa mojawapo nzuri ya Mtume ilikuwa kutokumnyima mtu aliyekuja kumuomba kitu. Kama hakuwa na kitu alitabasamu ili kuleta na furaha. Tukio lifuatalo ni mfano mzuri kabisa:

Mtume (s.a.w) alijielezea kuwa yeye ni kama wakalai alietumwa kugawa na akasisitiza kuwa kila kitu kilikuwa kikitolewa na Mwenyezi Mungu. Siku moja, bwana mmoja alikuja kwa Mtume (s.a.w). Alipowaona mbuzi wa Mtume (s.a.w), akamwomba. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akampa mbuzi wote. Yule bwana aliporudi kwa watu wake aliwaambia: "Muhammad ni mkarimu asiyehofia hata umasikini!"[170]

Mtu mwingine alikuja kumtembelea Mtume (s.a.w) na kumwomba kitu. Mtume (s.a.w) hakuwa na cha kumpa. Akamshauri akakope na kumwahidi kuwa angelipa hilo deni kwa niaba yake.

Kama ilivyokuwa kwa babu yake, Nabii Ibrahimu (a.s), Mtukufu Mtume (s.a.w) asingekula pekee yake bila kuwa na

---

Dâwûd, Hudûd 4; Ibn Mâjah, Hudûd 6; Dârimî, Hudûd 5; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, VI, 162

169. Bukhârî, Bad' al-wahy 5-6; Nasâî, Siyâm 2; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 288, 363; Ibn Hibbân, al Sahîh, VIII, 225.

170. Muslim, Fadâil 57; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, III, 107, 259; Ibn Hibbân, al-Sahîh, X, 354; Ibn Khuzaymah, al-Sahîh, IV, 70.

wageni. Alikuwa akiwalipia madeni marehemu, au kuwaambia wengine wawalipie. Asingemswalia maiti kabla ya deni kulipwa. Alisema:

"Mtu mkarimu yu karibu na Mwenyezi Mungu, yu karibu na pepo na yu karibu watu; lakini yu mbali na moto. Na mtu bakhili yu mbali na Mwenyezi Mungu, yu mbali na pepo na yu mbali watu, lakini yu karibu na moto wa jahanamu."[171]

Katika hadith nyingine, ameripotiwa akisema, "Sifa mbili kamwe hazipatikani kwa Muumini wa kweli: ubakhili au utovu wa maadili."[172]

Ukarimu wa Maswahaba

Maswahaba walikuwa wakishindana katika kufuata njia ya Mtukufu Mtume (s.a.w). Mifano ifuatayo inaelezea ushindani huu wa kushindania mambo mema. Umar (r.a) anasimulia kisa kifuatacho.

"Siku moja, Mtume (s.a.w) alituamrisha kutoa sadaka. Wakati huo nilikuwa na kiasi cha pesa. Nikajua kuwa hiyo ni siku ya kumshinda Abu Bakr kwa mazuri, nikampa Mtume nusu ya pesa zangu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akaniuliza:

'Umeacha nini kwa ajili ya familia yako?'

Nikajibu:

'Kiasi kama hiki nilichokupa.'

171. Tirmidhî, Birr 40; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, III, 27; al-Ismaîlî, Mu'jam, III, 733; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, VII, 428, 429.
172. Tirmidhî, Birr 41; al-Tayalisi, al-Musnad, I, 293; al-Qudâî, Musnad al-Shihâb, I, 211.

Kisha, Abu Bakr alikuja, alileta pesa zake zote. Mtume (s.a.w) akamuuliza, "Ewe Abu Bakr! Umeacha nini kwa ajili ya familia yako?"

Akajibu kwa kusema, "Nimewaachia Mwenyezi Mungu na Mtume wake!"

Baada ya kusikia jibu lake, nikajisemea mwenyewe, "Kamwe sitaweza kumshinda Abu Bakr (r.a), katika jambo lolote."[173]

Abu Bakr na Umar (r.a) walimrithi kikamilifu Mtukufu Mtume (s.a.w) kwa kukataa kuelekea kwenye starehe na anasa za ulimwengu huu. Mfumo wa maisha yao uliwashangaza hata wafalme wa Iran na Rumi.

Hakuna shaka kuwa mwenendo wao ulioneshwa na maswahaba wengine pia. Kwa mfano, siku moja maskini alikuja kwa Ali (r.a) na kumwomba kitu. Ali aliwaambia wanawe Hasan na Husayn;

"Nendeni kwa mama yenu mkalete dirham sita tulizonazo."

Wakaenda nyumbani kuleta dirham zile, kisha wakampa baba yao naye akampa yule masikini, licha ya ukweli kwamba wakati huo, walikuwa na haja na hizo pesa. Fatima alikuwa amepanga kununua unga kwa pesa hizo.

Ali (r.a) alirudi nyumbani na mara baada ya kufika nyumbani kwake, bwana mmoja aliyetaka kumuuza ngamia wake alifika. Akasema anamuuza kwa dirham arobaini na ali-

173. Tirmidhî, Manâqib 16; Abû Dâwûd, Zakat 40; Dârimî, Zakât 26; Al-Hâkim, al-Mustadrak, 1,574; al-Bayhaqî, al-Sunan, TV, 180; al-Bazzâr, al-Musnad, I, 263, 394.

kuwa tayari kupokea pesa hiyo baadaye. Alimfunga ngamia bustanini na kisha akaondoka. Baadaye akaja mtu aliyetaka kumnunua ngamia yule kwa dirham mia mbili. Akalipa pesa hapo hapo na kumchukua yule ngamia.

Ali alianza kumlipa mmiliki wa ngamia na pesa iliyobaki akampa Fatima. Akamwambia,

"Hii ni ahadi ya Mwenyezi Mungu kupitia Mtume wake: 'Yeyote anaetenda mema, atalipwa mara kumi ya wema wake.' Tulitoa dirham kumi na Mwenyezi Mungu akatupa mara kumi zaidi."

Tukio lifuatalo, kama lilivyosimuliwa na Hudhayfa , ni tukio muhimu sana, kwa maana linaakisi uungwana wa maswahaba:

"Wakati wa vita ya Yarmuk, baada ya ukali wa mapigano kupungua, na majeruhi wa Kiislamu walikuwa wakifa kwa mchanga uliokuwa na joto kali, nilikusanya nguvu zangu na kuanza kumtafuta Harith, mtoto wa ami yangu. Baada ya kutembea katikati ya askari waliojeruhiwa vibaya, ambao walikuwa wakivuta pumzi yao ya mwisho, nilifanikiwa kumuona. Kwa bahati mbaya, Harith alikuwa katikati ya damu na alikuwa hawezi kuongea zaidi ya kupepesa macho. Nikamwonesha maji niliyokuwa nimebeba na kumuuliza, "unataka maji?"

Kinywa chake kilikuwa kimekauka sana kutokana na joto kali na nikahisi kuwa alihitaji maji. Alipepesa macho kama vile alitaka kuniambia maumivu aliyonayo. Nikafungua kiriba cha maji tayari kwa kumpa maji. Ghafla sauti ya Ikrima ikasikika kwa mbali. "maji!.. . maji!.. . tafadhali nipe japo tone la maji!"

Mtoto wa ami yangu aliposikia kilio hicho, akaniashiria kwa kwa macho nimpelekee Ikrimah.

Nikamkimbilia Ikrima, kwa kuwaruka mashahidi walikuwa wamelala kwenye mchanga uliokuwa na joto kali. Htimaye, nikamfikia Ikrima na kujiandaa kumpa maji. Ghafla, tukasikia sauti ya Iyash:

"Tafadhali nipeni hata tone moja la maji! Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, tone la maji tafadhali!"

Ikrima aliposikia vile aliaashiria maji yapelekwe kwa Iyash. Kama ilivyokuwa kwa Harith, naye alikataa kunywa. Nilipompata Iyash baadaya kumtafuta katikati ya majeruhi, nilisikia maneno yake ya mwisho. Alikuwa anasema,

"Ewe Mwenyezi Mungu! Hatukuacha kuutoa uhai wetu kwa ajili ya imani. Usitunyime daraja ya kifo cha kishahidi. Tusamehe makosa yetu!"

Alikuwa akikaribia kukata roho na kupata heshima ya kifo cha kishahidi. Aliyaona maji niliyokuwa nayo lakini alikuwa hana muda wa kuyanywa kwa sababu alikuwa anamalizia kutoa *Kalima-i Shadah* (ninakiri kuwa hapana mola apaswaye kuabadiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu; na pia ninakiri kuwa Muhammad ni mja wake na mjumbe wake).

Nilikimbia haraka kurudi kwa Ikrima na nilipojaribu kumpa maji, niligundua kuwa ameshafariki dunia. Nikakimbia hadi alipokuwa mpwa wangu, Harith. Kwa bahati mbaya, roho yake pia ilikuwa imesharudi kwa Mwenyezi Mungu. Kwa maumivu, chupa ya maji ilibaki ikiwa imejaa na hakuna aliyeyanywa kati ya mashahidi hao watatu."

Hudhayfa (r.a) alielezea hali aliyokuwa nayo kutokana na tukio hilo: "Nilikutana na matukio mengi sana katika maisha

yangu, lakini hakuna tukio lililoniathiri na kunisisimua kama tukio hili. Hali ya Uungwana, kupendana, kuhurumiana kwa hali ya juu kabisa, pamoja na kuwa hawakuwa ndugu wa damu, kuliniachia athari kubwa moyoni mwangu."[174]

Ikhlasi, Uaminifu na Uadilifu wa Mtume (s.a.w)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) aliwahurumia sana watu wasiojua lipi zuri na lipi baya, wasiojua maamrisho na makatazo ya Mwenyezi Mungu. Wakati fulani alipokuwa akienda nyumba kwa nyumba kufundisha dini ya MwenyeziMungu, alifungiwa milango. Lakini hakuwachukia kwa muamala huu bali alihuzunika sana kutokana na ujinga wao.

Aliwaambia watu hawa, "*Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu!*" (Qur'an, Sad, 38:86)

Hakuna yeyote aliyefikia kiwango cha uadilifu na uaminifu uliofanywa na Mtukufu Mtume (s.a.w). Alikuwa yatima. Alifundishwa biashara na ami yake, mzee Abu Talib. Uaminifu na uadilifu wake ulithibitishwa na kila mtu, jambo lililompatia cheo cha heshima cha al-Amin, mwaminifu. Kila mtu katika jamii, masikini kwa tajiri waliku wa wakimwita al-Amin.

Mwanamke Mtukufu wa Makka, Khadija, alipendezewa sana na uaminifu wake na kumuomba amuoe. Baadaye Bibi Khadija akawa msaidizi wake mkubwa. Ulipoteremshwa wahyi kwa mara ya kwanza, alimfariji Mtume (s.a.w). Daima alisimama kumtetea Mtume na kumfariji katika nyakati nugumu.

174. al-Hâkim, al-Mustadrak, III, 270; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, III, 259; al-Mizzi, Tahthib al-Kamâl, V, 301; Ibn al-Mubârak, al-Zuhd, 1,185; al-Qurtubî, Tafsir, XVIII, 28.

Mtukufu Mtume (s.a.w) aliishi maisha ya matakatifu na yaliyojaa unyoofu. Hata wale waliokataa kuupokea ujumbe wake kutokana na kiburi, walikiri sifa zake nzuri.

Tangu kuja kwa Uislamu karne kumi na nne zilizopita, hakuna aliyeacha kukiri uadilifu na usafi wa moyo wake. Hata Mayahudi, waliokuwa maadui wa Uislamu, walikuja kwake pindi walipohitilafiana. Rasullullah (s.a.w) alisuluhisha ugomvi wao. Aliwatendea haki na uadilifu hata Wakristo na Mayahudi.

Alimpa Ali wosia ufuatao kuhusu uadilifu:

"Usihukumu kabla hujasikiliza pande zote mbili! Unaweza kutoa uamuzi sahihi baada ya kusikiliza pande zote!"[175]

Mtukufu Mtume (s.a.w) alipoamua kuhama kutoka Makkah kwenda Madina, alimchagua Ali awe msaidizi wake wa kurudisha vito mbalimbali vya thamani alivyokabidhiwa kama amana.[176]

Hayaa za Mtume (s.a.w)

Kwa mujibu wa maelezo ya maswahaba zake, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na haya sana kuliko binti anayejifunika asionekane nawatu. Hakuwa anaongea kwa sauti ya juu. Alipopishana na watu, alifanya hivyo taratibu na kwa tabasamu. Aliposikia maneno yasiyomfurahisha, hakuongea lolote mbele za watu. Hata hivyo uso wake ulionesha hisia zake na mawazo yake. Hivyo, watu walikuwa makini sana kuhusu mienendo yao pindi wanapokuwa karibu naye.

175. Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 90.
176. Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyahh, I, 482; Ibn al-Kathir, al-Bidâyah van-nihâyah, II, 176.

Hakuwahi kucheka kwa sauti kwa sababu ya staha yake. Alichofanya zaidi ilikuwa kutabasamu. Katika hadith moja imeelezewa kuwa, "Hayaa ni katika imani. Watu wenye hayaa watakuwa peponi! Ukosefu wa hayaa unatokana na ususuavu (ugumu) wa moyo. Wale wenye ususuavu wa moyowatakwenda motoni."[177]

Hadith nyingine inasema:

"Imani na staha vinaenda pamoja. Kimoja kinapoondoka na kingine hupotea pia."[178]

"Mazungumzo machafu hayaleti chochote zaidi ya aibu! Staha na heshima vinapamba popote pale vinapokuwa."[179]

Staha ya kweli inapatikana kwa "kukumbuka mauti", ambayo ni nyenzo ya kuondoa mapenzi ya dunia moyoni. Daima Mtume Muhammad (s.a.w) aliwausia maswahaba zake wampe Mwenyezi Mungu heshima yake anayostahiki. Siku moja, walisema kuwa wanamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumstahi. Mtukufu Mtume (s.a.w) akasema kuwa staha ya kweli ijumuisha kuvisafisha viungo vyote dhidi ya matendo yaliyokatazwa na kuyakumbuka mauti. Pia akasema kuwa wale wanaotamani kwa dhati akhera ndio wanaoacha kuipenda dunia. Na hao ndio wenye kuonesha na staha ya kweli kwa Mwenyezi Mungu.[180]

---

177. Bukhârî, Îmân 16; Muslim, Îmân 57-59; Abû Dâwûd, Sunnah 14; Tirmidhî, Îmân 7; Nasâî, Îmân 16; Ibn Mâjah, Zuhd 17; Muwatta, Husn al-Khuluq 10; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 56,147.
178. al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, VIII, 174 and same book IV, 374; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, VI, 140.
179. Muslim, Birr 78; Abû Dâwûd, Jihâd 1.
180. Tirmidhî, Sifatu'l-Qiyamah 24; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 387; al-Hâkim, al-Mustadrak, IV, 359; Ibn Abî Shaybah, al-Musannaf, VII, 77; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, VII, 226.

Uungwana wa Mtume (s.a.w)

Mtume Muhammad (s.a.w) hakusikitishwa tu na shida za watu, bali pia alijitahidi bila kuchoka kuwasaidia. Sifa hii imetajwa katika Qur'an:

"Hakika amekwishakujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe, yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni, anakuhangaikieni sana. Kwa waumini ni mpole na mwenye huruma." (Qur'an, Tawba, 9:128) Katika aya hii, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtukuza mjumbe Wake kwa kumpa sifa Zake mbili, *Rauf* na *Rahim*, yaani mpole na mwenye huruma.

Daima alipigania mafanikio ya watu wake na alijawa furaha na utulivu alipowaona watu wake wakifanya juhudi kujiletea ustawi na maendeleo.

Hakuwa kama viongozi wengine wanaotamani tu kuona mazuri katika jamii zao. Kinyume chake, alikuwa kiongozi aliyefanya kwa vitendo kuusaidia umma wake kwa namna yeyote ile.

Siku moja, swahaba alipouliza jinsi ya kujua hali yake ikiwa nzuri au mbaya. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alimwambia yafuatayo:

"Mwenye lengo la kupata manufaa ya dunia kupitia ibada, ambayo kwa kawaida hufanywa ili kwa lengo la kupata malipo peponi, hatapata chochote akhera."[181]

Alikuwa Rehma iliyowazunguka, iliyowaenea wanadamu wote kwa matendo, maneno na maadili yake. Alikuwa

181. Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, V, 134; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 32; al-Hâkim, al-Mustadrak, IV, 346; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, V, 334.

muongozo wao. Alikutana na changamoto ngumu na majaribu makubwa kabisa kwa ajili ya dini ya kweli. Aliitekeleza kazi aliyopewa na Mwenyezi Mungu kwa njia bora kabisa. Alikuwa mwenye shauku na subira sana katika kufanya hivyo, kiasi kwamba, wakati mwingine, ufunuo uliteremka kumtahadharisha asijiumize katika kazi yake hiyo.

Kiwango cha wema kilichooneshwa na Mtukufu Mtume (s.a.w) katika kuhakikisha kuwa wanadamu wanapata furaha kimeelezwa ndani ya Qur'an Tukufu katika aya ifuatayo: *"Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini."* (Qur'an, Shu'ara, 26:3)

Aya hii inaonesha kuwa, kutokana na huruma aliyokuwa nayo, Mtukufu Mtume (s.a.w) alitaka watu wote wamuamini Mwenyezi Mungu na hivyo waokoke dhidi ya moto wa jahannamu.

Hamza aliposikia kuwa Abu Jahl amemshambulia Mtume (s.a.w), naye alimshambulia Abu Jahl, na kumwambia Mtukufu Mtume (s.a.w): "Ewe Muhammad! Furahi, kwani nimeshalipiza kisasi kwa Abu Jahl.. ." Mtukufu Mtume (s.a.w) akamwambia:

"Sina haja ya kulipiza kisasi ! Nitafurahi ikiwa utasilimu." Hamza aligundua kuwa jibu hilo lilikuwa na hekma, hivyo akaamua kusilimu.[182]

Mwenendo na tabia yake adhimu havikuhitaji manufaa binafsi, misukumo ya kimaada au hisia za kulipiza kisasi. Tukichunguza tutagundua kuwa Mtukufu Mtume (s.a.w) hakuwahi kulipiza kisasi katika maisha yake yote.[183]

182. Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyahh, I, 292; al-Hâkim, al-Mustadrak,III, 213; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, III, 139; Ibn al-Kathîr, al-Bidâyah wan-nihâyah, II, 32.

183. al-Bukhârî, Manâqib 23; Muslim, Fadâil 77; Abû Dâwûd, Adab 4;

Mtume Muhammad (s.a.w) hakuwahi kumkosoa swahaba yeyote hadharani pindi alipofanya kosa. Badala yake alipenda kusema, "Kwa nini ninawaona mkifanya jambo hili na hili?"[184]

Alijifanya yeye ndiye mkosaji bila kumlenga mkosaji mwenyewe. Mtume Muhammad (s.a.w), aliyechukua hatua za ziada ili kuhakikisha kuwa hawavunji moyo maswahaba zake, alikuwa mnara wa huruma. Sifa hizi zilionekana katika matendo na maneno yake. Kama mfano, tafakari kauli ifuatayo:

"Enyi waumini! Mwenyezi Mungu awalinde! Awape salama! Awape amani !Awasaidie! Awanyanyue !Awaongoze! Awaweke chini ya ulinzi wake! Awaepushe na bahati mbaya zote! Na awalindie dini yenu!"[185]

Mtume (s.a.w) aliletwa kama Rehma kwa ulimwengu. Alikuwa kielelezo cha Majina ya Mwenyezi Mungu ya *al-Ghafur* na *al-Rahman,* yaani Msamehevu, na Mwenye huruma. Aliwahurumia na kuwasikitikia wale waliuokataa ujumbe wake na kuwaombea wasiingie moto wa jahannamu. Hapo, tahadhari kutoka kwa Mwenyezi Mungu ikaja:

"Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya." (Qur'an, Kahf, 18:6)

Kwa upendo na furaha, Maswahaba zake walitawanyika

Muwatta, Husnul-khuluq 2; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, V, 130,223.

184. Bukhârî, Aymân 3; Ibn Hibbân, al-Sahîh, IV, 534; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 515.

185. al-Bazzâr, al-Musnad, V, 395; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, IV, 208; Abu Nu'aym al-Isbahânî, Hilyah ai-Awliyâ, IV, 168; al-Bağdâdî, Muwaddih, II, 147.

kwenda maeneo ya mbali kueneza maarifa, maadili, na sifa za kimaanawi walizozipata kwa kusuhubiana naye. Huu ni mfano wa kanuni ya "mpende kiumbe kwa ajili ya Muumba."

Kila mtu alipata fungu katika mwenendo na ukarimu wake wahali ya juu. Wema na huruma yake vilikuwa kama mto mkubwa uliotawanyika kila mahali na kuzimwagilia ardhi bila ubaguzi. Hakuna aliyeachwa na njaa, kiu, au upweke pindi akiwa karibu na Mtume.

Uwajibikaji Wake

Kutimiza ahadi ni njia ya kuokoka na moto wa jahannamu; pia ni sifa ya mitume na watu wema. Mtu anapokuwa na sifa hizi, maisha yake hupata uelekeo na nidhamu. Ni kipimo cha ubinadamu na kigezo cha kumhukumu mtu au taifa. Watu hupata furaha kwa kadiri wanavyoliheshimu na kulithamini jambo hilo.

Kwa kuishi kwenye kilele cha uwajibikaji, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa mfano bora kwa wanadamu kuhusu kuchunga na kutimiza ahadi. Kuhusu hili, bibi Aishah (r.a) anasimulia kisa kifuatacho:

"Siku moja bibi mmoja alikuja kumtembelea Mtume (s.a.w). Walikuwa na mazungumzo murua. Baada ya yule bibi kuondoka, nikamuuliza:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ulionesha umakini mkubwa kwa bibi yule! Ninataka kujua, ni nani?" Akasema, "ni mtu aliyependa sana kututembelea pindi Khadija alipokuwa hai. Tambua kuwa "uwajibikaji ni katika imani."[186]

186. al-Hâkim, al-Mustadrak, I, 62; al-Qudâî, Musnad al-Shihâb, II, 102;

Baada ya tukio la Hunayn kundi moja la watu lilikuja kwa Mtukufu Mtume (s.a.w). Walitaka kuachiwa huru kwa mateka wa vita. Moja kati yao akasema, "Ewe Muhammad! Kabila letu lina mama zako waliokunyonyesha na dada zako wa kambo!"

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akajibu kwa uwa jibikaji mkubwa, "Nimewaachia huru mateka wote waliokuwa chini ya himaya yangu na wale walio chini ya watoto wa Abdulmuttalib."

Ansari na Muajiruni walivyoona mwenendo huu mtukufu wakafanya kama alivyofanya, wakasema, "Nasi pia tumewaacha huru mateka wetu kwa ajili ya Mtume!"

Matokeo yake siku ile, maelfu ya mateka waliachiwa huru bila malipo wala fidia za vikomboleo.[187] Hii ilikuwa ishara ya uwajibikaji na shukrani kwa maziwa aliyopewa alipokuwa mtoto. Ni funzo bora kabisa kwa kila jamii duni. Kwa bahati mbaya, wanadamu husahau haraka fadhila ambazo athari yake hufutika katika kumbukumbu. Kwa kawaida, "UWAJIBIKAJI" limebaki kuwa neno tu katika kamusi.

Katika kipindi cha maradhi yake ya mwisho, Mtume (s.a.w) alikuja msikitini, kisha akapanda kwenye mimbari na kusema,

"Enyi Muajiruni! Watendeeni wema Ansari kwa sababu watu wanaongezeka, lakini idadi yao imeendelea kuwa ile ile: Walinipa hifadhi nilipokimbilia kwao. Watendeeni wema waliowema miongoni mwao, na muwasamehe wakosaji wao."

---

al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, VI, 517.

187. Bukhârî, al-Târikh al-sagîr, I, 5; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, V, 271; Abû Bakr al-Qurashî, Makârim al-akhlâq, 1, 116.

Uaminifu na uwajibikaji wa Mtume (s.a.w) aliouonesha kwa Ansari kwa mema waliyomtendea ni mfano bora kabisa wa kuigwa kwetu sote. Maisha yake yamejaa mifano mingi ya uaminifu na uwajibikaji. Kwa mfano, kabla ya Hijjah, wakati maadui walipokuwa wanapanga jinsi ya kumuuua, alikuwa anapanga jinsi ya kuwarejeshea amana zao.

Siku ya vita ya Uhud, aliagiza maswahaba wawili waliokuwa rafiki wema wazikwe katika kaburi moja na kisha kasema,

"Hii ni kwa sababu walikuwa marafiki waliopendana kwadhati na waaminifu katika ulimwengu huu."[188]

Maadili yasiyo kifani ya Mtukufu Mtume (s.a.w) yalionekana katika maisha na uhusiano wa maswahaba wake uliojaa upendo kati yao.

Siku ya Hudaybiya, Uthman alitumwa kwenda Makkah. Aliwaambia waabudu masanamu wa Makkah kuwa Mtume (s.a.w) alikuja tu kufanya Hijja kwenye Ka'bah Tukufu. Walikataa ombi lile, lakini wakamruhusu Uthman kufanya Hijjah. Lakini, Uthman (r.a) alikataa na kuwambia:

"Siwezi kufanya Hijja kama Mtume hajaruhusiwa kufanya hivyo!.. Siwezi kukaa mahali ambapo Mtume haruhusiwi..."

Wakati Uthman alipokuwa akiwaambia hayo, Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akipokea bay'ah kutoka kwa maswahaba wake. Kutokana na kuwa Uthman hakuwepo, kwa niaba yake, Mtume (s.a.w) aliweka mkono wake juu ya mwingine kisha akasema:

188. Ibn Abi Shaybah, al-Musannaf, VII, 367; Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, V, 299; Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyahh, II, 98.

"Ewe Mola wangu! Bay'ah hii ni ya Uthman! Hakika yeye amemtumikia Mjumbe Wako."[189]

Kimsingi, kuwa muumini wa kweli kunategemea jinsi ambavyo tunafuata mfano wa Mtume (s.a.w) .

❀

Mtume Muhammad (s.a.w) alikuwa msafara wa miujiza mingi. Aidha, aliwasaidia wanadamu kuimarisha utu na shakhsia zao. Sifa mpya zikaingizwa katika jamii, sifa ambazo zilileta jamala na heshima kwenye utamaduni na ustaarabu. Mabadiliko haya ya kimapinduzi katika tabia za wanadamu chini ya uongozi wa Mtume Muhammad (s.a.w) ni muujiza mkubwa sana.

Maneno mazuri, mwenendo safi na matendo ya mfano yalikuwa vyanzo vya ustawi huu wa ustaarabu. Msingi wa yote hayo ni matendo ya mfano, mazungumzo na desturi za Mtukufu Mtume (s.a.w).

Katika uwiano na mizania aliyoiweka baina ya pande mbili tofauti za maisha, hakuna dosari iliyobaki. Kwa mfano, aliweka mizania baina ya kufanya kazi kwa ajili ya dunia na kazi kwa ajili ya akhera. Vivyo hivyo, aliweka uwiano na mizania baina ya kujituma na kukidhi haja za matamanio. Haiwezekani kupata mtu katika historia yote ya mwanadamu anayeweza kufananishwa naye.

Katika historia ya jamii, unaweza kuwapata watu wakubwa wenye vipawa vikubwa katika nyanja tofauti za maisha. Kwa ujumla, vipawa vyao vinaishia kwenye eneo moja tu.

189 Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, IV, 324; Ibn Abdilbarr, al-Tamhîd, XII, 148; Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyah, II, 315; Ibnul-Kathîr, al-Bidayah wan-Nihayah, II, 169.

Lakini kwa upande wa Mtukufu Mtume (s.a.w) shakhsia yake imekusanya sifa kubwa katika nyanja zote za maisha.

Zifuatazo ni kanuni za kimaadili zilizowekwa na Mtume (s.a.w), zinadhihirisha kiwango cha hali ya juu cha maisha yake. Mtukufu Mtume (s.a.w) anasema,

"Mola wangu aliniusia mambo tisa:

1. Muogope Mwenyezi Mungu ukiwa peke yako au katika kundi la watu

2. Tenda haki hata kama ukiwa furaha au hasira.

3. Ishi maisha ya wastani hata kama ukiwa tajiri au masikini.

4. Dumisha uhusiano na nduguzo hata kama wao hawafanyi hivyo.

5. Mpe anayekunyima.

6. Msamehe anayekukosea.

7. Tafakari ukiwa kimya.

8. Mtaje Mwenyezi Mungu pindi unapozungumza.

9. Jifunze unapotazama."[190]

Maneno yafuatayo yaliandikwa katika upanga wake: "Msamehe aliyekukosea; wasaidie nduguzo hata kama hawakujali; mrudishie wema aliyekuumiza; sema kweli hata kama itakuwa kinyume na maslahi yako."[191]

190 Nasâî, Sahw 62; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 148; Ibn Abî Shaybah, al-Musannaf, VI, 45; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, V, 328.

191 Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 148; al-Hâkim, al-Mustadrak, II, 563; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Kabîr, XVII, 269; al-Bayhaqî, al-Sunan al-Kubrâ, X, 235.

Hudhayfa (r.a) anasimulia kuwa Mtume (s.a.w) alisema:

"Msiwe wanyonyaji. Mtu mmoja anasema, "Radiamali yangu itategemea wale walionizunguka. Kama watanitendea wema, nami nitawatendea wema pia; kama wakinitendea ubaya nami nitawatendea ubaya pia." Badala yake, mnatakiwa kufuata kanuni ifuatayo: Wakikutendea wema nawe pia watendee wema, wakikutendea ubaya usilipize ubaya ."[192]

Alisema pia, "Mwenyezi Mungu hapendi mambo matatu:

1. Umbea,

2. Ubadhirifu,

3. Kuuliza bila sababu."[193]

Wosia mwingine wa Mtume (s.a.w) ni, "Usimcheke ndugu yako anapokuwa katika tabu kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweza kumuepusha na matatizo hayo na kukupa wewe."[194]

Wale wanaoyasoma na kuyadurusu maisha ya Mtume Muhammad (s.a.w) wataona kuwa daima amekuwa Mtume wa Rehma na mwenye huruma. Hakumlaani mtu yeyote na aliwalea watu bora kabisa kutoka katika jamii iliyokuwa imejaa uonevu. Kwa mfano, alipopigwa mawe na watu wa Taif,

192 Tirmidhî, Birr 62; (riwaya nyingine ya hadith hii ilisimuliwa kutoka kwa Abdullah ibn Mas'ûd kama hadith mawkûf kwa mfano; al-Tabaranî, al-Mu'jam al-Kabîr, IX , 152; Abû Nu'aym al-Isbahânî, Hilyah al-Awliyâ, I,137; Ibn al-Jawzî, Safwatus-safwah, 1,421)

193 Bukhârî, Zakât 53; Muslim, Akdiyah 12, 13; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, II, 327, 360; Ibn Khuzaymah, al-Sahîh, I, 10.

194 Tirmidhî, Qiyâmah 54; al-Tabarânî, al-Mu'jam al-Awsat, IV, 111; al-Qudâî, Musnad al-Shihâb, II, 77; al-Bayhaqî, Shu'ab al-Îmân, V, 315.

alimwomba Mwenyezi Mungu awaongoze.[195] Alipoingia Ka'bah, baada ya miaka kumi ya mateso ya watu wa Makkah, alionesha unyenyekevu na uvumilivu. Hakuchukua hata ufunguo wa Ka'bah kutoka kwa Uthman ibn Talha, ambaye alikuwa nazo hizo funguo kwa muda mrefu. Alisema, "leo ni siku ya huruma na uaminifu."[196]

Ni Sultani pekee ambaye hajaacha urithi wa mali. Alisema, "Sisi mitume, haturithiwi; chochote tunachokiaacha ni sadaka kwa Waislamu wote."[197] Urithi pekee aliouachia Ummah wake ni mfano bora wa maisha yake.

195 Bukhriî, Bad al-khalq 7; Muslim, Jihâd 111; Nasâî, al-Sunan al-Kubrâ, IV, 405; Ibn Hibban, al-Sahîh, XIV, 516.

196 Ibn Hishâm, al-Sirah al-Nabawiyyahh, II, 412; Ibn Kathîr, al-Bidayah wan-Nihayah, II, 300.

197 Bukhârî, Khumus 1; Muslim, Jihâd 54; Abû Dâwûd, İmârah 19; Tirmidhî, Siyar 44; Nasâî, Fay' 9; Muwatta, Kalâm 27; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 4.



Hitimisho

"Ucha Mungu ni hurma." *(Hadith, Bukhari, Muslim, Tirmidhi)*

Katika viumbe wote, wanadamu pekee ndio waliopata sehemu katika sifa za Mwenyezi Mungu – isipokuwa uzima wa m ilele. Sambamba na hili, Mwenyezi Mungu Mtukufu, k wa hekma Zake, amewapa uwezo wa kutenda mema na ku tenda mabaya pia. Amewafanya wanadamu kuwa wema au waovu.

Kwa muktadha huu, lengo la dini ni kuyadhibiti matamanio ya kihayawani ya nafsi ya mwanadamu, na kumpeleka kwenye ukamilifu wa sifa njema. Lakini, ili kufanikisha lengo hili, mwanadamu anahitaji kielelezo kamili na mfano halisi wa kufuata. Moja ya sababu za kuletwa kwa mitume ni ili kukidhi hitajio hilo la mfano kamili tunaoweza kuufuata.

Mwenyezi Mungu Mtukufu, anasema katika Qur'an: *"Na hatukumtuma Mtume yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu..."* (Qur'an, Nisa, 4:64)

Sifa hii ilifikia kilele chake kwa ujio wa Mtume Muhammad (s.a.w). Qur'an Tukufu inatueleza:

"Hakika ny inyi mnao mfano mwema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." (Qur'an, Ahzab, 33:21)

Mtume pekee katika historia ambaye maisha yake yame-

andikwa kwa undani kabisa ni Mtume Muhammad (s.a.w). Maneno yake, matendo yake na hisia zake ambazo zimeendelea kuandikwa, zimechukua nafasi kubwa katika historia kama kurasa za heshima na umuhimu mkubwa. Maisha yake yatakuwa kama mfano kwa wanadamu mpaka siku ya mwisho. Aya ifuatayo inatoa ushuhuda juu ya jambo hili: *"Na hakika wewe una tabia Tukufu."* (Qur'an, Qalam, 68:4)

Shakhsia na maisha ya mjumbe wa Allah (s.a.w) ni kilele kisichomithilika cha tabia kamili ya mwanadamu inayohitajika ili ukamilifu wa kimaanawi wa mwanadamu. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba mtume kwa lengo hili kwa wote. Kwa sababu hiyo, alimfanya Mtume apitie maisha ya aina zote, kutoka kuwa yatima asiye na nguvu mpaka kuwa mtume na mkuu wa dola. Hekma ya kufanya hivyo ni ili watu wote, bila kujali hali ya maisha yao, waweze kupata mfano halisiwa mwenendo wanaoweza kuutumia katika maisha yao kwa kadiri ya kipawa na uwezo wao.

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), pamoja na shakhsia yake adhimu, aliteuliwa kuwa Mtume wa mwisho kwa wanadamu wote. Nabii Ibrahimu (a.s) alimuomba Mwenyezi Mungu kwamba Mtume Muhammad (s.a.w) atokane na uzao wake. Nabii Issa (a.s.) alitoa biashara njema za ujio wake, na mama yake Mtume, Aminah, alimuona ndotoni kabla ya kuzaliwa kwake. Alilelewa moja kwa moja chini ya uangalizi wa Mwenyezi Mungu, akapambwa kwa sifa njema za tabia bora kabisa na kuteuliwa kuwa muongozo kwa wanadamu mwenye kuaminiwa zaidi.

Hivyo, wanadamu wa leo hawana budi kufuata mfano wa Mtume Muhammad (s.a.w) ili wapate furaha ya hapa duniani na kesho Akhera. Hata kupata upendo wa Mwenyezi

Mungu kunategemea na ufuasi wetu kwa Mtume (s.a.w), kwa maana Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema katika aya ifuatayo:

"Sema, 'Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu Na Mwenyezi Mungu ni mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu. ' (Qur'an, Al-i Imran, 3:31)

Kutokana na ukweli huu, roho zenye bahati zinazofuata na kutekeleza kwa vitendo mfano wa maisha ya Mtukufu Mtume (s.a.w) ndizo zinazoweza kupata upendo adhimu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Faida ya kwanza na ya muhimu kabisa ya kumtii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), ni kupata hadhi ya kupendwa na Mwenyezi Mungu. Aidha, kufuata mfanobora wa maadili na mwenendo wa Mtume (s.a.w) hutufanya tupate sehemu ya ukamilifu wake. Kwa kuwa maadili na mwenendo wake ndio bora kabisa, wale wenye kumfuata na kumpenda nao watakuwa bora. Ulimwengu wa ndani wa wale wanaompenda hufikia daraja ya juu kabisa, juu zaidi ya malaika. Maisha ya familia zao huakisi maisha ya Peponi. Jamii inayofuata mfano wa Mtukufu Mtume hupata amani na utulivu kwa kupuliziwa na upepo mwanana kutoka katika Zama za Furaha *(asr al-sa'adah)*. Huonja ladha ya furaha sahihi ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu katika ibada zao.

Kama kila mmoja, masikini au tajiri, kiongozi au raia, mtawala au mtawaliwa, mwenye nguvu au mnyonge, wangeishi kama waja wa Mwenyezi Mungu kwa kutekeleza maamrisho Yake, hili lingeleta uwiano wa kipekee katika jamii.

Kwa mfano, wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alipopewa jukumu la kuwaongoza wanadamu, watu wengi waliokuwa wakiishi maisha yaliyokosa maadali na ya aibu walibadilika na kuwa watu wema na wa kipekee kupitia mafunzo na malezi yao mapya. Hivyo, zama mbaya zikaisha na zama mpya zenye wema zikaanza. Watumwa walipata heshima na hadhi kama wanadamu na watawala wengi wakawa waadilifu na wema kutokana na kujifunza jinsi ya kuwa waja wa Mwenyezi Mungu. Maneno ya Najashi, mfalme Mkristo wa nchi ya Abyssinia, ni muhimu sana:

"Ninakiri kuwa Muhammad ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ndiye ambaye ujio wake ulielezewa hapo kabla na Issa (a.s). Nisingekuwa na majukumu niliyo nayo sasa kwa watu wangu ningeenda kumbebea viatu."[198]

Watu walipoona furaha na wokovu katika maisha ya duniani na Akhera, walimkimbilia kama mto unavyokimbilia baharini. Hii ilikuwa zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama ilivyoelezewa kwenye Aya ifuatayo ya Qur'an Tukufu:

"Itakapo kuja nusura ya Mwenyezi Mungu na ushindi. Na ukaona watu wanaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu kwa makundi, Zitakase sifa za mola wako mlezi na umwombe msamaha, hakika yeye ndiye anayepokea toba." (Qur'an, Nasr, 110:1-3)

Wale walioifuata njia yake waliishi maisha yenye unyoofu, staha, amani na Baraka, hata pale walipokabiliwa na changamoto na shida mbalimbali. Wakawa kama mawaridi yanayomea katika vichaka vya miiba. Furaha yao itaongezeka zaidi huko Akhera. Hii ni kwa sababu, huko kutakuwa na

198. Abû Dâwûd, Janâiz 62; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, I, 461; Abu 'Uthman al-Khorasânî, Kitâb al-Sunan, II, 228.

uombezi mkubwa *(Shafa'ah'Udhmaa)* atakaoufanya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kuwaombea wakosefu kutoka katika umma wake na hata wakosefu kutoka katika wafuasi wa mitume wa zamani. Hadith ifuatayo inaelezea jinsi tukio hili litakavyotokea :

"Nitakuwa wa kwanza kufufuliwa miongoni mwa watu. Wanadamu watakapokuwa mbele ya Mwenyezi Mungu, nitazungumza kwa niaba yao. Watakapokuwa hawana matumaini juu ya msamaha na Rehma za Mwenyezi Mungu, nitawapa habari njema. Nitabeba bendera ya Utukufu *(liwa al-hamd)*. Mimi ndiye mbarikiwa nitakayezungumza na Mwenyezi Mungu, lakini siyaelezi haya kwa kujifaharisha."[199]

Mtume wa Rehma atawaombe wakosefu siku ya hukumu na uombezi wake utakubaliwa na Mwenyezi Mungu. Aya ifuatayo katika Qur'an inaonesha kuwa uombezi wake wa kuwaombea waumini utakubaliwa na Mwenyezi Mungu:

"Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangelikujia, wakamwomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu." (Qur"an, Nisa, 4:64)

Aya hii ni maneno ya Mwenyezi Mungu yaliyobeba ahadi na habari njema kuwa uombezi wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kwa ajili ya umma wake utakubaliwa na Mwenyezi Mungu.

Ifuatayo ni habari njema nyingine kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) :

199. Tirmidhî, Manâqib 1; Ibn Mace, Zuhd 37; Dârimî, Muqaddimah 8; Ahmad b. Hanbal, al-Musnad, I, 281; al-Hâkim, al-Mustadrak, I, 83; Ibn Hibbân, al-Sahîh, al-Sahîh, XIV, 398.

"Siku ya hukumu, wanadamu wote watakuwa na hofu. Watamwendea Adamu (a.s) kuomba msaada na kumwambia,

'Tafadhali tuombee kwa Mwenyezi Mungu!'

Atawaambia:

'Sina daraja ya kuwaombea; nendeni kwa Ibrahimu! Hakika yeye ni rafiki wa karibu wa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma *(Khalil al-Rahman)*.'

Watamwendea Ibrahimu (a.s) kumuomba awaombee, lakini atawajibu:

'Sina daraja ya kuwaombea, nendeni kwa Musa! Hakika yeye ndiye aliyekuwa akiongea na Mwenyezi Mungu.'

Watakapoenda kwa Musa (a.s.) kumuomba awaombee, atawaambia:

'Sina daraja ya kuwaombea! Nendeni kwa Issah (a.s.). Hakika yeye ndiye Neno na Roho kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Hatimaye wataenda kwa Issah (a.s), lakini atawaambia:

'Sina daraja ya kuwaombea! Nendeni kwa Muhammad (s.a.w) .'

Mwishowe watakuja kwangu na nitawaambia:

'Ndiyo, daraja hii nimepewa mimi.'

Kisha nitaomba ruhusa kwenda mbele ya Mola wangu. Ruhusa hii itakubaliwa. Hapo, nitafunuliwa maneno ya kuhimidi, ambayo siyajui kwa sasa. Nitamhimidi Mola wangu kwa maneno hayo na kisha nitasujudu mbele yake. Hapo, Mwenyezi Mungu ataniambia:

'Ewe Muhammad! Inua kichwa chako! Sema! Utasikilizwa. Uliza! Utajibiwa! Omba na uombezi wako utakubaliwa!'

Nitasema,

'Ewe Mola wangu! Ninauombea Ummah wangu, Ninauombea Ummah wangu!'

Mwenyezi Mungu Mtukufu ataniambia,

'Ewe Muhammad! Nenda kawalete wale wenye imani ndogo moyoni mwao kiasi cha punje ya shayiri.'

Nitaenda kufanya kama nilivyoagizwa. Kisha, nitarudia kusema maneno yale yale ya kuhimidi na kisha nitasujudu. Nitaambiwa tena.

'Ewe Muhammad! Inua kichwa chako! Sema! Utasikilizwa. Uliza! Utajibiwa! Omba! Uombezi wako utakubaliwa.'

Nitasema tena,

'Ewe Mola wangu! Ninauombea Ummah wangu! Ninauombea Ummah wangu!'

Mwenyezi Mungu ataniambia:

'Nenda kawalete wale wenye imani ndogo nyoyoni mwao kiasi cha chembe au mbegu ya mharadali!'

Nitaenda kufanya kama nilivyoagizwa. Kisha nitarudi tena. Kwa kutumia maneno yale yale ya kuhimidi, nitamhimidi Mola wangu na kusujudu. Mwenyezi Mungu ataniambia:

'Ewe Muhammad! Inua kichwa chako! Sema! Utasikilizwa.Uliza! Utajibiwa! Omba, uombezi wako utakubaliwa.'

Nitasema,

'Ewe Mola wangu! Ninauombea Ummah wangu, Ninauombea Ummah wangu!'

Mwenyezi Mungu Mtukufu, ataniambia,

'Nenda kawalete wale ambao wana imani ndogo kuliko mbegu ya mharadali!'

Nitaendelea kufanya kama ninavyoagizwa na nitarudi kwa mara ya nne. Kwa kutumia maneno yale yale ya kuhimidi, nitamhimidi Mola wangu na kusujudu. Mwenyezi Mungu ataniambia:

'Ewe Muhammad! Inua kichwa chako! Sema! Utasikilizwa. Uliza! Utajibiwa! Omba, uombezi wako utakubaliwa.'

Mara hii nitamwambia:

'Ewe Mola wangu! Ninawaombea wale wote waliotamka 'La ilaha illallah' (hapana Mola apaswaye kuabudiwa ila Mwenyezi Mungu!)

Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema:

'Ninaapa kwa uwezo wangu, Kwa Utukufu wangu, kwa Ulwa na Ukuu wangu ! Nitawaokoa wale wote waliotamka 'La ilaha illallah!'''[200]

Ili kupata baraka hizi yatupasa kuepuka tamaa na matamanio ya kihayawani kwa kuingiza vitendoni mfano bora wa maisha ya Mtume Muhammad (s.a.a.w).

Imesimuliwa kuwa kulikuwa na bwana mmoja ambaye alikuwa Muislamu lakini hakuwa akifuata mfano wa Mtukufu Mtume (s.a.w). Siku moja alimuona Mtukufu Mtume (s.a.w) ndotoni, lakini Mtume (s.a.w) hakuonesha kuwa na shauku naye. Yule bwana alifadhaika na kumuuliza:

200. Bukhârî, Tawhîd 36; Muslim, Îmân 322; Tirmidhî, Qiyâmah 11.

"Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Hujafurahishwa nami?"

"Hapana!"alijibu.

"Lakini mbona huoneshi kunijali?"

"Kwa sababu sikujui!"

"Hilo linawezekanaje Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu? Mimi ni miongoni mwa Ummah wako. Nimesikia kutoka kwa wanazuoni kuwa unamtambua kila mmoja katika ummah wako kama mama anavyomtambua mwanae."

"Ndio, hilo ni kweli. Hata hivyo, sioni alama yoyote kwako kutoka katika mfano wangu (yaani *sunnah*). Vile vile, hujanitakia rehma (yaani *salawat*). Unatakiwa ujue kuwa namtambua mtu katika Ummah wangu ikiwa anafuata *sunnah* zangu."

Yule bwana aliamka akiwa na huzuni sana na kutubu dhambi zake. Akafuata *sunnah* za Mtume (s.a.w) katika maisha yake na kumtakia rehma Mtukufu Mtume (s.a.w). Usiku mmoj, alimwona tena Mtume (s.a.w) ndotoni. Mtume (s.a.w) akamwambia

"Sasa nimekutambua na nitakuwa tayari kukuombea."

Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa na tabia ya kipekee, inayostahili kupendwa katika nyanja zake zote. Yeye ndiye mwanadamu mwema na mzuri kuwahi kuishi ardhini. Yeye ndiye mtu mwenye huruma zaidi kuwahi kuwalilia wanadamu. Yeye ndiye kiongozi na mwalimu pekee wa kweli. Yeye ndiye aliyeibadili mioyo migumu ya watu waliokuwa hata wakidiriki kuwazika watoto wao wakiwa hai na kuwafanya kuwa watu wenye huruma na nyoyo laini. Aliwafundi-

sha kitabu kitukufu na kuwapa hekma. Kushikamana naye na kumpenda kwa shauku isiyokuwa na mipaka ni ishara ya ukamilifu wa imani. Kilele cha upendo huo kinaoneshwa katika hadith ifuatayo: "Haitakamilika imani ya mmoja wenu mpaka anipende zaidi ya wazazi wake, zaidi ya watoto wake na zaidi ya mwanadamu yeyote yule."[201]

Hadith hii ni onyo na ukumbusho kuwa mtu hawezi kupata ukamilifu wa imani ila tu kwa kumpenda kikamilifu Mtukufu Mtume (s.a.w). Wale wasiokuwa na upendo huu hufungiwa milango ya ustawi na maarifa ya kimaanawi na kiroho. Mbegu ya upendo wa Mwenyezi Mungu haiwezi kumea isipokuwa katika udongo wenye rutuba ya upendo wa kumpenda Mtume. Yeye ni chemchemi ya baraka zitokazo kwa Mungu zinazoustawisha na kuurutubisha moyo. Moyo unaompenda yeye ukilinganisha na moyo usiompenda ni kama kipande cha dhahabu kilicho katika miamba michafu.

Mwenzi unaoakisi mwanga kutoka juani, ni ishara ya uwepo wa jua. Vivyo hivyo, mawalii waliomulikwa kwa nuru ya Mtume Muhammad (s.a.w) ni mashahidi wake. Kwa sababu hiyo, mwenye kutamka maneno yafuatayo kwa upendo kutoka moyoni, huhisi nuru kutoka kwa Mwenyezi Mungu ndani ya roho yake:

Ashhadu an la ilaha ill , Wa ashhadu anna Muhammadan Abduhu wa Rasuluhu.

Yaani: Ninakiri kuwa hapana Mola apaswaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na Ninakiri kuwa Muhammad ni mja na ni Mjumbe wake.

Wakati mwingine, shauku na upendo wa kimaanawi

201. Bukhari, Îmân 8; Muslim, Îmân 70; Nasâî, Îmân 19.

huwa kubwa kiasi kwamba roho huhisi furaha ya ladha ya imani isiyoelezeka. Kisa cha Bilal wa Abyssinia (r.a) kimejaa mafunzo na mazingatio mengi.

Bilal alikuwa mpweke kwa sababu hakuwa na mtu wa kumsaidia; hakuwa na rafiki wa kushirikiana huzuni yake. Alikuwa ni mtumwa wa kawaida. Lakini, siku moja alipata hadhi na heshima ya imani. Baada ya hapo, imani yake na jitihada zake za kuikamilisha imani yake zikawa mfano bora kwa vizazi vijavyo vya waumini.

Alikutana na Mtume (s.a.w) na kuingia katika bustani ya upendo wake. Ilikuwa kama vile amekuwa sehemu ya Mtume. Lakini mmiliki wake aliyeondoshwa katika nuru ya muongozo, alimfungia kwenye mchanga wa moto na kumtesa sana. Alimcharaza bakora kwenye mwili wake uliokuwa bila nguo. Ngozi yake ilivuja damu. Mkusanyiko wa watu wajinga waliomzunguka walipiga kelele,

"Wewe mtumwa mchafu! Rudi katika imani yetu ujiokoe!"

Lakini, Bilali aliunguruma kama simba aliyejeruhiwa, akiwa amelala kwenye bahari ya mchanga wa moto na huku akisema kwa nguvu zake zote: "Mungu mmoja, Mungu mmoja."

Maneno haya yaliwaongezea hasira na kuanza kumpiga zaidi na zaidi… Hiyo haikutosha kuwatuliza. Hivyo, walimfunga kamba shingoni mwake na kumburuza. Licha ya haya, Bilal alitaka kimbilio katika upendo wa MtukufuMtume (s.a.w). Ilikuwa kana kwamba hakuhisi kilichokuwa kikimtokea, kwa maana moyo wake ulikuwa umejaa upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Moyo wake ulikuwa na furaha, ingawa katika ulimwengu wa nje

alikuwa katika hali ya maumivu. Hakuwa na hata kibanda cha kulala.

Hivyo, upendo wa Bilal kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) ulimnyanyua kutoka katika utumwa hadi kuwa sultani wan yoyo za waumini. Akawa muaddhin (mtoa adhana) wa Mtume (s.a.w) aliyewaita watu kwenye swala mara tano kwa siku. Alimpenda sana Mtume (s.a.w) kiasi ambacho wakati akivuta pumzi yake ya mwisho ya uhai wake alikuwa akisema:

"Furahini! Furahini! Ninarudi kwa Mtume !"[202]

Haya ndiyo yaliyokuwa maneno yake ya mwisho kabla ya kuelekea katika ulimwengu mwingine.

Kwa hiyo, kama hadith isemavyo "mtu huwa pamoja na ampendaye",[203] kanuni yetu katika safari yetu kuelekea kwenye uzima wa milele ni kufuata aya isemayo:

"Na anacho kupeni Mtume chukeni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." (Qur'an, Hashr, 59:7)

Ewe Mwenyezi Mungu! Ifanye kazi hii dahalili, ambayo ina ukomo wa ufasaha, iwe chanzo cha rehma na msamaha wako na utupe Baraka ya ukweli ulioletwa na Mtume Wako Muhammad (s.a.w) kwa wanadamu. Tupe Baraka ya kumpenda Mtume Wako wa mwisho (s.a.w). Tupe Baraka ya kupata uombezi wake.

❀

202. Ibn Abdilbarr, al-Istî'âb, 1,178.
203. Bukhârî, Adab 96; Muslim, Birr 165; Tirmidhî, Zuhd 50; Dârimî, Riqâq 71; Ahmad ibn Hanbal, al-Musnad, IV, 395; Ibn Hibbân, al-Sahîh, II, 316; al-Humaydî, al-Musnad, II, 389.

Tunatambua kuwa maelezo yetu kuhusu Mtu huyu ambaye ni kilele ambacho binadamu wanatakiwa kukifikia hayatoshi kabisa kuielezea hakika yake na dhati yake. Tunahisi tabu hata kudai kuwa tumemtambulisha Mtume ipasavyo. Maneno yetu yanawakilisha tu udhaifu wetu wa kumuelezea kikamilifu. Tulicholenga kwa kazi hii si kingine bali kupata heshima ya kutimiza dhamira hiyo na kuwa tumejaribu pia. Yeye ni ulimwengu usio na mwisho ambao mtu huweza kupenya kwa kadri tu ya upendo na uaminifu alionao kwake.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atubariki kwa kuzifungua mbawa zetu katika anga za ulimwengu huu wa kiroho.

Amiin



Bibliografia

Abû Dâwûd, Sulaymân ibn Ash'ath al-Sijistânî, *al-Sunan,* Istanbul 1413/1992, juzuu IV.

Abû Nu'aym al-Isbahâni, Ahmad ibn Abdillah, *Hilyah al-Awliyâ*, Dâr al-Kitâb al-Arabî, Beirut 1405, juzuu X.

Abû Ya'lâ, Ahmad ibn 'Ali ibn al-Muthannâ al-Mawsilî al-Tamîmî, *al-Musnad,* ed. Husayn Salîm Asad, Dâr al-Ma'mûn li al-Turath, Damascus, 1404/1984, vol. XIII.

Ahmad ibn Hanbal al-Shaybânî, *al-Musnad,* Istanbul, 1413/1992.

Ahmad ibn Hanbal al-Shaybânî, *Kitâb al-Zuhd*, ed. Dr. Muhammad Jalâl Sharaf, Dâr al-Fikr al-Jâmi'î, Cairo, 1984.

Ahmad ibn Hanbal, *al-Musnad,* Muassasah Qurtubah, Egypt, juzuu VI.

Asyalı, Arif Nihat, *Dualar ve Aminler*, Istanbul, 1973

al-Bayhaqî, Abû Bakr Muhammad ibn al-Husayn ibn 'Ali ibn Mussa, *al-Sunan al-Kubrâ,* ed. Muhammad 'Abdulkâdir 'Atâ, Maktabah Dâr al-Bâz, Makkah al-Mukarramah 1414/1994, juzuu X.

al-Bayhaqî, Abû Bakr Muhammad ibn al-Husayn ibn 'Ali ibn Mussa, *Kitâb al-Zuhd al-Kabîr*, ed. al-Shaykh 'Âmir Ahmad Haydar, Muassasah al-Kutub al-Thaqâfiyyah, Beirut, 1996.

al-Bayhaqî, Abû Bakr Muhammad ibn al-Husayn, *Shu'ab alÎmân*, ed. Muhammad al-Saîd Basyûnî Zaglûl, Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah, Beirut 1410, juzuu VIII.

al-Bazzâr, Abû Bakr Ahmad ibn 'Amr ibn Abdilhâlık, *Musnad al-Bazzâr,* ed. Dr. MahfuzurRahmân Zaynullah, Muassasah Ulûm al-Qur'an & Maktabah al-Ulûm wa'l-Hikam, Beirutal-Madînah 1409, juzuu X.

al-Bukhârî, Abû Abdillah Muhammad ibn Ibrahîm ibn Ismâ'îl al-Ju'fî, *al-Târîkh al-Sagîr,* ed. Mahmûd Abraham Zâyed, Dâr al-Wa'y & Maktabah Dâr al-Turath, Aleppo-Cairo, 1397/1977, juzuu II.

al-Bukhârî, Abû Abdillah Muhammad ibn Ibrahîm ibn Ismâ'îl al-Ju'fî, *Sahîh al-Bukhârî,* Istanbul 1413/1992, juzuu III.

Can Şefik, *Mesnevi Tercemesi*, (Istanbul, 1997).

al-Daylamî, Abû Shujâ' Shîrawayh ibn Shardâr al-Hamazânî, *al-Firdaws bi Ma'sûr al-Khitâb,* ed. El-Saîd ibn Basyûnî Zaglûl, Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah, Beirut 1986, juzuu V.

al-Dârakutnî, Abû al-Hasan 'Ali ibn 'Umar al-Bagdâdî, *al- Sunan,* ed. al-Sayyid 'Abdullah Hâshim Yamânî al-Adanî, Dâr al-Ma'rifah, Beirut 1386/1966, juzuu IV.

al-Dârimî, Abû Muhammad Abdullah, *al-Sunan*, Istanbul 1413/1992.

Ghazali, Abû Hâmid, *al-Munqiz min al-Dalâl*, (Beirut, 1988).

al-Harawî, Abû Ismâîl 'Abdullah ibn Muhammed ibn 'Ali, *al-Arba'în fî Dalâil al-Tawhîd,* ed. Ali ibn Muhammad al-Faqîhî, al-Madînah al-Munawwarah 1404.

al-Hatîb al-Bagdâdî, Abû Bakr Ahmad ibn 'Ali, *Muwaddıh Awhâm al-Jam' va al-Tafrîq*, ed. 'Abdulmu'tî Amîn al-Kal'ajî, Dâr al-Ma'rifah, Beirut 1407, juzuu II.

al-Hatîb al-Bagdâdî, Abû Bakr Ahmad ibn 'Ali, *Târikhu Bagdâd,* Dâr al-Kutub al-'Ilmiyyah, Beirut, juzuu XIV.

al-Haythamî, 'Ali ibn Abî Bakr, *Majma' al-Zawâid wa Manba' al-Fawâid,* Dâr al-Rayyân li al-Turath-Dâr al-Kitâb al-'Arabî, Cairo-Beirut 1407, juzuu X.

al-Hâkim, Abû Abdillah Muhammad ibn Abdillah al-Naysâbûrî, *al-Mustadrak alâ al-Sahîhayn,* ed. Mustafa Abulkâdir'Atâ, Dâr al-Kutub al-'Ilmiyyah, Beirut 1411/1990, juzuu IV.

al-Humaydî, Abû Bakr 'Abdullah ibn al-Zubayr, *Musnad el- Humaydî,* (ed. HabîburRahmân al-A'zâmî), Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah & Maktabah al-Mutanabbî, Beirut-Cairo, juzuu II.

al-Khourasânî, Abû 'Uthmân Saîd ibn Mansûr, *Kitâb al-Sunan,* (ed. HabiburRahmân al-A'zâmî), al-Dâr al-Salafiyyah, al- Hind (India) 1982.

al-Kissî, Abû Muhammad 'Abd ibn Humayd ibn Nasr, al- *Musnad,* (ed. Subhî Badrî al-Sâmarrâî & Mahmûd Halîl al-Saîdî), *Maktabah al-Sunnah, Cairo 1408/1988.*

al-Marwazî, Abû 'Abdillah Muhammad ibn Nasr ibn al-Hajjâj, *al-Sunnah,* ed. Sâlim Ahmad al-Salafî, Muassasah al-Kutub al-Thaqâfiyyah, Beirut 1408.

al-Marwazî, Abû 'Abdillah Muhammad ibn Nasr ibn al-Hajjâj, *Ta'zîm Qadr al-Salât*, (ed. 'AbdurRahmân 'Abduljabbâr al-Farîwâî), Maktabah al-Dâr, al-Madînah al-Munawwarah 1406, juzuu. II.

al-Nabhânî, Yûsuf ibn Ismâ'îl, *al-Anwâr al-Muhammadiyyah min al-Mawâhib al-Ladunniyyah*, Dâr al-Îmân, Damascus 1405/1985.

al-Nasâî, Abû AbdirRahmân Ahmad ibn Shu'ayb, *al-Sunan (al-Mujtabâ)*, Istanbul 1413/1992, juzuu III.

al-Nasâî, Abû AbdirRahmân Ahmad ibn Shu'ayb, *al-Sunan al-Kubrâ*, ed. AbdurRahmân Suleiman al-Bundârî, Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah, Beirut 1411/ 1991, juzuu VI.

al-Qudâ'î, Abû Abdillah Muhammad ibn Salâmah ibn Ja'far, *Musnad al-Shihâb*, ed. Hamdî ibn Abdilmajîd al-Salafî, Muassasah al-Risâlah, Beirut 1407/1986, juzuu II.

al-Qurashî, Abû Bakr 'Abdullah ibn Muhammad, *Makârim al-Akhlâq*, ed. Majdî al-Sayyid Ibrahîm, Maktabah al-Qur'an, Cairo 1411/1990.

al-Qurtubî, Abû Abdillah Muhammad ibn Ahmad, *al-Jâmi' li Ahkâm al-Qur'ân*, ed. Ahmad 'Abdulalîm al-Barounî, Cairo, Dâr al-Sha'ab 1372, Juzuu XX.

al-Rabî ibn Habîb ibn 'Umar al-Azdî al-Basrî, *Musnad al-Rabî'*, ed. Muhammad Idrîs & 'Ashûr ibn Yousuf, Dâr al-Hikmah & Maktabah al-Istiqâmah, Beirut-Saltanah 'Ammân 1415.

al-San'ânî, Abû Bakr 'Abdurrazzâk ibn Hammâm, *Kitâb al-Mosannaf*, ed. Habîburranman al-A'zamî, al-Maktab al-Islâmî, Beirut 1403, juzuu XI.

al-Shâshî, Abû Saîd al-Haytham ibn Kulayb al-Shâshî, *Musnad al-Shâshî*, ed. Dr. MahfuzurRahmân Zaynullah, Maktabah al-Ulûm wa'l-Hikam, al-Madînah al-Munawwarah 1410, juzuu II.

al-Suyûtî, Jalâluddîn ‘AbdurRahmân, *Târîkh al-Khulafâ*, ed. Qâsım al-Shimâ’î & Muhammad al-’Uthmânî, Dâr al-Kalam, Beirut 1406/1986.

al-Tabarânî, Abû al-Kâsım Sulaymân ibn Ahmad, *al-Mu’jamal-Awsat*, ed. Târık ibn ‘Avadullah & Abdulmuhsin ibn Abraham al-Husaynî, Dâr al-Harâmayn, Cario 1415, juzuu X.

al-Tabarânî, Abû al-Kâsım Sulaymân ibn Ahmad, *al-Mu’jam al-Kabîr*, ed. Hamdî ibn ‘Abdilmajîd al-Salafî, Maktabah al-’Ulûm va al-Hikam, al-Mawsıl 1404/1983, juzuu XX.

al-Tahâwî, Abû Ja’far Ahmad ibn Muhammad bi Salamah, *Sharh Ma’ânî al-Âthâr*, ed. Muhammad Zuhrî al-Najjâr, Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah, Beirut 1399, juzuu IV.

al-Tayâlisî, Abû Dâwûd Suleiman ibn al-Jârûd al-Basrî, *al-Musnad*, Dâr al-Ma’rifah, Beirut.

al-Tirmidhî, Abû Îsâ Muhammad ibn Îsâ, *al-Sunan*, Istanbul 1413/1992, juzuu III.

al-Zahabî, Abû Abdillah Muhammad ibn Ahmad ibn ‘Uthmân, *Siyar A’lâm al-Nubalâ*, ed. Shu’ayb al-Arnaût, Muassasah al-Risalah, Beirut 1413, juzuu XXIII.

Hannâd ibn al-Sariy al-Kûfi, *al-Zuhd*, ed. ‘AbdurRahmân ‘Abduljabbâr al-Farîwâî, Dâr al-Hulafâ li al-Kitâb al-Islâmî, al-Kuwait 1406, juzuu II.

Ibn ‘Abdilbarr, Abû ‘Umar Yûsuf ibn ‘Abdillah al-Namarî, *al-Istî’âb fî Ma’rifah al-Ashâb*, ed. ‘Ali Muhammad al-Bajâwî, Dâr al-Jîl, Beirut 1412, juzuu IV.

Ibn ‘Abdilbarr, Abû ‘Umar Yûsuf ibn ‘Abdillah al-Namarî, *al-Tamhîd*, ed. Mustafa ibn Ahmad al-’Alawî & Muhammad ‘Abdulkabîr al-Bakrî, Vezarah ‘Umûm al-Awqâf, al-Magrib 1387, juzuu XXIV.

Ibn 'Adî, Abû Ahmad 'Abdullah ibn 'Adî ibn Muhammad al-Jurjânî, *al-Kâmil fi Du'afâ al-Rijâl,* ed. Yahyâ Muhtâr Gazâvî, Dâr al-Fikr, Beirut 1409/ 1988, juzuu VII.

Ibn Abî 'Âsım, 'Amr al-Dahhâk al-Shaybânî, *Kitâb al-Zuhd*, ed. 'Abdulalî 'Abdulhamîd Hâmid, Dâr al-Rayyân li al-Turath, Cairo 1408I.

Ibn Abî Âsım, 'Amr al-Dahhâk al-Shaybânî, *al-Sunnah,* ed. Muhammad Nâsıruddîn al-Albânî, al-Maktab al-Islâmî, Beirut 1400, juzuu II.

Ibn Abî Shaybah, Abû Bakr 'Abdullah ibn Muhammad ibn Abî Shaybah al-Kûfî, *al-Musannaf,* (ed. Kamâl Yousuf al-Hût), Maktabah al-Rushd, al-Riyâd 1409, juzuu. VII.

Ibn al-Jawzî, Abu al-Faraj AbdurRahmân ibn 'Ali ibn Muhammad, *Safwah al-Safwah,* ed. Mahmud Fâkhûrî & Muhammad Rawwâs Qal'ajî, Dâr al-Ma'rifah, Beirut 1399/1979, juzuu IV.

Ibn al-Kathîr, Abu al-Fidâ Ismâîl ibn 'Umar al-Qurashî al-Hâfız, *al-Bidâyah wa'n-Nihâyah,* ed. Fuâd al-Sayyid & 'Ali 'Abdussâtir, Dâr al-Kutub al-'Ilmiyyah, Beirut 1408/1988, juzuu VIII.

Ibn al-Mubârak, Abû 'Abdillah Abdullah ibn al-Mubârak ibn Wâdıh al-Marwazî, *al-Zuhd*, ed. HabiburRahmân al-A'zamî, Dâr al-Kutub al-Ilmiyyah, Beirut.

Ibn Hagar al-'Asqalânî, Abu al-Fadl Ahmad, *al-Isâbah fî Tamyîz al-Sahâbah,* (ed. 'Ali Muhammad al-Bajâwî, Dâr al-Jîl), Beirut 1412/1992, juzuu VIII.

Ibn Hagar al-'Asqalânî, Abu al-Fadl Ahmad, *Fath al-Bârî Sharh Sahîh al-Bukhârî,* ed. Muhammad Fuâd 'AbdulBâqî, Dâr al-Ma'rifah, Beirut 1379, juzuu XIII.

Ibn Hajar al-'Asqalânî, Abu al-Fadl Ahmad, *Lisân al-*

Mîzân, ed. Dâriah al-Ma'rif al-Nizâmiyyah-India, Muassasah al-A'lamî li al-Matbû'ât, Beirut 1406/1986, juzuu VII.

Ibn Hibbân, Abû Hâtim Muhammad ibn Hibbân ibn Ahmad al-Bustî, *al-Majrûhîn*, ed. Mahmûd Abraham Zâyed, Dâr al-Wa'y, Aleppo, juzuu III.

Ibn Hibbân, Abû Hâtim Muhammad ibn Hibbân ibn Ahmad al-Bustî, *al-Sahîh*, ed. Shu'ayb al-Arnaût, Muassasah al-Risâlah, Beirut 1414/1993, juzuu XVIII.

Ibn Hishâm, *al-Sîrah al-Nabawiyyah*, ed. Mustafa al-Saqqâ & Abraham al-Abyârî, Dâr Ibn Kathîr.

Ibn Ishâq, Muhammad ibn Yasâr, *al-Sîrah (Kitâb al-Mubtada' wa'l-Mab'ath wa'l-Magâzî)*, ed. Muhammad Hamîdullah, Hayra Hizmet Vakfı, Konya 1401/1981.

Ibn Khuzaymah, Abû Bakr Muhammad ibn Ishâq al-Sulamî, *al-Sahîh*, ed. Muhammad Mustafa al-A'zamî, al-Maktab al-Islâmî, Beirut 1390/1970, juzuu IV.

Ibn Mâjah, Abû Abdillah Muhammad ibn Yazîd al-Qazwînî, *al-Sunan*, Istanbul 1413/1992, juzuu II.

Ibn Sa'd, Abû Abdillah Muhammad ibn Sa'd ibn Manî'al-Basrî, *al-Tabaqât al-Kubrâ*, Dâr Sâdır, Beirut, juzuu VIII.

Imâm Mâlik, Abû Abdillah Malik ibn Anas al-Himyarî, *al-Muwatta'*, Istanbul 1413/1992.

Ma'mar ibn Râshid al-Azdî, *al-Jâmi'*, ed. Habîb al-A'zamî, al-Maktab al-Islâmî, Beirut 1403, juzuu II (kimechapishwa kama sehemu ya al-Musannaf ya al-San'ânî).

Muslim, Abu'l-Husayn Muslim ibn Hajjâj, *Sahîhu Muslim*, Istanbul 1413/1992, juzuu III.

Rûmî, Jalâladdin, *Mathnawî Ma'nawî*, (Tehran, 1378).

FOR FREE IN PDF FORMAT

ISLAMIC WORKS

YOU CAN DOWNLOAD IN PDF FORMAT

1350 BOOKS IN **60 LANGUAGES** FOR FREE

Islamic books in different languages are waiting
for you in PDF format at the web site
www.islamicpublishing.org

ERKAM PUBLICATIONS | islamicpublishing.org |